# Gethsemane

Akiwa pamoja na wanafunzi wake, Mwokozi, kwa taratibu, alielekea kwenye bustani ya Gethsemane. Mwezi wa pasaka, ukiwa dhahiri na kamili, uliangaza kutoka katika anga isiyo na mawingu. Mji mwenye mahema ya watu waliekwenda kuzuri mahali patakatifu ulitulia kimya.

Yesu alikuwa amezungumza na wanafunzi wake na kuwafundisha kwa bidii, lakini alipokaribia Gethsemane, alikuwa na kimya cha kushangaza. Mara nyingi alikuwa akifika eneo hili kwa ajili ya kutafakari nakuomba, lakini kamwe si kwa moyo uliojaa huzuni kama usiku huu wa mwisho wa maumivu makali. Katika maisha yake yote hapa duniani alikuwa ameembea katika nuru ya kuwepo kwa Mungu. Aliposhindana na watu waliovuviwa na roho ya shetani, aliweza kusema, "naye aliyenipeleka yu pamoja nami. Baba hakuniacha peke yangu, kwa sababu nafanya sikuzote yale yampendezayo" (Yoh. 8:29.) Lakini sasa alionekaa kutenwa na nuru ya kuwepo kwa Mungu iliyomtegemeza. Sasa alihesabiwa pamoja na wakosaji. Alipaswa kubeba hatia ya wanadamu wadhambi. Juu yake asiyejua dhambi lazima wekwe hatia yetu sisi sote. Dhambi inaonekana ya kuogofya sana kwake, uzito wa hatia anaopaswa kuubeba ni mkubwa sana, kiasi kwamba anajaribiwa kuhofia kuwa itamtenga milele nje ya upendo wa baba yake. Akihisi jinsi ilivyo ya kutisha ghadhabu ya Mungu dhidi ya uasi, aliwaambia "Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa."

Walipoikaribia bustani, wanafunzi waligundua mabadiliko yaliyompata Bwana wao. Kamwe hapo kabla awajawahi Kumwona akiwa na huzuni kuu na Kimya hivi. Alivyoendelea mbele, huzuni hii ya ajabu ilizidi; hata hivyo hawakuthubutu kumwuliza sababu. Umbo lake liliyumba kana kwamba angeanguka mara. Alipofika bustanini, wanafunzi kwa haraka walitafuta mahali pake pa kawaida pa kupumzika, ili Bwana wao apumzike. Kila hatua aliyopiga sasa ilikuwa ni kwa kujibidisha sana. Aliugua kwa sauti ya juu kana kwamba alikuwa katika maumib makali a mzigo wa kutisha. Mara mbili, wenzi wake walimsaidia, au sivyo angeanguka hata nchi.

Karibu na lango la bustani, yesu aliwaacha wanafunzi wote isipokuwa watatu, akawaagiza waombe kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili yake pia. Pamoja na Petro, Yakobo na Yohana, aliingia sehemu ya ndani ya faragha. Hawa wanafunzi watatu walikuwa wenzi wa karibu sana wa Kristo. Walikuwa wameuona utukufu wake katika mlima alipogeuka sura; waliwaona Musa na Eliya wakizungumza naye; waliisikia sauti toka mbinguni; sasa katika mashindano yake makuu, Kristo alitamani kuwepo kwao karibu naye. Mara nyingi walipitisha naye usiku katika mahali hapa salama pa faragha. Katika matukio hayo, walipokuwa wamemaliza kipindi cha kukesha na kuomba, walilala bila kubughudhiwa hatua chache kutoka kwa Bwana wao, hadi alipowaamsha asubuhi kwenda upya kazini. Lakini sasa aliwataka wakeshe naye kwa maombi. Hata hivyo hakustahimili kuwa waweze kushuhudia maumivu makali aliyopaswa kuhimili.

"Kaeni hapa," alisema "mkeshe pamoja nami." Akaendelea mbele kidogo, - siyo mbali sana, lakini ambapo wangeweza kumwona na kumsikia – na akaanguka kifudifudi hata nchi. Alihisi kuwa kwa ajili ya dhambi alikuwa akitenganishwa kutoka kwa Baba yake. Shimo lililowatenga lilikuwa kubwa sana, jeusi, lenye kina, kiasi kwamba roho yake ilitetemeka. Katika Maumivu haya makali hakupaswa kutumia uwezo wake wa

ungu ili kuyaepuka. Kama mwanadamu, lazima ateseke kwa matokeo ya dhambi za mtu. Kama mwanadamu lazima astahimili ghadhabu ya Mungu juu ya uasi.

Sasa Kristo alisimama kwa namna toauti na alivyokuwa akisimama kabla. Maumivu yake yanaweza kuelezwa vizuri kutumia naneno ya nabii "Amka, Ee Upanga, juu ya mchungaji wangu, na juu ya Mtu aliye mwenzangu, asema Bwana wa majeshi" (Zekaria 13:7.) Kama badala na dhamana kwa mdhambi, Kristo alikuwa anateseka chini ya haki ya Mungu, aliona kile haki ilichomaanisha. Hata sasa alikuwa mwombezi kwa ajili ya wengine; sasa alitamani awe na mwobezi kwa ajili yake mwenyewe.

Kristo alihisi kuwa umoja wake na Baba unavunjika, alihofia kwamba katika asili yake ya ubinadamu asingeweza kuvumilia vita vilivyokuwa vikimkabili na nguvu za gaza. Katika majaribu kule Jangwani hatima ya wanadamu ilikuwa hatarini. Kristo alikuwa ni mshindi. Sasa mjaribu alikuja kwa shindano la mwisho la kuogofya. Ka ajili ya shindano hili adui amekuwa akijiandaa kwa miaka mitatu ya huduma ya kristo. Kila kitu kwake kilikuwa hatarini. Kama akishindwa hapa, tumaini lake la ukuu litatoweka; falme zote za dunia hatimaye zitakuwa za kristo; yeye mwenyewe angeondolewa na kutupiliwa nje. Lakini Sasa Kristo akishindwa, dunia itakuwa ufalme wa Shetani na wanadamu wote wangekuwa chini ya uwezo wake milele. Huku akikabiliwa na shindano mbele yake, roho ha Kristo ilijawa na hofu ya kutengwa na Mungu. Shetani alimwambia kuwa kama angekuwa dhamana kwa ulimwengu wenye dhambi, utengano wake na Mungu ungekuwa wa milele. Angeshirikishwa na ufalme wa Shetani, na kamwe asingeuwa tena na Umoja na Mungu.

Ni nini kingepatikana kutokana na kafara hii? Jinsi gani ilionekana pasipo tumaini hatia na kukosa shukranikwa wanadamu! Katika hali hizi ngumu Shetani alishinikiza hali hiyo kwa Mkombozi: Watu wanaodai kufanikiwa zaidi ya wengine katika hali ya kimwili na kiroho wamekukataa. Wanatafuta kukuangamiza, uliye msingi, kiini na muhuri wa ahadi zote walizopewa kama watu pekee. Mmoja wa wanafunzi wako, aliyesikiliza mafundisho yako, na ambaye amekuwa kati ya wenye bidii kwa kazi za Kanisa, atakusaliti. Mmoja kati ya wafuasi wako wenye bidii atakukana. Wote watakuacha. Umbile zima la Kristo lilichukizwa na wazo hilo. Kwamba wale aliokusudia kuwaokoa, wale aliowapenda sana, wangeshiriki katika shauri baya la Shetani, hili liliumiza sana moyo wake. Pigano lilikuwa la kutisha. Kipimo chake kilikuwa hatia ya taifa lake, washitaki na wasaliti wake, hatia ya ulimwengu uliozama maovuni. Dhambi za wanadamu zilimlemea Kristo, na hisia ya ghadhabu ya Mungu juu ya dhambi iliseta uhai wake.

Mtazame akitafakari gharama ipaswayo kulipwa kwa ajili ya roho za watu. Katika maumivu yake makali anashikilia ardhi iliyopoa, kana kwamba kujizuia ili asitengwe zaidi na Mungu. Umade baridi was usiku ulianguka juu ya umbile lake lililolala chni, lakini hakuujali. Kutoka katika midomo yake iliyopauka kilitoka kilio cha uchungu, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Saa hiyo hiyo akaongeza kusema "Walakii si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe."

Moyo wa mwanadamu hutamani huruma ya wengine katika mateso. Tamaa hii kristo aliihisi kwa kina cha upeo kabisa cha umbile lake. Katika wakati wa maumivu makuu ya roho yake, anakuja kwa wanafunzi wake kwa hamu kubwa ya kusikia maneno fulani ya faraja kutoka kwa wale ambao mara kwa mara amewabariki na kuwafariji, na amewalinda katika huzuni na fadhaa. Yule ambaye daima alikuwa na maneno ya huruma kwao sasa alikuwa katika maumivu makuu yaliyo zaidi ya ubinadamu, na alitamani kujua

kuwa walikuwa wakiomba kwa ajili yake na wao pia, Jinsi gani ubaya wa dhambi ulionekana kama giza kuu! Lilikuwa la kutisha sana jaribu la kuwaacha wanadamy kubeba matokeo ya hatia yao, wakati akisimama bila hatia mbele za Mungu. Kama angejua tu kuwa wanafunzi wake walilielewa na kuthamini kujitoa kwake, basi angetiwa nguvu.

Aliinuka kwa jitihada yenye maumivu, na kwa kupepesuka alikwenda pale alipowaacha wanafunzi wake. Lakini "akawakuta wamelala." Kama angewakuta wanaomba, angeweza kutiwa moyo na kufarijika. Kama wangetafuta kimbilio kwa Mungu, ili mawakala wa Shetani wasipate ushindi juu yao, angeweza kufarijiwa na imani yao thabiti. Lakini hawakutee onyo hili lililorudiwarudiwa kuwa "kesheni na kuomba." Mwanzoni walifadhaika sana kumwona Bwana wao ambaye kwa kawaida ni mtulivu na mweny heshima, akishindana na huzuni iliyopita ufahamu. Walikuwa wameomba waliposikia kilio kikuu toka kwa bwana aliyekuwa akiteseka. Hawakukusudia kumwacha Bwana wao, lakini walikuwa kama wamepooza kwa kulewa, hali ambayo wangeweza kuiondoa kama wangedumu kumsihi Mungu. Hawakutambua umuhimu wa kukesha na maombi ya bidii ili kushinda majaribu.

Muda mfupi kabla ya kuelekea bustanini, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Ninyi nyote mtakunguwazwa kwa ajili yangu usiku huu." Walikuwa wamemthibitishia kuwa wako tayari kwenda naye gerezani na hata kifoni. Na maskini Petro, mwenye kujitumaini aliongeza "Hata wajapokunguwazwa wote, lakini siyo mimi" (Marko14:27, 29.) Walakini wanafunzi walijitegemea wenyewe. Hawakumwangalia msaidizi mweny nguvu kama Kristo alivyokuwa ameashauri kufanya. Hivyo wakati Mwokozi akihitaji sana huruma na maombi yao, walikutwa wamelala. Hata Petro alikuwa amelala.

Na Yohana, mwanafunzi mpendwa aliyeegama kifuani pa Yesu, alikuwa amelala. Hakika, upendo wa Yohana kwa Bwana wake ungepaswa kumfanya awe macho. Maombi yake ya bidii yangeungana na yale ya mwokozi wake mpendwa katika saa ya huzuni yake kuu. Mkombozi alitumia nyakati za usiku akiombea wanafunzi wake, ili imani yao isije ikashindwa. Kama sasa Yesu angewauliza Yakobo na Yohana swali alilowauliza kabla "Je, mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi na kubatizwa kwa ubatizo ninaobatizwa nao? Wasingethubutu kujibu "twaweza" (Mathayo 20:22.)

Wanafunzi waliamshwa na sauti ya Yesu, lakini ilikuwa vigumu kumtambua, uso wake ulikuwa umebadilika sana kutokana na uchungu moyoni. Akimwambia Petro, Yesu alisema "Simoni umelala wewe? Hukuweza kukesha saa moja? Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribune. Roho I radhi, lakini mwili ni dhaifu." Udhaifu wa wanafunzi uliamsha huruma ya Yesu. Aliogopa kuwa wsingeweza kuvumilia jaribu ambalo lingeapata kwa kusalitiwa kwake na kufa. Hakuwakemea, lakini alisema, "Kesheni ninyi na kuomba, msije mkaingia majaribuni." Hata katika maumivu yake makuu, alitafuta kusameheUdhaifu wao. "Roho kweli I radhi" alisema "laini mwili ni dhaifu."

Mara tena mwana wa mungu alishikwa na maumivu makuu zaidi ya uwezo wa kibinadamu, na kwa kuzimia na kuishiwa nguu kabisa, alipepesuka kuelkea mahali pale alipokuwa akiomba. Mateso yake yalikuwa makuu mno kuliko muda uliopita. Jinsi maumivu makuu yalivyomjia, "jasho lake likawa kama matone ya damu yakidondoka nchi." Misunobari na mitende ilishuhudia kwa kimya maumivu yake. Kutoka katika majani yake, ulidondoka umande mzito juu ya mwili wake, kana kwamba viumbe vya asili vililia juu ya muumba wao kushindana peke yake na nguvu za giza.

Muda mfupi kabla, Yesu alisimama kama mwerezi wenye nguvu, akistahimili tufani ya upinzai ulioelekeza hasira yao kwake. Nia shupavu na mioyo iliyojawa na uovu na hila nyingi vilijaribu, bila mafanikio, kumchanganya na kumshinda. Alisimama mbele katika ukuu wa uungu kama Mwana wa Mungu. Sasa alikuwa kama unyasi uliopigwa na kupindishwa na dhoruba yenye hasira. Aliukaribia mwisho wa kazi yake kama mshindi, ambaye katika kila hatua alikuwa amepata shindi dhidi ya nguvu za giza. Kama mmoja aliyekwisha kutukuzwa, alidai umoja na Mungu. Kwa matamshi yasiyo na makosa alitoa nyimbo za sifa. Alikuwa ameongea kwa wanafunzi wake maneno ya ujasiri na upole. Sasa ulikuja wakati wa nguvu za giza. Sasa sauti yake ilisikiwa katika upepo tulivu wa usiku, si kwa namna ya shangwe, lakii iliyojaa maumivu makuu ya kibinadamy. Maneno ya Mwokozi yalifika masikioni mwa wanafunzi waliolemewa na usingizi akisema "Baba yangu, kama haiwezekani kikombe hiki kiniepuke, kame nikikinywea, Mapenzi yako yatimizwe."

Nia ya kwanza ya wanafunzi ilikuwa kwenda kwake; lakini alikuwa amewaamuru wangoje pale, wkikesha na kuomba. Yesu alipokuja kwao, aliwakuta bado wamelala. Kwa mara nyingine tena alihisi hitaji la kuwa na rafiki, alitamani maneno machache kutoka kwa wanafunzi wake ambayo yangeleta faraja, na kuvunja mvuto wa giza ambalo karibu lingemzidi nguvu. Lakini macho yao yalikuwa mazito; "wala hawakujua wamjibu nini." Kuwepo kwake kuliwaamsha. Waliona uso wake ukiwa na jasho la damu lililotokana na maumivu makali, nao wakajawa na woga sana. Maumivu yake ya akili, hawakuweza kuyafahamu. "Uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wanadamu" (Isaya 52:14.)

Alipowaacha, Yesu alirudi mahali pake, na kuanguka kifudifudi, kwa kuzidiwa na kitisho cha giza kuu. Ubinadamu wa Mwana wa Mungu ulitetemeka katika saa hiyo ya majaribu. Sasa hakuomba kwa ajili ya wanafunzi wake ili imani yao isitindike, bali aliomba kwa ajii ya roho hake iliyojaribiwa na yenye maumibu makuu. Wakati wakutisha ulikuwa umewadia – wakati ambao ungeamua hatima ya ulimwengu. Ajali ya wanadamu ilitetemeka kwenye mizani. Hata sasa bado Kristo angeweza kukataa kukinywea kikombe walichopewa wanadamu wadhambi. Bado alikuwa hajachelewa. Angeweza kupangusa lile jasho la damu kutoka usoni pake, na kumwacha mwanadamu aangamie katika uovu wake. Angeweza kusema, hebu mwasi apokee adhabu ya dhambi zake, nami nitarudi kwa Baba yangu. Je, Mwana wa Mungu atakinywea kikombe kiki kichungu cha kufedhehesha na chenye maumivu makuu? Yeye asiye na hatia atateseka kwa matokeo ya laana ya dhambi, kumwokoa mwenye hatia? Kwa kutetemeka maneno yalitoka kwenye midomo iliyopauka ya Yesu, "Baba yangu, kama kikombe hiki kisiponiepuka, nikikinywea, mapenzi yako yatimizwe."

Baada ya kufanya uamuzi, alianguka katika hali ya kufa katika ardhi aliyokuwa amejaribu kuinuka. Wako wapi sasa wanafunzi wake, ili kuweka kwa huruma mikono yao chini ya kichwa cha Bwana wao anayezimia, na kuosha uso, ule ulioharibika kuliko wana wa watu? Mwokozi alikanyaga shinikizo peke yake, na katika watu hakuna aliyekuwa pamoja naye.

Lakini Mungu aliteseka pamoha na Mana wake. Malaika waltazama maumivu ya Mwokozi. Walimwona Bwana wao akiwa amezingirwa na vikose vya majeshi ya Shetani, asili yake ilielemewa na mtetemo wa hofu ya ajabu. Kulikuwa na kimya mbingyi. Hakuna kinubi kilichoguswa. Laiti kama wanadamu wangeona mshangao wa jeshi la malaika katika kimya cha huzuni walipotazama Baba akitenga miali yake ya

nuru, upendo na utukufu kutoka kwa Mwanawe mpendwa, wangeweza kutambua vizuri zaidi jinsi dhambi ilivyo ya kuchukiza mbele zake.

Dunia ambazo hazikuasi na malaika wa mbinguni walikuwa wameangalia kwa makkini sana kadri pagano lilivyokaribia mwisho wake. Shetani na muungano wake wa uovu, majehi ya uasi, waliangalia kwa bidii saa hii muhimu katika kazi ya ukombozi. Nguvu za wema na uovu zilingoja kuona ni jibu gani litakuja kwa ajili ya ombi la Kristo lililoridiwa mara tatu. Malaika walitamani kuleta msaada kwa huyu mtesekaji wa kiungu, lakini hili haliwezi kufanyia. Hakuna njia ya kukwepa iliyopatikana kwa ajili ya Mwana wa Mungu. Katika kipeo hiki cha kutisha, wakati kila kitu kilikuwa hatarini, wakati kikombe cha siri kilipotetemeka mikononi mwa Mwokozi, mbingu zilifunguka, nuru ikaangaza kati ya giza la saa hii muhimu, na malaika mwenye nguvu asimamaye mbele za Mungu, anayeshikilia nafasi ambayo Shetani alianguka, alikuja upande wa Kristo. Malaika hakuja kuondoa kikombe mikononi mwa Kristo, lakini ili kumtia nguvu kukinywea, pamoja na uthibitisho wa upendo wa Baba. Alikuja kumpa nguvu aliye kafara ya kiungu – kibinadamu. Alimwonyesha mbingu zilizo wazi, akimweleza huhusu roho zitakazookolewa kama matokeo ya mateso yake. Alimhakikishia kuwa Baba yake ni mkuu na mwenye nguvu kuliko Shetai, Kwamba kifo chake kitasababisha kuchanganyikiwa kabisa kwa Shetani, na kuwa falme za dunia hii watapewa watakatifu wake Aliye juu. Alimwambia kuwa ataona matunda ya taabu ya nafsi yake na kuridhika, maana ataona makutano makubwa ya watu waliokombolewa, wamekombolewa milele.

Maumivu makali ya Kristo hayakukoma, lakini huzuni na kukata tamaa vilimuacha. Dhoruba haikupungua nguvu kwa namna yoyote, lakini yule aliyekuwa lengo, alitia nguvu kukabili ghadhabu yake kali. Alitoka akiwa mtulivu na shwari. Amani ya mbinguni ilitulia katika uso wake uliokuwa na madoa ya damu. Alistahimili kile ambacho hakuna mwanadamu ambaye angeweza kustahimili, naana alionja mateso ya mauti kwa ajili ya kila mtu.

Wanafunzi waliokuwa wamelala waliamshwa ghafla na nuru iliyomzunguka Mwokozi. Walimwona malaika ameinama kwa Bwana wao aliyeanguka kifudifudi. Walimwona akiinua kichwa cha mwokozi kifuani pake, na kuelekeza mbinguni. Waliisikia sauti yake, kama muziki mtamu, akitamka maneno ya faraja na matumaini. Wanafunzi walikumbuka tukio katika mlima alipobadilika sura. Walikumbuka utukufu uliomzunguka hekaluni, na sauti ya Mungu iliyotoka katika wingu. Sasa utukufu uleule ulidhihirishwa tena, na hawakuwa na woga zaidi kwa Bwana wao. Alikuwa chini ya utunzaji wa Mungu; malaika mwenye nguvu alikuwa ametumwa kumlinda. Kwa mara nyingine tena wanafunzi katika uchovu wao wakakubali kuzidiwa na hali ya kuzimia. Yesu akawakuta tena wamelala.

Akiwaangalia kwa huzuni alisema “laleni sasa, mpumzike, tazama saa imekaribia, na Mwana wa Adamu anatiwa katika mikono ya wenye dhambi.”

Hata alivyokuwa akisema hayo maneno, alisikia vishido vya kundi la watu waliokuwa wakimtauta na akasema “Ondokeni, twende zetu; tazama yule anayenisaliti amekaribia.”

Hakukuwa na dalili yoyote ya maumivu yake ya awali yaliyoonekana wakati Yesu alipotembea kukutana na msaliti wake. Akisimama mbele ya wanafunzi wake alisema "“i nani mnayemtafuta?” Nao wakamjibu “Ni Yesu Mnazareti.” Yesu akawaambia “Ni mimi.” Maneno haya yalipokuwa yakisemwa, malaika yue aliyemhudumia Yesu alisimama kati yake na lile kundi la watu waliokuja kumkamata. Nuru ya uungu iliangaza uso wa Mwokozi, na umbile kama la hua likamfunika. Mbele ya utukufu huu

wa kiungu, kundi hili la wauaji hawakuweza kusimama hata kwa muda mfupi. Walipepesuka na kurudi nyuma. Makuhani, wazee, maaskari na hata Yuda, walianguka chini kaa wafu.

Malaika akatoweka, na ile nuru ikapotea. Yesu alikuwa na nafasi ya kutoroka, lakini alibaki palepale, akiwa mtulivu na mwenye kujitawala. Kama aliyetukuzwa alisimama kati ya kundi hili kaidi, lililoanguka chini, bila msaada miguuni pake. Wanafunzi waliangalia, wakiwa kimya kwa mshangao na hofu.

Lakini ghafla sura ya mambo ilibadilika. Lile kundi liliamka. Maaskari wa kirumi, makuhani na Yuda walimkaribia Kristo. Walionekana kuaibika kwa udhaifu wao, na kuogopa kuwa huenda angeweza bado kutoroka. Swali liliulizwa tena na Mkombozi "Ni nani mnayemtafuta?" Walikuwa wamepata ushahidi kuwa aliyesimama mbele yao ni Mwana wa Mungu, lakini hawakukubali kusadikishwa. Kwa swali, "Ni nani mnayemtafuta?" walijibu tena "Ni Yesu Mnazareti." Ndipo Mwokozi akasema "Nimekwisha kuwaambieni ya kwamba ni mimi: basi ikiwa mnanitafuta mimi, wwcheni hawa waende zao," akielekeza kwa wanafunzi wake. Alijua jinsi gani imani yao ilikuwa dhaifu, na alitafuta kuwaepusha na majaribu na taabu. Kwa ajili yao alikuwa tayari kujitoa kafara mwenyewe.

Yuda msaliti hakusahau sehemu ambayo angefanya. Lile kundi lilipoingia bustanini, aliongoza njia, akifuatiwa kwa karibu na Kuhani Mkuu. Kwa wale waliomtafuta Yesu aliwapa ishara, akisema "nitakayembusu, huyo ndiye, mkamateni" (Mathayo 26:48.) Sasa alijifaya kama hanashirika nao. Alimkaribia Yesu na kushika mkono wake kama wa rafiki mzoefu. Kwa maneno "Salaam Bwana," akimbusu mara kadhaa, na kuonekana akilia kana kwamba alimhurumia katika hatari yake.

Yesu akamwambia, "Rafiki, kwa hiyo umekuja?" Sauti yake ilitetemeka kwa huzuni alipoongeza kusema "Yuda, wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?" Lalamiko hili lingeweza kuamsha dhamiri ya msaliti, na kugusa moyo wake mzito; Lakini heshima, uaminifu, na huruma ya ubinadamu vilikuwa vimemwacha. Alisimama bila kuona haya na kutaka shari, bila kuonyesha moyo wa kuacha kusudi lake baya. Alijitoa kwa Shetani, na hakuwa na uwezo wa kumpinga. Yesu hakukataa busu la msaliti.

Lile kundi lilipata ujasiri walipomwona Yuda akimshika Mtu ambaye si muda mrefu uliopita alitukuzwa mbele yao. Sasa walimkamata Yesu, na kufunga ile mikono ya thamani ambayo daima ilitumika kutenda mema.

Wanafunzi walifikiri kuwa Bwana wao hatakubali achukuliwe. Maana uwezo ule uliofanya wale wauaji waanguke kama wafu, ungeweza kuwafanya wabakie hali hiyo hiyo bila msaada, hadi Yesu na wenzake watoroke. Walisikitishwa sana na kuona uchungu walipoona kamba zikiletwa mbele ili kufunga mikono yake yeye waliyempenda. Petro kwa hasira alitoa upanga wake na kujaribu kumlinda Bwana wake, lakini alikata tu sikio la mtumishi wa Kuhani Mkuu. Yesu alipoona kilichofanyika, alifungua mikono yake ijapokuwa ilishikiliwa kwa nguvu na maashari wa Kirumi, na kusema "Mwe radhi kwa hili," aligusa sikio lililojeruhiwa, na mara moja lilipona. Halafu akamwambia Petro, "Rudisha upanga alani mwake; maana wote waushikao upanga wataangamia kwa upanga. Ama wadhani mimi siwezi kumsihi Baba yangu naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?" – jeshi moja badala ya kila mwanafunzi mmoja. Ee, kwa nini hajiokoi mwenyewe na sisi? waliwaza wanafunzi. Akijibu mawazo yao yasiyotamkwa, aliongeza "Yatatimizwaje basi maandiko, ya kwamba hivyo ndivyo ilivyopasa kujiri?" "Kikombe alichonipa Baba nisikinywee?"

Heshima kuu ya viongozi wa Kiyahudi, haikuwazuia kujiunga kumtafuta Yesu. Kukamatwa kwake lilikuwa jambo muhimu sana ambalo lisingeweza uachwa mikononi mwa viongozi wa chini, Makuhani na wazee wajanja walijiunga na mapoisi wa hekalu na watu wengi wakifanya ghasia wakimfuata Yuda kwenda Gethsemane. Kundi la jinsi gani kwa hawa viongozi wa dini kuungana nalo – kundi lililokuwa na bidii ya msisimko, na wenye silaha za vifaa vyote, kana kwamba walikuwa wakifukuza mnyama ya porini.

Akiwageukia makuhani na wazee, Kristo aliwakazia jicho lake la uchunguzi. Maneno aliyoyasema, kamwe hawatasahau siku zote za maisha yao. Yalikuwa kama mishale mikali ya Mwenyezi. Kwa mamlaka alisema: "Je, mmekujawenye panga na marungu kama kumkamata mnyang'anyi? Kila siku nilifundisha hekaluni. Mlikuwa na kila nafasi ya kunikamata, lakini hamkufanya lolote. Usiku unafaa sana kwa kazi yenu. "Hii ndiyo saa yenu na mamlaka ya giza."

Wanafunzi walitishika sana walipoona Yesu akiruhusu achukuliwe na kufungwa. Walichukizwa kwamba alikubali kudhalilishwa hivi na wao pia. Hawakuelewa utendaji wake, na walimlaumu kwa kujiweka chini ya kile kikosi. Katika uchungu wao na hofu, Petro alipendekeza wajiokoe wenyewe. Kwa kufuata mawazo hayo "wote walimwacha, wakakimbia." Lakini Kristo alikuwa ametabiri juu ya utoro huo. "Angalia" alisema "saa inakuja, na sasa hivi ipo, ambapo mtatawanyika kila mmoja kwao na kuniacha mimi peke yangu; walakini mimi si peke yangu, kwa kuwa Baba yupo pamoja nami" (Yohana 16:32.)

# Mbele Ya Anasi na Baraza la Kayafa

Juu ya kijito cha Kidroni, kupitia bustani na Vichaka vya mizeituni, na kati ya mitaa iliyo kimya ya mji uliolala, walimharakisha Yesu. Ilikuwa zaidi ya usiku wa manane na makelele ya kundi hili lenye kuzomea lililomfuata zilisikika kwa ukali katika anga iliyotulia. Mwokozi alifungwa na kulindwa kwa karibu, na alitembea kwa maumivu. Lakini kwa shauku ya haraka watekaji wake walipita naye hadi katika jumba la Anasi, Kuhani Mkuu aliyemaliza muda wake.

Anasi alikuwa ndiye kiongozi wa familia ya kikuhani iliyokuwa ikihudumu, na kwa kuheshimu umri wake alitambuliwa na watu kama kuhani mkuu. Ushauri wake ulitafutwa na kutekelezwa kama sauti ya Mungu. Lazima amwone kwanza Yesu mateka wa nguvu za kikuhani. Lazima awepo katika kuanza kumhoji mfungwa, kwa hofu kuwa Kayafa asiyekuwa na uzoefu wa kutosha anaweza kushindwa kupata kusudio waliokuwa wakitafuta. Mbinu zake za kijanja, werevu na hila nyingi lazima zitumike wakati huu; maana katika matukio yote kuhukumiwa kwa Kristo lazima kupatikane.

Kristo ilikuwa ahukumiwe kwa kawaida mbele ya Sanhedrini, lakini mbele ya Anasi alikabiliwa na hukumu ya awali. Chini ya utawala wa kirumi, baraza la Sanhedrini halingeweza kutoa adhabu ya kifo. Wangeweza tu kumhoji mfungwa na kutoa hukumu, ambayo ingeidhinishwa na mamlaka ya Kirumi. Hivyo ilikuwa muhimu uleta dhidi ya Kristo mashitaka ambayo yangeonekana ni ya uvunjaji sheria kwa Warumi. Lazima pia mashitaka yapatikane yatakayomtia hatiani kwa wayahudi. Wengi miongoni mwa makuhani na watawala walikuwa wamesadikishwa na mafundisho ya Kristo, na ni hofu tu ya kutengwa iliyowazuia wasimkiri. Makuhani walikumbuka visuri swali la Nikodemo, "Je, torati yetu humhukumu mtu kabla ya kumsikia kwanza au kujua atendavyo?" (Yohana 7:51.) Swali hili kwa wakati huo lilivunja baraza, na kuzuia mipango yao. Yusufu wa Arimathayo na Nikodemo hawakupewa mwaliko wakati huu, lakini kulikuwa na wengine walioweza kuzungumza kutetea haki. Hukumu lazima ifanyike kwa namna itakayounganisha wajumbe wa Sanhedrini dhidi ya Kristo. Kulikuwa na mashitaka mawilli ambayo makuhani walikusudia kuyadimisha. Kama Yesu atathibitishwa kama mtu aliyekufuru, atahukumiwa na Wayahudi. Kama akipatikana na hatia ya uchochezi, itasababisha kuhukumiwa kwake na Warumi. Shitaka la pili Anasi alijaribu kwanza kulianzisha. Alimwuliza Yesu kuhusu wanafunzi wake na mafundisho yake, akitumaini mfungwa atasema kitu kitakachompatia kitu cha kufanyia kazi. Alifikiria kupata kauli kadhaa za kuthibitisha kuwa alitaka kuanzisha jumuiya ya siri, yenye kusudi la kuanzisha ufalme mpya. Halafu makuhani wangemkabidhi kwa Warumi kama mtu anayevuruga amani na kuanzisha maasi juu ya Serikali.

Kristo alisoma kusudi la kuhani kama kitabu kilicho funuliwa, kana kwamba anasoma roho ya ndani kabisa ya yule aliyemhoji, alikana kuwa kati yake na wafuasi wake kulikuwa na muunganiko wa siri, au kwamba aliwakusanya kwa siri na gizani ili kuficha mipango yake. Hakuwa na siri kuhusiana na makusudi au mafundisho yake. "Niliongea

wazi kwa ulimwengu" alijibu; "Dama nilifundisha katika masinagogi na katika hekalu, mahali wakutanikapo Wayahudi," wala sikusema lolote kwa siri."

Mwokozi alitofautisha namna alivyofanya kazi na taratibu za wale waliomshitaki. Kwa miezi kadhaa walimtafuta, wakifanya bidii kumnasa na kumleta mbele ya baraza la hukumu, mahali ambapo wangeweza kupata kwa kusema uongo, kile ambacho isingewezekana kupata kwa njia halali. Sasa walikuwa wanatimiza kusudi lao. Kukamatwa usiku na kundi la watu, kuzomewa na kunyanyaswa kabla hajatiwa hatiani na hata kushitakiwa, ilikuwa namna yao ya kufanya kazi na siyo yake. Vitendo vyao vilikuwa vya uvunjaji sheria. Kanuni zao wenyewe zilisema mtu anapaswa kutendewa kama si mkosaji hadi pale atakapo thibitishwa kuwa na hatia. Kwa kanuni zao wenyewe makuhani walisimama wamehukumiwa.

Akimgeukia yule aliyekuwa akimhoji, Yesu alisema, "Kwa nini kuniuliza mimi? Je, makuhani na watawala hawakutuma wapelelezi ili kufuatilia nyendo zake, na kuripoti kila neno? Je, hawakuwepo katika kila kusanyiko la watu, na kuwapelekea makuhani taarifa ya yote aliyosema na kutenda? Waulize wale walionisikia, ni nini niliyowaambia," Yesu alijibu; "tazama wanajua niliyoyasema."

Anasi alinyamazishwa na uamuzi wa majibu. Kwa kuogopa kuwa Kristo angesema jambo kuhusu mwenendo wake ambalo alipendelea liwe siri, hakusema neno zaidi kwake kwa wakati huo. Mmoja wa wasaidizi wake, akiwa amejawa hasira kwa kuona Anasi amenyamazishwa, alimpiga Yesu usoni, akisema, "wewe unamjibu hivyo kuhani mkuu?"

Kristo alijibu kwa utulivu, "kama nimesema vibaya, ushuhudie ule ubaya, bali kama nimesema vema, wanipigia nini?" Hakutamka maneno yeyote makali yakulipiza kisasi. Jibu lake tulivu lilitoka katika moyo usio na dhambi, mvumilivu na mpole usioweza kukasirishwa.

Kristo aliumia sana kwa kuchalilishwa na matukano. Mikononi mwa viumbe alivyoviumba, na ambao kwa ajili yao alikuwa anatoa kafara isiyo kifani, alipokea kila aina ya ufidhuli. Na aliteseka kwa kulinganisha ukamilifu wa utakatifu wake na chuki yake dhidi ya dhambi. Kujaribiwa kwake na watu waliotenda kama mashetani ilikuwa kwake kafara ya kudumu. Kuzungkukwa na wanadamu waliotawaliwa na Shetani ilikuwa chukizo kwake. Na alijua kuwa kwa mara moja, kwa kudhihirisha uwezo wake wa Uungu, angewalaza watesaji wake mavumbini. Hii ilifanya jaribu liwe gumu sana kustahimili.

Wayahudi walitazamia Masihi kudhihirishwa kwa mwonekano wa nje. Walimtazamia kuwakwa mng'ao mmoa tu mkuu wa mapenzi yake, kubadilisha mwelekeo wa mawazo ya watu, na kuwalazimisha kuikubali mamlaka yake. Hivyo waliamini, angejipatia kutukuzwa, na kutosheleza tamaa yao ya kuwa maarufu. Hivyo Kristo alipotendewa kwa dharau, lilimjia jaribu la nguvu sana kudhihirisha tabia yake ya Uungu. Kwa neno, kwa mtazamo, angeweza kuwalazimisha watesi wake kukiri kuwa alikuwa Bwana juu ya wafalme na watawala, makuhani na hekalu. Lakini lilikuwa jukumu lake gumu kudumu katika nafasi aliyokuwa ameichagua kama mmoja pamoja na wanadamu.

Malaika wa mbinguni walishuhudia kila tendo dhidi ya kamanda wao waliyempenda. Walitamani kumwokoa Kristo. Chini ya Mungu, malaika ni wenye nguvu zote. Katika tukio moja, kwa kutii agizo la Kristo, waliangamiza katika jeshi la Waashuru katika usiku mmoja watu mia moja themanini na tano elfu. Ingekuwa rahisi jinsi gani, malaika, wakiangalia tukio hili la aibu la kuhukumiwa Kristo, kudhihirisha uchungu wao kwa kuwaangamiza maadui wa Mungu! Lakini hawakuamuriwa kufanya hivyo. Yeye

ambaye angeweza kuwaangamiza hata kifo maadui zake, alivumilia ukatili wao. Upendo wake kwa Baba yake, na ahadi yake tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu, kuwa mbeba-dhambi, vilimfanya kuvumilia bila manung'uniko, mabaya aliyotendewa na wale aliokuja kuwakomboa. Ilikuwa sehemu ya utume wake kuvumilia, katika hali yake ya ubinadamu, mizaha na mabaya yote ambayo watu wangeweka juu yake. Tumaini pekee la wanadamu lilikuwa katika kujidhili huku kwa Kristo kwa yale yote ambayo angeweza kuvumilia kutoka mikononi na mioyoni mwa watu.

Kristo alikuwa hajasema lolote ambalo lingewafaidia washitaki wake; lakini bado alikuwa amefungwa, kuonyesha kuwa alikuwa amehukumiwa hatia. Hata hivyo, lazima kuwe na kujifanya kutenda haki. Ilikuwa muhimu kuwa na aina ya mashitaka ya kisheria. Hili utawala ulidhamiria kuliharakisha. Walijua heshima ambayo Yesu alipewa na watu, na waliogopa kuwa kama kukamatwa kwake kungetangazwa hadharani, kungekuwa na jaribio la kumwokoa. Tena, kama kesi na kukata hukumu havitaharakishwa, kutakuwa na ucheleweshaji wa wiki kuhusiana na kusherehekea Pasaka. Hili lingeweza kuvunja mipango yao. Katika kutafuta kumtia Yesu hatiani walitegemea zaidi madai ya watu, wengi wao ghasia kwa Yerusalemu. Kama kungekuwa na ucheleweshaji kwa wiki, msisimko ungepungua nguvu, na hali iliyo kinyume kabisa ingeweza kutokea. Sehemu bora ya watu ingeamshwa kwa ajili ya kumsaidia Kristo; wengi wangejitokeza na ushahidi ili kumtetea, wakiweka wazi matendo makku aliyoyafanya. Hili lingechochea hasira ya umati dhidi ya baraza la Sanhedrini. Mashitaka yao yangelaumiwa, na Yesu kuachwa huru, kupokea heshima kuu kutoka kwa makutano. Makuhani na watawala, kwa hiyo, wakadhamiria kuwa kabla kusudi lao halijafahamika, Yesu lazima awe amekabidhiwa mikononi mwa Warumi.

Lakini jambo la kwanza, shitaka lazima lipatikane. Walikuwa bado hawajapata chochote hadi sasa. Anasi aliamuru Yesu apelekwe kwa Kayafa. Kayafa alikuwa miongoni mwa Masadukayo, ambao baadhi yao sasa walikuwa maadui wabaya mno wa Yesu. Yeye mwenyewe, ijapokuwa alipungukiwa nguvu ya kitabia, lakini alikuwa mkali, asiye na huruma, na asiye mwangalifu kama alivyokuwa Anasi. Angejaribu kila njia kumwangamiza Yesu. Ilikuwa sasa ni alfajiri na giza lilikuwa nene; kwa mwanga wa mienge na taa za mikononi kundi lenye silaha na mahabusu wao walielekea kwenye jumba la Kuhani Mkuu. Hapa, wakati wajumbe wa baraza la Sanherini walipokuwa wanakusanyika, Anasi na Kayafa walimhoji tena Yesu, lakini bila mafanikio.

Wakati baraza lilipokuwa limekusanyika katika ukumbi wa kuhukumia, Kayafa alikalia kiti chake kama afisa mkuu. Pande zote kulikuwa na waamuzi na hasa wale waliopendelea kesi. Maaskari wa Kirumi waliwekwa jukwaani chini ya kiti cha ufalme. Miguuni pa kiti hicho alisimama Yesu. Masho yote ya makutano yalielekezwa kwake. Msisimko ulikuwa mkali sana. Kati ya wote waliokuwepo pale ni Yeye tu alionekana mtulivu na mwenye amani. Hewa ya mahali iliyomzunguka ilionekana imeenea mvoto mtakatifu.

Kayafa alimhesabu Yesu kama adui yake. Hamu ya watu kumsikiliza Mwokozi, na utayari wao wa kupokea mafundisho yake, viliamsha wivu mkali sana wa kuhani mkuu. Lakini sasa Kayafa alipomtzama mfungwa, alivutiwa sana na ubora wa tabia na uvumilivu wake wa heshima. Alishawishika kuwa mtu huyu alihusiana na Mungu. Muda mfupi tu uliofuata alitupilia mbali wazo hilo kwa dharau. Mara moja sauti yake ilisikika kwa kicheko cha dharau, na sauti ya kiburi ikidai kwamba Yesu afanye mojawapo ya miujiza yake mikubwa mbele yao. Lakini maneno yake yalikuwa kana

kwamba hayakusikika masikioni mwa Mwokozi. Watu walitofautisha msisimko na tabia ya kudhuru wengine ya Anasi na Kayafa, na utulivu na uvumilivu mkuu wa Yesu. Hata katika fikra za haya makutano yenye mioyo migumu lilizuka swali, je, Mtu huyu mwenye mfano wa kuwepo kwa Mungu atahukumiwa kama mvunja sheria?

Kayafa, kwa kutambua mvuto uliokuwa ukienea, aliharakisha kesi. Maadui wa Yesu walikuwa katika fadhaa kuu. Walikuwa wamekusudia kumtia hatiani, lakini jinsi ya kutimiza hilo hawakujua. Idadi ya wana baraza iligawanyika kati ya Mafarasayo na Masadukayo. Kulikuwa na chuki kali na mashindano kati yao; baadhi walibishia hoja ambazo hawakutaka kuzikabili kwa kuhofia ugomvi. Kwa maneno macache Yesu angeweza kuchochea chuki ya wao kwa wao, na hivyo kugeuza hasira yao kutoka kwake. Kayafa alilijua hili, na alikusudia kuzuia kuamsha mabishano. Kulikuwa na mashahidi wengi kuthibitisha kuwa Kristo aliwasema vibaya Mmakuhani na waandishi, kwamba alikuwa amewaita wanafiki na wauaji; lakini ushahidi huu haukuwa shauri la kutanguliza. Masadukayo katika baadhi ya mabishano yao makali na Mafarisayo walitumia lugha hiyo hiyo kwao. Na ushahidi kama huo usingekuwa na uzito kwa Warumi, ambao walichukizwa na hali ya kujifanya ya Mafarisayo. Kulikuwa na ushahidi tele kuwa Yesu alikuwa amedharau desturi za wayahudi, na kuzungumza pasipo kuheshimu sheria zao nyingi; lakini kuhusiana na swala la desturi Mafarisayo na Masadukayo walikuwa kwenye hatua ya ncha ya upanga; na ushahidi huu pia usingekuwa na uzito kwa Warumi. Maadui wa Kristo hawakuthubutu kumshitaki kwa uvunjaji Sabato, isijekuwa mahojiano yakadhihirisha tabia ya kazi yake. Kama miujiza yake ya uponyaji ingefunuliwa wazi, kusudio la makuhani lingeshindwa.

Mashahidi wa uongo walipewa rushwa kumshitaki Yesu kwa kuchochea uasi na kutaka kuanzisha serikali iliyojitenga. Lakini ushahidi wao ulidhihirisha kuwa si dhahiri na ulipingana. Katika mahojiano waligeuza kauli zao wenyewe.

Manzoni katika huduma yake Kristo alisema "Livunjeni hili hekalu, nami katika siku tatu nitalijenga." Katika lugha mfano ya unabii, alikuwa ameeleza mauti na kufufuka kwake. "Alinena kuhusu hekalu la mwili wake" (Yohana 2:19, 21). Maneno hayo Wayahudi waliyatafsiri kikawaida, kana kwamba yalihusu hekalu la Yerusalemu. Katika yote aliyoyasema Kristo, makuhani hawakupata lolote la kutumia dhidi yake isipokuwa hili. Kwa kupindisha maneno hayo walitumaini kujipatia faida. Warumi walikuwa wameshiriki kujenga upya na kupamba hekalun na ni jambo waliloonea fahari kubwa; dharau yoyote ambayo ingeonyeshwa juu yake hakika ingechochea hasira yao. Hapa Warumi na Wayahudi, Mafarisayo na Masadukayo, walikutana; maana wote walilichukulia hekalu kwa heshima kuu. Kwa hoja hii mashahidi wawili walipatikana ambao ushahidi wao haukupingana sana kama ulivyokuwa wa wengine. Mmoja wao aliyekuwa amepewa hongo ili kumshitaki Yesu, alitangaza "Huyu mtu alisema ninaweza kuliharibu hekalu la Mungu, na kulijenga katika siku tatu." Hivyo maneno ya Kristo yalipotoshwa. Kama yangeelezwa sawasawa kama alivyoyasema, yasingeweza kusababisha hukumu yake hata na baraza la Sanhedrini. Kama Yesu angekuwa mwanadamu wa kawaida kama walivyodai Wayahudi, madai yake yangeonyesha tu roho ya kujisifu isiyo na sababu, lakini yasingetafsiriwa kuwa ni kufuru. Hata yalivyopotoshwa na mashahidi wa uongo, maneno yake hayakuwa na chochote ambacho kingehesabika na warumi kuwa uvunjaji wa sheria uliostahili kifo.

Kwa subira Yesu alisikiliza ushahidi huo uliopingana. Hakutamka neno lolote la kujitetea. Hatimaye washitaki wake walitatanika, wakachanganyikiwa, na kuingiwa

wazimu. Kesi ilikuwa haina maendeleo yoyote; ilionekaana kuwa hila yao ingeshindwa. Kayafa alikata tamaa. Tegemeo moja la mwisho lilibakia; Kristo lazima alazimishwe kujihukumu mwenyewe. Kuhani mkuu alianza kutoka kitini pake pa hukumu, uso wake ukiwa umekunjamana kwa hasira, sauti yake na mwenendo vikionyesha wazi kuwa, laiti ingekuwa katika uwezo wake, angempiga chini mfungwa aliye mbele yake. "Hujibu Kitu?" alisema ghafla "Hawa wanakushuhudia nini?"

Yesu alinyamaza, "Alikuwa amedhulumiwa na kuteswa, wala hakufunua kinywa chake: aliongozwa kama mwanakondoo aendaye machinjoni, na kama kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake, hakufunua kinywa chake" (Isaya 53:7).

Hatimaye, Kayafa akiinua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni, alimwambia Yesu katika hali ya kumwapisha: "Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu."

Kwa ombi hili Kristo asingebakia kimya. Kulikuwa na wakati wa kukaa kimya, na wa kusema. Hakuzungumza hadi alipoulizwa moja kwa moja. Alijua kuwa kujibu sasa kungehakikisha kifu chake. Lakini rufani hii ilitolewa na mamlaka ya juu inayokubalika kitaifa, na kwa jina la Aliye juu kupita wote. Kristo asingeshindwa kuonyesha heshima inayostahili kwa sheria. Zaidi ya hayo, uhusiano wake binafsi na Baba ulitiliwa mashaka. Lazima atangaze wazi tabia yake na utume wake. Yesu aliwaambia wanafunzi, "Yeyote atakayenikiri mbele ya watu, mimi nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 10:32). Sasa kwa kielelezo chake mwenyewe alirudia fundisho hilo.

Kila sikio lilitegwa kusikiliza, kila jicho likakazwa usoni pake alipojibu, "wewe wasema." Nuru ya kimbingu ilionekana kuangaza uso wake alipoongeza kusema, "Lakini nawaambieni, tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni."

Kwa kitambo uungu wa Kristo uliangaza kupitia ubinadamu wake. Kuhani mkuu alinywea kwa hofu mbele ya macho yenye kupenya hadi ndani ya Mwokozi. Kule kutazama kulionekana kusoma mawazo yake yaliyofichika, na kuchoma moyoni mwake. Kamwe hakusahau ule mtupo wa jicho wenye kuchunguza ndani wa Mwana wa Mungu aliyekuwa akiteseka.

"Baadaye," Yesu alisema, "Mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, na akija juu ya mawingu ya mbinguni." Katika maneno haya Kristo alieleza kinyume cha tukio lililokuwa likiendelea. Yeye, Bwana wa uzima na utukufu, atakuwa ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Atakuwa mhukumu wa dunia yote, na kutokana na uamuzi wake hakutakuwa na kukata rufaa. Ndipo kila jambo la siri litawekwa katika nuru ya uso wa Mungu, na hukumu kutolewa juu ya kila mtu kulingana na matendo yake.

Maneno ya Kristo yalimshtusha kuhani mkuu. Wazo kuwa kungekuwa na ufufuo wa wafu, wakati wote watakaposimama mbele ya baraza la hukumu la Mungu, ili kulipwa sawasawa na kazi zao, lilikuwa wazo la utisho kwa Kayafa. Hakutaka kuamini kuwa wakati ujao mbele atahukumiwa sawasawa na kazi zake. Kwa haraka picha ya tukio la hukumu ya mwisho ilipita mawazoni mwake. Kwa muda alioa tukio la kutisha la makaburi kuwatoa wafu wao, na siri alizotumaini zilifichika milele. Kwa muda alihisi kama amesimama mbele za mwamuzi wa milele, ambaye macho yake ambayo huona kila kitu, yalikuwa yakisoma roho yake, yakifunua siri zilizodhaniwa kufichwa na wafu.

Tukio lilihama kutoka njozi ya kuhani. Maneno ya Kristo yalimchoma, kama Sadukayo, hadi moyoni. Kayafa alikana fundisho la ufufuo, hukumu na maisha yajayo. Sasa alitiwa wazimu na hasira ya kishetani. Mtu huyu, mfungwa mbele yake, atapinga

kwa nguvu nadharia zake anazozipenda sana? Akirarua vazi lake, ili watu waone kitisho chake cha kujifanya, alidai kuwa bila mambo mengine ya awali, mfungwa ahukumiwe kwa kikifuru. "Tuna haja gani tena ya mashahidi?" alisema, "Tazameni, sasa mmesikia hiyo kufuru yake, mwaonaje ninyi?" Na wote wakamhukumu.

Thibitisho la hatia ya kosa vikichanganyika na hasira vilimwongoza Kayafa kufanya alivyotenda. Alijikasirikia mwenyewe kwa kuamini maneno ya Kristo, na badala ya kutoa moyo wake chini ya hisia kali za ukweli, na kukiri kuwa Kristo alikuwa ndiye Masihi, alirarua mavazi yake ya ukuhani katika upinzani uliokusudiwa. Tendo hili lilikuwa na maana sana. Kayafa alielewa kidogo sana maana yake. Katika tendo hili, lililokusudiwa kushawishi waamuzi na kupata hukumu ya Kristo, kuhani mkuu alijihukumu mwenyewe. Kwa sheria ya Mungu alipoteza sifa za ukuhani. Alikuwa amejitangazia mwenyewe hukumu ya kifo.

Kuhani Mkuu hakupaswa kurarua mavazi yake. Kwa sheria ya walawi, hili lilikatazwa chini ya hukumu ya Kifo. Kwa jambo lolote, kwa tukio lolote kuhani hakupaswa kurarua vazi lake. Ilikuwa ni kawaida kwa baadhi ya wayahudi kurarua mavazi kwa dufiwa na rafii, lakini makuhani hawakutakiwa kushika mila hii. Agizo dhahiri lilitolewa na Kristo kwa musa kuhusu jambo hili. Walawi 10:6.

Kila kitu kilichovaliwa na kuhani kilipaswa kuwa kamili na bila ila. Kwa yale mavazi mazuri yaliyo rasmi iliwakilishwa tabia yake aliye halisi au kamili, Yesu Kristo. Si kingine isipokuwa ukamilifu, katika mavazi na mwenendo, katika maneno na roho, vingekubaliwa na Mungu. Yeye ni mtakatifu, na utukufu wake na ukamilifu lazima viwakilishwe na huduma ya duniani. Ni ukamilifu tu ungeweza kuwakilisha kwa usahihi utakatifu wa huduma ya mbinguni. Mtu aliye na mpaka angeweza kurarua moyo wake kwa kuonyesha roho ya unyenyekevu na upole. Hii Mungu ataitambua. Lakini hakuna kurarua ambako kungefaywa katika mavazi yakikuhani, kwani hili lingeharibu uwakilishi wa mambo ya mbingui. Kuhani mkuu aliyethubutu kuonekana katiak ofisi takatifu, na kushiriki katika huduma za Patakatifu, na vazi lililo raruliwa, aliangaliwa kama aliyejitenga kutoka kwa Mungu. Kwa kurarua mavazi yake alijitnga mwenyewe kuwa mwakilishi kielelezo. Hakukubaliwa tena na Mungu kama kuhani aliyehudumu. Tendo hili, kama lilivyoonyeshwa na Kayafa, lilionyesha hasira ya kibinadamu, na upungufu wa kibinadamu.

Kwa kurarua mavazi yake, Kayafa hakutii sheria ya Mungu kwa kufuata desturi za wanadamu. Sheria za kibinadamu ziliruhusu kuwa katika swala la kukufuru kuhani angeweza kurarua mavazi yake kwa hofu kwa hiyo dhambi na asiwe na hatia. Hivyo sheria ya Mungu ilihalifiwa na sheria za wanadamu.

Kila tendo la kuhani mkuu liliangaliwa kwa udadisi na watu; na Kayafa alifikiria matokeo, kuonyesha kujitoa kwake. Lakini katika tendo hili lililokusudiwa kuwa shitaka dhidi ya Kristo, alikuwa akimbeza yeye ambaye Mungu alisema, "Jina langu limo ndani yake" (Kutoka 23:21). Yeye mwenyewe alikuwa anafanya kufuru. Akisimama chini ya hukumu ya Mungu, alimhukumu Kristo kama mtu aliye kufuru.

Wakati Kayafa aliporarua mavazi yake, tendo lake liliashiria nafasi ambayo taifa la Kiyahudi lingekuwa nayo kama taifa mbele za Mungu, wakati ujao. Taifa lililopendelewa na Mungu lilikuwa likijitenga kutoka kwake na kwa upesi wakawa watu waliokataliwa na Mungu (Yehova). Wakati Kristo alipolia msalabani, "Imekwisha" (Yohana 19:30), na pazia la hekalu likararuliwa vipande viwili, Msimamizi Mtakatifu alitangaza kuwa Wayahudi walikuwa wamemkataa Yeye aliyekuwa halisi wa mifano

yao, na lengo la vivuli vyao. Israeli ilitalikiwa kutoka kwa Mungu. Hapo ndipo Kayafa angeweza kurarua mavazi yake rasmi, yaliyoashiria kuwa alidai kumwakilisha Kuhani Mkuu kabisa; maana tangu hapo hayakuwa tena na maana kwake wala kwa watu. Heri kuhani mkuu angerarua mavazi yake sasa kwa hofu kwa ajili yake mwenyewe na kwa taifa.

Baraza la Sanhedrini lilitangaza kuwa Kristo alistahili kifo; lakini ilikuwa kinyume na sheria ya Kiyahudi kuendesha kesi ya mfungwa usiku. Katika hukumu halali hakuna ambacho kingefanyika isipokuwa katika mwanga wa mchana na mbele ya kikao kamili cha baraza. Walakini, sasa Mwokozi alitendewa kama mhalifu aliyehukumiwan na kutolewa ili atendwe vibaya na upotovu wa binadamu. Jumba la kuhani mkuu lilizingira sehemu wazi ya baraza mahali maaskari na makutano walipokuwa wamekusanyika. Kupitia baraza hii Yesu alichukuliwa hadi chumba cha walinzi, kila upande akizomewa kwa madai yake kuwa ni Mwana wa Mungu. Maneno yake mwenyewe "ameketi mkono wa kuume wa nguvu" na "”akija katika mawingu ya mbinguni" yalirudiwa kwa dhihaka. Alipokuwa katika chumba cha walinzi akisubiri kesi ya kisheria, hakupewa ulinzi wowote. Umati usiojua kitu uliona ukatili aliotendewa mbele ya baraza, na kwa hio wakapata kibali kuonyesha hali yote ya Shetani iliyomo katika asili zao. Wema nwa Kristo na uvumilivu wake wa Kiungu uliwachochea na kuwa wazimu. Upole wake, kutokuwa na kosa, uvumilivu wake mkuu, uliwafana wawe na chuki iliyotoka wa Shetani. Rehema na haki vilikanyagwa chii. Kamwe mhalifu hakuwahi kutendewa kwa hali ya ukatili kama alivyotendewa Mwana wa Mungu.

Lakini maumivu makali yaliupasua moyo wa Yesu; pigo lililosababisha maumivu makali hakuna mkono wa adui ambao ungejaribu kupiga. Wakati akihojiwa kwa dhihaka mbele za Kayafa, Kristo alikanwa na mmoja wa wanafunzi wake.

Baada ya kumkimbia Bwana wao bustanini, wawili kati ya wanafunzi walidiriki kufuata, kwa mbali, kundi la watu waliomkamata Yesu. Wanafunzi hawa waliuwa na Petro na Yohana. Makuhani walimtambua Yohana kama mwanafunzi wa Yesu aliyefahamika sana, na aliruhusiwa kuingia ukumbini, kwa kutumaini kuwa kwa kushuhudia kudhalilishwa kwa kiongozi wake, angedharau wazo la kuwa huyo alikuwa Mwana wa Mungu. Yohana alimtetea Petro, na kufanya naye aruhusiwe kuingia ndani.

Ukumbini moto uliwashwa, maana ulikuwa wakati wa baridi wa usiku, muda ulio kabla ya mapambazuko. Kundi la watu liliukaribia moto, na Petro kwa kujiamini alikaa pamoja nao. Hakutaka kujulikana kama mwanafunzi wa Yesu. Kwa kujichanganya na umati pasipo uangalifu, alitumaini kwamba angechukuliwa kuwa mmoja wa wale waliomleta Yesu ukumbini.

Lakini Kadri mwanga ulivyoangaza uso wa Petro, Mwanamke aliyelinda mlango alimwangalia wa kumpeleleza. Alikuwa amemgundua kuwa aliingia na Yohana, aliona hali ya huzuni uson pake, na akafiiria kuwa atakuwa ni mwanafunzi wa Yesu. Alikuwa mmoja wa watumishi wa ngumba ya kayafa na alidadisi ili kujua. Alimwambia Petro "Wewe si mmoja wa wanafunzi wa mtu huyu?" Petro alishtushwa na kuchanganyikiwa; macho ya watu wote yalimwelekea. Alijifanya kana kwamba hakumwelewa; lakini aliendelea, na kuwaambia wale waliomzonguka kuwa mtu huyu alikuwa pamoja na Yesu. Petro alijisikia kulazimishwa kujibu, na akasema kwa hasira, "Mwanamke, mimi simjui." Hapa alimkana kwa mara ya kwanza na mara tu jogoo aliwika. Ewe Petro, mapema hivi unamwonea aibu Bwana wako! Mapema hivi kumkana Bwana wako!

Mwanafunzi Yohana, alipoingia kwenye ukumbi wa hukumu, hakujaribu kuficha ukweli kwamba alikuwa ni mfuasi wa Yesu. Hakujichanganya na kundi jeuri lililokuwa linamtukana Bwana wake. Yeye hakuulizwa maana hakutwaa tabia ya uongo, na hivyo kufanya aweze kushukiwa. Alitafuta pembe tulivu, ambapo asingeonekana kwa lile kundi, lakini karibu sana na Yesu kadri alivyoweza kuwa. Hapa angeweza kuona na kusikia yote yaliyotendeka katika kesi ya Bwana wake.

Petro hakukusudia kuwa tabia yake halisi ijulikane. Kwa kutwaa hali ya kutojali alikuwa amejiweka mwenyewe katika uwanja wa Shetani, na alikuwa mateka rahisi kwa majaribu. Kama angeliitwa kupigana kwa ajili ya Bwana wake, angekuwa askari jasiri; lakini wakati aliposondwa kidole cha dhihaka, alithibitisha kuwa mwoga. Wengi wasiorudi nyuma kutoka katika mapambano hai kwa ajili ya Bwana wao, hulazimishwa na dhihaka kukana imani yao. Kwa kuungana na wale wanaopaswa kuwaepuka, hujiweka katika ngia ya majaribu. Wanamkaribisha adui kuwajaribu, na kuwaongoza kusema na kutenda yale ambayo katika hali nyingine kamwe wasingekuwa na hatia. Mwanafunzi wa Kristo ambaye katika siku zetu huficha imani yake kwa hofu ya mateso au kushutumiwa anamkana Bwana wake kama vile Petro alivyofanya katika ukumbi wa hukumu.

Petro alijaribu kuonyesha hali ya kutotaka kujua kesi ya Bwana wake, lakini moyo wake ulisongwa na huzuni aliposikia masuto ya ukatili na kuona mateso mabaya aliyokuwa akipata. Zaidi ya hayo, alishangaa na kukasirika kwamba Yesu alijidhili hivi na wafuasi wake kwa kukubali kutendewa hayo. Ili kuficha hisia zake halisi, alijitahidi kujiunga na wale waliomtesa Yesu katika mizaha yao wakati usiofaa. Lakini kuonekana kwake kulikuwa si kwa kawaida. Alikuwa anafanya udanganyifu, na huku akitafuta kuongea bila kuhusika, hakuweza kuzuia kuonyesha uso wa hasira kwa ukatili uliotendwa kwa Bwana wake.

Usikivu ulielekezwa tena kwake kwa mara ya pili, na tena alishtakiwa kuwa mfuasi wa Yesu. Sasa alitangaza kwa kiapo, “simjui mtu huyu.” Bado alipewa nafasi nyingine. Saa nzima ilipita, mmoja wa watumishi wa kuhani mkuu, akiwa jamaa wa karibu wa yule mtu aliyekatwa sikio na Petro, alimwuliza “Je, mimi sikukuona wewe pamoja naye bustanini? Hakika wewe ne mmoja wao; maana u Mgalilaya wewe, na hata usemi wako wakutambulisha.” Kwa hili Petro alipata hasira kali. Wanafunzi wa Yesu walitambulikana kwa lugha yao safi, na ili kuwadanganya wale waliomhoji, na kuhalalisha tabia hii bandia, sasa Petro alimkana Bwana wake kwa kulaani na kuapa. Kwa mara nyingine jogoo aliwika. Petro akasikia, na akakumbuka maneno ya Yesu “Kabla jogoo hajawika mara mbili, utanikana mara tatu” (Marko 14:30).

Wakati kiapo hiki cha kudhalilisha kilipokuwa bado kibichi katika midomo ya Petro, na sauti nyembamba ya kuwika jogoo ikingali masikioni mwake, Mwokozi aligeuka toka kwa waamuzi waliochukia, na kumtazama huyu mwanafunzi maskini. Wakati huohuo macho ya Petro yalivutwa kwa Bwana wake. Katika uso ule wa upole alisoma huruma na huzuni, lakini hapakuwa na hasira pale.

Kuona uso ule uliopauka, na wenye kuteseka, midomo ile iliyotetemeka, ule mtazamo wa huruma na msamaha, vilichoma moyo wake kama mshale. Dhamiri iliamshwa. Kumbukumbu ilifanya kazi. Petro alikumbuka ahadi yake masaa machache yaliyopita kuwa atakuwa tayari kwenda na Bwana wake kifungoni na hata kifoni. Alikumbuka huzuni yake Mwokozi alipomwambia katika chumba kile cha juu kwamba atamkana Bwana wake mara tatu usiku ule. Petro ndipo tu alikuwa ametamka kwamba hamjui

Yesu, lakini sasa alitambua kwa uchungu sana jinsi gani Bwana wake alimjua vizuri, na ambavyo kwa usahihi alikuwa ameusoma moyo wake, udanganyifu uliokuwa haufahamiki hata kwake mwenyewe.

Wimbi la kumbukumbu lilipita juu yake. Rehema ya upole ya Mwokozi, wema na uvumilivu wake, huruma na subira yake kwa mwanafunzi wake mkosaji, - vyote vilikumbukwa. Alikumbuka tahadhari aliyopewa "Simoni, tazama, Shetai amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike…" (Luka 22:31, 32). Alitafakari kwa utisho kutokuwa na shukrani kwake, uongo, na kukosa msimamo. Kwa mara nyingine alimwangalia tena Bwana wake, na kuona mkono uliowekwa wakfu na kutumiwa vibaya ukiwa umeinuliwa ili kumpiga usoni. Kwa kushindwa kustahimili hali iliyokuwepo, kwa haraka, na moyo uliovunjika aliondoka ukumbini.

Aliendelea mbele katika upweke na giza, hakujua wala kujali ni wapi aendako. Hatimaye alijikuta Gethsemani. Tukio la masaa machache yaliyopita lilikuwa dhahiri akilini mwake. Uso wa mateso wa Bwana wake, ukiwa na alama za matone ya damu na kutikiswa na maumivu makali, vilikuwa mbele yake. Alikumbuka kwa uchungu mkuu kuwa Yesu alilia na kusihi katika maombi peke yake, wakati wale ambao wangeungana naye katika saa ile ya majaribu walikuwa wamelala. Alikumbuka agizo lake kuu "kesheni na kuomba, ili msije mkaingia majaribuni" (Mathayo 26:41). Alishuhudia tena matukio katika jumba la hukumu. Ilikuwa ni mateso kwa moyo wake ulioumia kujua kuwa ameongeza mzigo mzito katika kufedheheshwa na huzuni kwa Mwokozi. Mahali palepale Yesu alipoomba – katika maumivu makali, kwa Baba yake, Petro alianguka kifudifudi na kutamani kuwa afe.

Ilikuwa kulala wakati Yesu alimwamuru akeshe na kuomba ndiko Petro aliandaa njia kwa dhambi yake kuu. Wanafunzi wote, kwa kulala katika saa ile ya hatari, walipata hasara kubwa. Kristo alijua mateso makali ambayo wangeyapitia. Alijua jinsi ambavyo Shetani angefanya ili kuwatia ganzi hisia zao ili wasiwe tayari kwa majaribu. Kwa hiyo ndiyo maana aliwaonya. Kama yale masaa bustanini yangetumika kwa kukesha na kuomba, Petro asingeachwa kutegemea nguvu zake dhaifu. Asingemkana Bwana wake, Kama wanafunzi wangekesha na Kristo katika maumivu yake Makali, wangeandaliwa kuangalia mateso yake msalabani. Wangeweza kuelewa kwa kiasi fulani asili ya maumivu yake makali yazidiyo uwezo. Wangeweaza kukumbuka maneno yaliyotabiri mateso, kifo na kufufuka kwake. Kati ya huzuni ya saa hii ya majaribu, mionzi ya matumaini ingeangaza giza na kutegemeza imani zao.

Mara tu kulipopambazuka, baraza la Sanhedrini lilikutana tena, Yesu akaletwa tena ukumbini. Alikuwa ametangaza kuwa yeye ni Mwana wa Mungu, nao wakawa wamefasiri maneno yake kuwa mashtaka dhidi yake. Lakini hawakuweza kumhukumu kwa hilo, maana wegi wao hawakuwepo wakati wa usiku, na hivyo hawakusikia maneno yake. Na walijua kuwa baraza la Kirumi halitaona chochote katika maneno hayo kinachostahili kifo. Lakini kama kutoka kinywani mwake wangesikia maneno hayo yakirudiwa, kusudi lao lingepatikana. Madai yake kuwa ni Masihi yangefasiriwa kama ushawishi wa kisiasa.

"Wewe ndiwe Kristo?" Walisema, "tuambie." Lakini Kristo alibakia kimya. Lakini waliendilia kumbana kwa maswali. Hatimaye kwa sauti ya maombolezo ya huzuni, alijibu, "Nijapowaambia, hamtasadiki kabisa. Tena nikiwauliza, hamtajibu, wala

kuniachia huru.” Lakini ili wasipate udhuru aliongeza onyo la kutisha, “Tangu sasa Mwana wa Adamu atakuwa ameketi mkono wa kuume wa nguvu wa Mungu.”

“Basi wewe ndiwe Mwana wa Mungu?” Waliuliza kwa sauti moja. Akawaambia “Ninyi mwasema kwamba mimi ndiye.” Wakasema “Tuna haja gani tena ya ushuhuda? Maana, sisi wenyewe tumesikia maneno ya kinywa chake.”

Na hivyo kwa hukumu ya tatu ya mamlaka ya Kiyahudi Yesu alipaswa kufa. Kilichokuwa muhimu sasa, walifikiri, ilikuwa kwa Warumi kuidhinisha hukumu hii, na kumkabidhi mikononi mwao.

Baadaye likaja tukio la tatu la unyanyasaji na kuzomea, baya hata kuliko alilopata kwa umati usiojua kitu. Mbele ya makuhani na watawala, na kwa idhini yao, hili lilitendeka. Kila hisia ya huruma na utu vilitoweka mioyoni mwao. Kama hoja zao zilikuwa dhaifu, na hata zikashindwa kunyamazisha sauti yake, walikuwa na silaha nyingine, ambazo kwa miaka yote zimetumika kunyamazisha wazushi, - mateso na nguvu, na kifo.

Hukumu ya Yesu ilipotangazwa na waamuzi, hasira ya kishetani iliwajaa watu. Mvumo wa suti ulikuwa kama wa wanyama wa porini. Umati ulimsonga Yesu haraka wakisema, ana hatia, auawe! Kama sio maaskari wa Kirumi, Yesu asingeishi kufikia kupigiliwa msalabani. Angeraruliwa vipande mbele ya waamuzi wake, kama si mamlaka ya Warumi kuingilia kati, na kwa nguvu ya silaha kuzuia fujo za watu.

Watu wa Mataifa waliudhika kwa ukatili aliotendewa Yeye ambaye hakuna kilichothibitishwa dhidi yake. Maofisa wa kirumi walitangaza kuwa kwa kumhukumu Yesu walikuwa wanavunja sheria dhidi ya Mamlaka ya Rumi, na hata ilikuwa pia kinyume cha cheria ya kiyahudi kumhukumu mtu kifo kwa ushahidi wake mwenyewe. Kuingilia huku kulileta utulivu kwa kile kilichokuwa kinaendelea kwa kitambo, lakini viongozi wa Kiyahudi walikosa huruma na aibu.

Makuhani na watawala walisahau heshima ya ofisi yao, na walimnyanyasa Mwana wa Mungu kwa sifa mbaya. Walifanyia mzaha wazazi wake. Walitangaza kuwa madai yake ya kujitangaza kama Masihi yalifanya astahili kifo kibaya cha kudhalilisha. Watu wenye sifa ya ufisadi walishiriki katika unyanyasaji usio wa kawaida kwa mwokozi. Vazi kuukuu lilitupwa kichwani kwake, na watesi wake wakambiga usoni, wakisema “tabiri kwetu, ewe Kristo, ni nani aliyekupiga?” Vazi lilipoondolewa, mwovu mmoja maskini alimtemea usoni.

Malaika wa Mungu kwa uaminifu waliandika kila mtazamo, neno au tendo la dhihaka dhidi ya amiri wao mpendwa. Siku moja watu duni waliodhihaki na kutema mate katika uso mtulivu na uliopauka wa Kristo watautazama katika utukufu wake, uking’aa kuliko jua.

# Katika Ukumbi wa Hukumu Wa Pilato

Katika ukumbi wa hukumu wa Pilato, liwali wa Kirumi, Kristo anasimama amefungwa kama mfungwa. Karibu naye ni kundi la maaskari walinzi, na ukumbi kwa haraka unafurika watazamaji. Nje tu ya lango kuna waamuzi wa Sanhedrini, makuhani, watawala, wazee na umati.

Baada ya kumhukumu Yesu, baraza la Sanhedrini lilikuja kwa Pilato ili hukumu ithibitishwe na kutekelezwa. Lakini hawa maafisa wa Kiyahudi hawawezi kuingia katika ukumbi wa hukumu wa Kirumi. Kulingana na sheria yao ya ibada watanajisika, na hivyo kutoruhusiwa kushiriki katika ikukuu ya Pasaka. Katika upofu wao hawakuona kuwa chuki ya kuua ilikuwa imenajisi mioyo yao. Hawakuona kuwa Kristo alikuwa imenajisi mioyo yao. Hawakuona kuwa Kristo alikuwa ndiye Mwanakondoo halisi wa Pasaka, na kuwa kwa vile wamemkataa Yeye, sikukuu hii kubwa ilipoteza umuhimu wake kwao.

Mwokozi alipoletwa katika ukumbi wa hukumu, Pilato alimwangalia kwa jicho lisilo la urafiki. Liwali huyu wa Kirumi alikuwa ameitwa kwa haraka kutoka katika chumba chake cha kulala, na alikusudia kufanya kazi yake haraka iwezekanavyo. Alijiandaa kushughulika na mfungwa kama mweye amri. Kwa kutanguliza uso usio na huruma aligeuka kuangalia aina ya mtu anayepaswa kumhoji, kiasi kwamba aliitwa kutoka usingizini mapema asubuhi. Alijua kuwa lazima awe mtu ambaye mamlake ya Kiyahudi walitaka ahukumiwe na adhabu itekelezwe kwa haraka.

Pilato aliwatazama wale waliomshitaki Yesu, halafu akamkazia macho Yesu kwa kumpeleleza. Alikuwa ameshughulika na aina zote za hahalifu; lakini kamwa kabla mtu mwenye dalili za wema na tabia nzuri namna hii hajawahi kuletwa mbele yake. Katika uso wake hakuona ishara yoyote ya hatia, hakuna mwonekano wa hofu, hakuna majivuno au kutaka shari. Alimwona mtu mwenye utulivu na heshima, ambaye uso wake haukuwa na dalili yoyote ya uhalifu, isipokuwa mwonekano wa kimbingu.

Mwonekano waKristo ulifanya mvuto wa kusaidia kwa Pilato. Asili yake njema ikaamshwa. Alikuwa amesikia habari za Yesu na kazi zake. Mke wake alimwambia kitu fulani cha tendo la ajabu lililotendwa na nabii huyu Mgalilaya, aliyeponya wagonjwa na kufufua wafu. Sasa hili liliamshwa kama ndoto akilini mwa Pilato. Alikumbuka tetesi alizozisikia kutoka vyanzo kadhaa. Alinuia kuwauliza wayahudi mashtaka yao dhidi ya mfungwa.

Mtu huyu ni nani, na kwanini mmemleta? Alisema. Mashtaka gani mmeyaleta dhidi yake? Wayahudi walifadhaika. Wakijua kuwa hawawezi kuthibitisha mashtaka yao dhidi ya Kristo, hawakupendelea mahojiano ya hadhara. Walijibu kuwa alikuwa mdanganifu aliyeitwa Yesu wa Nazereti.

Pilato akauliza tena, “Mashtaka gani mmeyaleta dhidi ya mtu huyu? Makuhani hawakujibu swali lake, lakini kwa maneno yaliyoonyesha kuchukizwa kwao, walisema “Kama mtu huyu asingekuwa mtenda mabaya, tusingemleta kwako.” Wakati wana baraza la Sanhedrini, watu wa mbele katika taifa, wanaleta mtu kwako wanayona anastahili kufa, kuna haja gani kuuliza mashtaka dhidi yake? Walitumaini kumbutia Pilato kwa hisia ya umuhimu wao, na hivyo kumwongoza kukubali ombi lao bila kupitia taratibu nyingi za awali. Walikuwa na bidii ili uamuzi wao uidhinishwe; maana walijua

kwamba watu walioshuhudia kazi za ajabu za Kristo wangeeleza hadithi tofauti kabisa na uzushi ambao wao wenyewe walikuwa wakiusimulia.

Makuhani walifikiri kuwa pamoja na Pilato aliye dhaifu na mwenye kusitisita wangeweza kufanikisha mipango yao bila matatizo. Kabla ya hapo alikuwa ameidhinisha hati za vifo haraka haraka, zilizowahukumu kifo watu ambao walijua hawakustahili kifo. Katika maamuzi yake uhai wa mfunwa haukuwa na umuhimu sana; kwamba hakuwa na kosa au alikuwa na hatia haikuwa muhimu sana. Makuhani walitumaini kwamba Pilato angeidhinisha hukumu ya kifu kwa Yesu bila ya kumsikiliza. Hili walilitafuta kama upendeleo katika tukio kuu la sikukuu ya kitaifa,

Lakini kulikuwa na kitu ndani ya huyu mfungwa kilichomzuia Pilato kufanya hili. Hakuthubutu kufanya hilo. Alitambua makusudi ya makuhani. Alikumbuka jinsi, sio muda mrefu uliopita, Yesu alikuwa amemfufua Lazaro, mtu aliyekuwa amekufa siku nne; na alikusudia kujua, kabla ya kuidhinisha tamko la hukumu, ni nini yalikuwa mashtaka dhidi yake, na kama yangeweza kuthibitishwa.

Kama hukumu yenu inatosha, alisema, kwa nini kumleta kwangu? "Mchukueni, mkamhukumu kulingana na torati yenu." Kwa kubanwa hivi, makuhani walisema kwamba tayari wamekwisha mhukumu, lakini lazima wapate hukumu ya Pilato ili kuhalalisha hukumu yao. Hukumu yenu ni nini? Pilato aliuliza. Hukumu ya kifo, walijibu; lakini si halali kwetu kuua mtu. Walimwomba Pilato kuamini maneno yao kuhusu hatia ya Kristo, na kuidhinisha hukumu yao. Nao watawajibika kwa matokeo yake.

Pilato hakuwa mwamuz wa haki wala mwenye bidii kutenda mema, lakini ijapokuwa alikuwa dhaifu kimaadii, alikataa kuridhia ombi hili. Hatamhukumu Yesu hadi mashtaka yaletwe dhidi yake.

Makuhani walikuwa kwenye mashaka. Waliona kuwa lazima wafiche unafiki wao chini ya kifuniko kinene zaidi. Hawapaswi kuruhusu ionekane kuwa Kristo alikamatwa kwa misingi ya kidinni. Kama hali lingetangulizwa kama sababu, kuendelea mbele na kesi kusingukuwa na uzito kwa Pilato. Ni lazima wafanye ionekana kuwa Yesu alikuwa anapinga sheria ya jamii; hivyo angeadhibiwa kama mhalifu wa kisiasa. Ghasia na maasi dhidi ya serikali ya Kirumi viliibuka mara kwa mara miongoni mwa Wayahudi. Kwa maasi haya Warumi waliyashughulikia vikali, na daima walikuwa mmacho kukandamiza chochote ambacho kingepelekea chanzo cha mlipuko wa fujo.

Siku chache tu zilizopita mafarisayo walijaribu kumnasa Kristo kwa swali, "Je, ni halali kwetu kulipa kodi kwa Kaisari?" Lakini Kristo alifunua unafiki wao. Warumi waliokuwepo walishuhudia kushindwa kabisa kwa hawa wafanya hila, na kuchangayikiwa kwao na jibu lake, "Mlipeni Kaisari, vilivyo vya Kaisari" (Luka 20:22-25).

Sasa makuhani walifikiria kufanya ionekane kwa katika tukio hili Kristo alifundisha kile walichotumaini atafundisha. Katika kikomo chao waliita mashahidi wa uongo ili kuwasaidia, "aanao wakaanza kumshitaki, wakisema, tumemwona Mtu huyu akipotosha taifa letu na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yaye mwenyewe ni Kristo mfalme." Mashtaka matatu, yote pasipo msingi wowote. Makuhani walilijua hili, lakini walikuwa tayari kushuhudia uongo ili kufanikisha hatima yao.

Pilato aligundua kusudi lao. Kakuamini kuwa huyu mfungwa alipanga hila dhidi ya serikali. Mwanekano wake wa upole na unyenyekevu havikukubaliana kabisa na mashitaka dhidi yake. Pilato alishawishika kuwa hila kuu ilipnagwa ili kumwangamiza

mtu huyu asiye na hatia aliyesimama katika njia ya wakuu wa kidini wa Kiyahudi. Akimgeukia Yesu aliuliza “Wewe ni mfalme wa wayahudi?” Mwokozi akajibu “Wewe wasema.” Na alipokuwa akisema, uso wake uling`aa kana kwamba miali ya jua iliangaza juu yake.

Waliposikia jibu lake, Kayafa na wote waliokuwa pamoja naye walimtaka Pilato kushuhudia kuwa Yesu alikiri kosa aliloshitakiwa kwalo. Kwa mlio wa makelele, makuhani, waandishi na watawala wakadai kwamba ahukumiwe kufa. Wito wao ulipokelewa na ule umati na makelele yakikuwa yenye kuziba masikio. Pilatoo aichanganikiwa. Kwa kuona kuwa Yesu hakuwajibu lolote washitaki wake, Pilato akamwambia “Hujibu wewe chochote? Tazama yalivyo mengi mambo wanayokushitaki. Wala Yesu hakujibu nino tena.”

Akisimama nyuma ya Pilato, na kuwaona wote waliokuwa ukumbini, Kristo alisikia dhihaka; lakini kwa mashitaka yote ya uongo dhidi yake, hakujibu neno. Umbile lake lote lilitoa ushahidi wa kujitambua hana kosa. Alisimama bila kuyumbishwa na ghadhabu ya mawimbi yaliyomkabili. Ilikuwa kana kwamba mawimbi mazito yenye hasira yakipanda juu na zaidi, kama mawimbi ya bahari yenye nguvu, yalilipika kumzunguka lakini hayakumgusa. Alisimama kimya, lakini kimya chake kilikuwa maneno fasaha. Ilikuwa kama nuru ing`aayo toka mtu wa ndani kuja mtu wa nje.

Pilato alishangazwa kwa uvumilivu wake. Mtu huyu anadharau mashitaka kwa sababu hajali kuokua maisha yake? Alijiuliza. Alipomwagalia Yesu, akistahimili matukano na dhihaka bila kulipizia, alihisi kuwa asingekuwa mwovu na asiye haki kama walivyodai makuhani. Akitumaini kupata ukweli kutoka kwake na kuepuka ghasia za makutan, Palato alimchukua Yesu pembeni, na kumwuliza, tena “wewe ni mfalme wa Wayahudi?”

Yesu hakujibu moja kwa moja hili swali. Alijua kuwa Roho Mtakatifu alikuwa akishindana na Pilato, na alimpatia nafasi ya kukubali ushawishi wake. “Wewe wasema hivyo kwa nafsi yake” aliuliza “au watu wengine walikuambia habari zangu?” Hii ina maana, Je yalikuwa ni mashitaka ya makuhani au hamu ya kupokea nuru kutoka kwa Kristo, kulikochochea swali la Pilato? Pilato alielewa Kristo alichomaanisha; lakini kiburi kikainuka moyoni mwake. Hakutaka kukubali ushawishi uliokuwa juu yake. “Mimi ni Myahudi?” alisema. “Taifa lako na wakuu wa makuhani ndio waliokuleta kwangu. Umefanya nini?”

Nafasi ya thamani sana kwa pilato ilipita. Hata hivyo Yesu hakumwacha bila nuru zaidi. Wakati hakujibu moja kwa moja swali la Pilato, alidhihirisha utume wake wazi. Alimfanya Pilato kufahamu kuwa alikuwa hatafiti ufalme wa duniani.

“Ufalme wangu si wa dunia hii” alisema; “kama ufalme wangu ungekuwa wa dunia hii, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa. Ndipo Pilato akamwuliza, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye na hiyo kweli, hunisikia sauti yangu.”

Kristo alithibitisha kuwa maneno yake yalikuwa ni ufunguo ambao ungefunua siri kwa wale waliokuwa tayari kuyapokea. Yalikuwa na nguvu binafsi ya kujieleza, na hii ilikuwa ndiyo siri ya kuenea kwa ufalme wake wa Kweli. Alitamani Pilato aelewe kuwa ni kwa kupokea na kuutumia ukewli ambako kungewezesha asili yake iliyoharibiwa iweze kutengenezwa.

Pilato alikuwa na hamu ya kuujua ukweli. Akili yake ilichanganyikiwa. Alishikilia maneno ya Mwokozi kwa shaukun na moyo wake uliamshwa na kutamani sana kujua ilikuwa nini hasa, na jinsi gani angeipata. "Kweli ni nini?" aliuliza. Lakini hakusubiri kupewa jibu. Ghasia zilizokuwa nje zilimkumbusha haja kuu ya saa ile; maana makuhani walidai hatua ya mara moja ichukuliwe. Akielekea nje kwa Wayahudi alitangaza kwa kukazia "Mimi sioni hatia yoyote kwake."

Maneno haya kutoka kwa mwamuzi mmataifa yalikuwa karipio kali kwa usaliti na uongo wa watawala wa Israeli waliokuwa wanamshitaki Mwokozi. Makuhani na wazee waliposikia tangazo la Pilato, masikitiko na hasira yao kali haikujua mipaka. Kwa muda mrefu walipanga hila na walisubiri nafasi hiyo. Kwa walivyoona mwelekeo wa kuachiwa Yesu, walionekana kuwa tayari kumrarua vipande. Walimshutumu Pilato kwa kelele na kumtishia kwa masuto ya serikali ya Kirumi. Walimlaumu kwa kukataa kumhukumu Yesu, ambaye, walitangaza kuwa alikuwa amejiweka kuwa kinyume na Kaisari.

Sauti zenye hasira zilisikika, zikitangaza kuwa mvuto wa uchochezi wa Yesu dhidi ya serikali ulijulikana kwa taifa zima. Makuhani walisema, "Anawachochea watu, akifundisha katika Uyahudi wote, toka Galilaya hata mahali hapa."

Pilato kwa wakati huu hakuwa na wazo la kumhukumu Yesu. Alijua kwamba Wayahudi walikuwa wamemshitaki kwa sababu ya chuki na nia ya kumletea mdhara. Alijua wajibu wake ni nini. Haki ilidai kuwa Kristo afunguliwe mara moja. Lakini Pilato alihofia nia mbaya ya watu. Kama akiwakatalia kumkabidhi Yesu mikononi mwao, ghasia zitaanzishwa, na hizi aliogopa kuzikabili. Aliposikia kwamba Yesu anatoka Galilaya, aliamua kumpeleka kwa Herode, mtawala wa wilaya ile, ambaye kwa wakati huo alikuwepo Yerusalemu. Kwa njia hii, Pilato alifikiri kuhamisha wajibu wa kesi kutoka kwake hadi kwa Herode. Pia aliona huu ni wakati mzuri wa kuponya ugomvi wa zamani kati yake na Herode. Na hivyo ndivyo ilithibitika. Majaji hawa wawili walifanya urafiki kwa kesi ya Mwokozi.

Pilato alimkabidhi Yesu tena kwa maaskari na kati ya dhihaka na kudhalilishwa na umati ule, aliharakishwa hadi katika Jumba la hukumu la Herode. "Herode alipomwona Yesu alifurahi sana."Kamwe hakuwahi kukutana na Mwokozi, "Lakini alikuwa na hamu ya kumwona muda mrefu, maana alikuwa amesikia habari nyingi kumhusu, na alitumaini kuona baadhi ya miujiza aliyofanya." Huyu Herode ni yule aliyekuwa na hatia ya damu ya Yohana Mbatizaji. Herode aliposikia habari za Yesu kwa mara ya kwanza aliogopa sana, na akasema, "Huyu ni Yohana niliyemkata kichwa, amefufuka katika wafu," "kwa hiyo nguvu hizo zinatenda kazi ndani yake" (Marko 6:16; Mathayo 14:2). Lakini bado Herode alitaka kumwona Yesu. Sasa kulikuwa na nafasi ya kuokoa maisha ya nabii huyu, na mfalme alitumaini kukomesha milele kutoka mawazoni mwake kumbukumbu ya kichwa kile kilichojaa damu kulicholetwa mbele yake katika kombe. Pia alitamani udadisi wake ufurahishwe, na alifikiri kwamba kama Kristo atapewa matazamio yoyote ya kuachwa huru, atafanya lolote ambalo angetakiwa kufanya.

Kundi kubwa la makuhani na wazee waliandamana na Yesu hadi kwa Herode. Na wakati Mwokozi alipoletwa ndani, hawa wakuu wa dini, wote wakiongea kwa msisimko, walihimiza mashitaka dhidi yake. Lakini Herode hakutilia Umuhimu madai yao. Aliamuru kuwa na utulivu, akitaka nafasi ya kumhoji Kristo. Aliagiza kuwa pingu za Kristo zifunguliwe, na wakati huo huo akiwaumu maadui wake kwa kumtendea vibaya. Akitazama kwa huruma katika uso uliopauka na shwari wa Mkombozi wa ulimwengu,

aliona tu katika uso wake hekima na usafi. Yeye kama vile Pilato aliridhika kwamba Kristo alishitakiwa kutokana na fitina na chuki.

Herode alimhoji Kristo kwa maneno mengi, lakini kwa muda wote Mwokozi alidumisha kimya chenye ufahamu mkuu. Kwa amri ya mfalme, wakongwe na vilema waliletwa ndani, na Kristo aliamuriwa kuthibitisha madai yake kwa kufanya muujiza. Watu wanasema kwamba unaweza kuponya wagonjwa, alisema Herode. Natamani kuona kuwa sifa yako njema iliyoenea pote siyo uongo. Yesu hakujibu, na Herode bado aliendelea kuhimiza: Kama huwezi kufanya miujiza kwa ajili ya wengine, fanya sasa kwa ajili yako mwenyewe, nayo itakufaa. Akaamuru tena, tuonyeshe ishara kwamba una uwezo ambao uvumi umekupatia. Lakini Kristo alikuwa kama mtu ambaye hakusikia wala kuona. Mwana wa Mungu alitwaa asili ya binadamu. Ni lazima afanye kama ambavyo mtu anapaswa kufanya katika hali ya jinsi hiyo. Kwa hiyo asingefanya muujiza ili kujiokoa na maumivu na kudhalilishwa ambako mtu anapaswa kuvumilia anapokabili hali kama hiyo.

Herode aliahidi kwamba kama Kristo atafanya muujiza mbele yake, basi angeachiwa huru. Washitaki wa Kristo waliona kwa macho yao wenyewe matendo makuu yaliyotendwa kwa nguvu zake. Walimsikia akiamuru makaburi kuatoa wafu wake. Walikuwa wamewaona wafu wakitoka kwa kutii amri yake. Hofu iliwashika isiwe akafanya sasa muujiza. Katika mambo yote, zaidi walihofia udhihirisho wa nguvu zake. Onyesho hilo litahakikisha pigo la mauti kwa mipango yao, na huenda itawagharimu maisha yao. Kwa mara nyingine makuhani na watawala waliokuwa kwenye mashaka makuu, walihimiza mashitaka yao dhidi yake. Wakipaaza sauti zao, walisema, Ni msaliti, na amekufuru. Anafanya miujiza yake kwa nguvu alizopewa na Beelzebubu, mkuu wa pepo. Ukumbi ukawa mahali pa machafuko, wengine wakisema hili, wengine lile.

Dhamiri ya Herode sasa ilikuwa na hisia za mbali kuliko alipottetemeka kwa utisho kutokana na ombi la Herodia kwa kichwa cha Yohana Mbatizaji. Kwa muda alikuwa amehisi michomo mikali ya majuto kwa tendo lake la kutisha; lakini fahamu zake za uadilifu zilidhoofhika sana kutokana na maisha yake ya anasa. Sasa moyo wake ulikuwa mgumu kiasi cha kuweza hata kujisifu kwa adhabu iliyotolewa kwa Yohana kwa kuthubutu kumkemea. Na sasa alimtishia Yesu, akitanganza kwa kurudiarudia kwamba yeye alikuwa na uwezo wa kumfungua au kumhukumu. Lakini hakuna dalili kutoka kwa Yesu iliyoonyesha kuwa alisikia neno.

Herode alikasirishwa na ukimya huu. Ilionekana kuashiria kutojali kabisa mamlaka yake. Kwa mfalme huyu mwenye kiburi na majivuno, karipio la wazi lisingechukiza sana kuliko kutojaliwa namna hii. Kwa hasira alimtishia Yesu tena, ambaye bado alibakia bila kuyumbishwa na kimya.

Utume wa Kristo hapa duniani haukuwa wa kufurahisha udadisi wa bure. Alikuja kuponya waliovujika moyo. Kama angetakiwa kusema neno lolote kuponya majeraha ya roho inayougua dhambi, asingeweza kukaa kimya. Lakini hakuwa na neno kwa wote ambao wangeukanyaga tu ukweli chini ya miguu yao miovu.

Kristo angeweza kusema maneno kwa Herode ambayo yangepenya masikio ya mfalme huyu kaidi. Angeweza kumshtusha kwa hofu na kutetemeka kwa kumfunulia uovu wote wa maisha yake, na utisho wa ajali yake iliyokuwa imekaribia. Lakini ukimya wa Kristo ulikuwa karipio kali ambalo angeweza kumpatia. Herode alikuwa amekataa ukweli alioambiwa na nabii mkuu, na hakukuwa na ujumbe mwingine ambao angepokea.

Hakuna neno ambalo mkuu wa mbinguni alikuwa nalo kwa ajili yake. Sikio lile ambalo daima lilikuwa wazi kwa misiba ya wanadamu, halikuwa na nafasi kwa amri ya Herode. Macho yale ambayo daima yaliwatazama wadhambi waliotubu kwa huruma, na upendo wenye kusamehe, hayakuweza kumtazama Herode. Midomo ile iliyotamka daima ukweli wenye mvuto sana, ambayo kwa sauti ya maombi ya huruma ilisihi mdhambi sana na aliye duni saa, ilifungwa kwa mfalme mwenye kiburi ambaye hakuhisi hitaji la Mwokozi.

Uso wa Herode ukawa mweusi kwa hasira. Akiwageukia makutano, kwa hasira alimshutumu Yesu kuwa mlaghai. Halafu kwa Kristo akasema, kama hutatoa uthibitisho wa madai yako, nitakukabidhi kwa maaskari na watu. Wanaweza kufaulu kukufanya uzungumze. Kama wewe ni mlaghai, kifo mikononi mwao ndicho tu unastahili; kama wewe ne Mwana wa Mungu, jiokoe mwenyewe kwa kufanya muujiza.

Mara tu maneno haya yalipotamkwa, kulikuwa na harara kwa ajili ya Kristo. Kama wanyama misitu, makutano walimrukia mateka wao. Yesu alivutwa huku na kule, Herode akiungana na umati ili kumdhalilisha Mwana wa Mungu. Kama maaskari wa Kirumi wasingeingia kati, na kurudisha nyuma umati uliopagawa, Mwokozi angeraruliwa vipande.

"Herode na maaskari wake wakamfanya duni na kumdhihaki, na kumvika mavazi mazuri." Maaskari wa Kirumi walijiunga katika utesaji huu. Yote ambayo hawa maaskari waovu na wala rushwa, wakisaidiwa na Herode na wakuu wa Kiyahudi, wangeweza kuchochea yaliwekwa juu ya Mwokozi. Hata hivyo uvumilivu wake wa Kiungu haukushindwa.

Watesi wa Kristo walijaribu kupima tabia yake na yao wenyewe; walikuwa wamemwelezea kuwa mwovu kama wao. Lakini nyuma ya yote yaliyokuwa yakitokea pale onyesho jingine lilijiingiza lenyewe, - onyesho ambalo siku moja wataliona katika utukufu wake wote. Kuna baadhi waliokuwa wakitetemeka mbele ya Kristo. Wakati umati jeuri ulipokuwa ukiinama mbele yake kwa dhihaka, baadhi yao waliokuja mbele kwa kusudi hilo walirudi nyuma, wakiogopa na kunyamazishwa. Heroe alishawishika. Mionzi ya mwisho ya mwanga wa rehema ilingaa katika moyo wake mgumu wa dhambi. Alihisi kuwa huyu hakuwa mtu wa kawaida; maana Uungu uliangaza kupitia ubinadamu. Katika muda hasa wakati Kristo alipozingirwa na wenye kudihaki, wazinzi, na wauaji, Herode alihisi alikuwa anamtazama Mungu juu ya kiti chake cha enzi.

Pamoja na kuwa mgumu, Herode hakudiriki kukubali hukumu ya Kristo. Alitamani kujipatia nauu ya wajibu ule wa kutisha, na akamrudisha Yesu tena kwenye ukumbi wa hukumu wa Kirumi.

Pilato alisikitika na kusumbuka sana. Wayahudi waliporudi na mfungwa wao, aliuliza kwa hasira ni nini walitaka aanye. Aliwakumbusha kuwa alikuwa tayari amemhoji Yesu, na hakuona kosa lolote kwa,e; aliwaambia kuwa walikuwa wameleta malaumu dhidi yake, lakini hawakuweza kuthibitisha shitaka hata moja. Alimpeleka Yesu kwa Herode, liwali wa Galilaya, na moja wa taifa lao wenyewe, lakini hata yere hakuona lolote juu yake linalostahili kufa. "Hivyo nitamrudi" Pilato alisema "na kumwachilia."

Hapa Pilato alionyesha udhaifu wake. Alikuwa amesema kwamba Yesu hana hatia, lakini bado akawa tayari apigwe mijeledi ili kuwatuliza washitaki wake. Angeacha haki na kanuni ili kupatana na watu. Hili lilimweka pabaya. Makutano walitumia vibaya kusitasita kwake, na kudai zaidi uhai wa mfungwa. Kama tangu awali Pilato angesimama thabiti, na kukataa kumhukumu mtu aliyempata hana hatia, angeweza kuvunga mnyororo wa kufisha ambao ungemfunga katika majuto na hatia katika siku

zote za maisha yake. Kama angetekeleza uthibitisho wake wa haki, Wayahudi wasingethubutu kumwamuru nini afanye. Kristo angeuawa, lakini hatia isingekuwa juu ya Pilato. Lakini Pilato hatua kwa hatua alipinga dhamiri yake. Alikuwa amejiepusha kuhukumu kwa haki na usawa, sasa alijikuta hana msaada mikononi mwa makuhani na watawala. Kusitasita na kufanya uamuzi kwake, kulimhakikishia uangamivu wake.

Hata sasa Pilato hakuachwa kutenda kama kipofu. Ujumbe kutoka kwa Mungu ulimwonya dhidi ya tendo alilotaka kufanya. Kwa kujibu ombi la Kristo, mke wa Pilato alifikiwa na malaika kutoka mbinguni, na katika ndoto alimwoa Mwokozi na kuzungumza naye. Mke wa Pilato hakuwa Myahudi, lakini alipomtazama Yesu katika ndoto yake, hakuwa na mashaka kuhusu tabia au utume wake. Alimtambua kuwa Mwana wa Mungu. Alimwona katika majaribu katika jumba la hukumu. Aliona mikono ikiwa imefungwa kwa nguvu kama ya mhalifu. Alimwona Herode na Maaskari wake wakitekleza kazi yao ya kutisha. Aliwasikia makuhani na watawala, wakijawa na chuki na uovu, kama vichaa wakishitaki. Alisikia maneno "Tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa." Alimwona Pilato akimtoa Yesu ili apigwe mijeledi, baada ya kuwa ametangaza kuwa "Sioni hatia yoyote kwa mtu huyu." Alisikia hukumu ikitangazwa na Pilato, na alimwona akimkabidhi Kristo kwa wauaji wake. Aliuona msalaba ukiinuliwa Kalvari. Aliona dunia imefunikwa na giza, na akasikia kilio cha ajabu, "Imekwisha." Bado tukio jingine lilikutana na macho yake. Alimwona Kristo ameketi juu ya wingu kubwa jeupe, wakati dunia inawayawaya angani, na wauaji wake wakikimbia mbele ya utukufu ake. Kwa kilio cha hofu akaamka, na mara moja akamwandikia Pilato Maneno ya maonyo.

Wakati Pilato anasitasita afanye nini, mjumbe alijipenyeza kati ya makutano, na kumkabidhi barua kutoka kwa mkewe iliyosomeka; "Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake."

Uso wa Pilato ulipauka. Alichanganywa na hisia zake zilizokuwa zikipingana. Lakini wakati akikawia kuamua makuhani na watawala waliendelea kuchochea mawazo ya watu. Pilato alilazimishwa kuchukua hatu. Sasa alifikiria mwanyewe desturi ambayo ingesaidia kufanikisha kufunguliwa kwa Kristo. Ilikuwa desturi katika sikukuu hii kuwafungulia mfungwa mmoja ambaye watu wangemchagua. Destur hii ilivumbuliwa na wapagani, hakukuwa na kivuli chochote cha haki ndani yake, lakini ilithaminiwa sana na Wayahudi. Mamlaka ya Kirumi kwa wakati huo yalimshikilia mfungwa aliyeitwa Baraba, aliye kuwa amehukumiwa kifu. Mtu huyu alikuwa amedai kwamba yeye ni Masihi. Alidai kuwa na mamlaka ya kuanzisha mfumo mpya wa mambo, kuiweka dunia katika hali sawa. Chini ya udanganyifu wa Shetani alidai kuwa chochote ambacho angepata kutokana na wizi na unyang`anyi ilikuwa mali yake. Alikuwa amefanya mambo ya ajabu kwa njia ya mawakala wa Shetani, alikuwa amepata wafuasi miongoni mwa watu, na alikuwa ameamsha uchochezi dhidi ya serikali ya Kirumi. Chini ya kivuli cha bidii ya didini alikuwa mtu mbaya sana, kaidi na aliyekata tamaa, aliyejielekeza katika uasi na ukatili. Lakini kuwapa watu kuchagua kati ya mtu huyu na Mokozi asiye na hatia, Pilato alifikiria kuamsha watu kwa hisia ya haki. Alitumaini kupata huruma yao kwa ajili ya Yesu ili kuwapiga makuhani na watawala. Hivyo akiwageukia makutano, alisema kwa bidii "Mnataka niwafungulie yupi? Baraba au Yesu aitwaye Kristo?"

Kama mlio wa wanyama mwitu lilikuja jibu la watu, "Tufungulie Baraba!" Zaidi na zaidi makelele yaliendelea, Baraba! Baraba! Akifikiri watu hawakuelewa swali lake, Pilato aliuliza, "Mnataka niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?" Lakini walipiga kelele

“Mwondoshe mtu huyu, na utufungulie Baraba!” “Nimtedeeje basi Yesu aitwaye Kristo?” Pilato aliuliza. Kwa mara nyingine makutano waliunguruma kama mapepo. Mashetani wenyewe, katika sura ya binadamu, walikuwemo kati ya makutano, na ni nini kingetazamiwa kama siyo jibu “Asulubiwe?”

Pilato alifadhaika. Hakufikiria kama ingefikia hivyo. Aliynywea dhidi ya kumkabidhi mtu asiye na hatia kwa kifo kibaya sana cha aibu na ukatili ambacho kingetendeka. Baada ya ngurumo za makelele kutulia, aliwageukia watu, na kusema, “Kwa nini, ni ubaya gani alioutenda?” Lakini swala hili lilikuwa limefika mbali kwa hoja. Sio ushahidi wa Kristo kutokuwa na hatia uliokuwa unatakiwa, bali hukumu yake.

Hata Hivyo Pilato alijutahidi kumwokoa. “Aliwaambia kwa mara ya tatu, Kwani, ni ubaya gani alioutenda? Sikuona sababu yoyote ya kufa kwake: Hivyo nitamrudi, na kumwachilia aende zake.” Lakini kule kutaja tu kufunguliwa kwake kulichochea watu kuwa wazimu mara kumi zaidi. “Msulibishe, msulibishe” walipiga makelele. Zaidi na zaidi makelle yaliongezeka ya ghasia zilizotokana na kusitasita kwa Pilato kufanya maamuzi.

Yesu alichukuliwa, akizimia kwa uchovu na mwenye Majeraha, alipigwa mijeledi mbele ya watu. “Na maaskari wakamchukua hadi katika ukumbi, ulioitwa Praitoria; wakamkusanyikia kikosi kizima. Nao wakamvika vazi la rangi ya zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani, wakaanza kumsalimu, Salamu Mfalme wa Wayahudi! Nao… wakamtemea mate, wakapiga magoti, wakamsujudia.” Mara kadhaa mikono fulani miovu ilinyakua mwanzi uliokuwa umewekwa mikononi mwake, na kuipiga taji ya miiba iliyowekwa kichwani pake, na kusukumiza miiba mwiini mwake, na kutoa damu iliyotiririka usoni kwake na kidevuni.

Staajabuni, enyi mbingu! Na kastaajabuni enyi dunie! Tazameni mwoneaji na yeye aliyeonewa. Umati uliopagawa unamzingira Mwokozi wa ulimwengu. Dhihaka na vicheko vya mzaha vilichanganyika na viapo vya kishenzi vya kukufuru. Kuzaliwa kwake kwa unyenyekevu na maisha ya kujishusha yanatolewa maoni na watu hawa waliokufa ganzi. Madai yake kuwa Mwana wa Mungu yanafanyiwa dhihaka, na mizaha ya kishenzi na matukano ya vicheko vya dharau yanapitishwa toka kinwa hadi kinywa.

Shetani aliongoza watu hawa katili katika kumnyanyasa Mwokozi. Lilikuwa kusudi lake kumchochea ili alipize kisasi ikiwezekana, au kumlazimisha kufanya muujiza ili kujiokoa mwenyewe, na hivyo kuharibu mpango wa Wokovu. Doa moja katika maisha yake ya ubinadamu, kushindwa mara moja kwa ubinadamu wake kuvumilia majaribu ya kutisha, ndipo Mwanakondoo wa Mungu angekuwa dhabihu isiyo kamilifu, na ukombozi wa mwanadamu kushindikana. Lakini Yeye ambaye kwa amri moja angeweza kulazimisha wale watu kukimbia kwa hofu kutoka mbele zake kwa mafunuo ya Uungu wake, - alijisalimisha kwa utulivu mkamilifu kwa unyanyasaji mbaya sana wa kikatili na wenye kufedhehesha.

Maadui wa Kristo walikuwa wamedai muujiza kama ushahidi wa Uungu wake. Walikuwa na uthibitisho mkuu zaidi sasa kuliko wowote walioutafuta. Kwa kadri ukatili wao ulivyoshusha mateso yake chini ya utu na kufanana na Shetani, hivyo ndivyo upole a uvumilivu ulivyomwinua Yesu juu ya ubinadamu, na kuthibitisha asili yake kwa Mungu. Kujishusha kwake kulikuwa kiapo cha kutukuzwa kwake. Matone ya damu ya maumivu ambaye kutoka katika mwili wake uliojeruhiwa ilitiririka usoni na kidevuni ilikuwa kiapo cha kutiwa mafuta kwa “mafute ya shangwe” (Waebrania 1:9) kama kuhani mkuu wa juu sana.

Ghadhabu ya Shetani ilikuwa kubwa alipoona kwamba unyanyasaji wote uliosababishwa juu ya Mwokozi aukumlazimisha kunung`unika hata kidogo kwa kinywa chake. Ijapokuwa alitwaa asili ya ubinadamu juu yake, alitegemezwa kwa uvumilivu wa Uungu, na hakuacha hata kidogo mapenzi ya Baba yake.

Wakati Pilato alipomtoa Yeu ili apigwe mijeledi na kudhihakiwa, alifikkiri kuamsha huruma ya makutano. Alitumaini wangeamua kwamba hii ilikuwa ni adhabu ya kutosha. Hata uovu wa makuhani, alifikiri, sasa ungetosheka. Lakini kwa akili kali za utambuzi Wayahudi waliona udhaifukwa kumwadhibu hivyo mtu aliyekwishamtangaza kwamba hana hatia. Walijua kwamba Pilato alikuwa anajaribu kuokoa maisha ya mfungwa, nao walidhamiria kuwa Yesu asifunguliwe. Ili kutufurahisha na kuturidhisha, Pilato amempiga mijeledi, walitafakari, na kama tukishinikiza jambo tulililoliamua, kwa hakika tutafanikiwa.

Sasa Pilato aliagiza Baraba aletwe barazani. Naye akawaleta mbele wafungwa wote wawili, mmoja kila upande, na akielekeza kwa Mwokozi alisema kwa sauti ya heshima yenye kusihi, "Mtu huyu namleta nje kwenu, mpate kufahamu ya kuwa mimi sioni hatia yoyote kwake."

Pale alisimama Mwana wa Mungu, akiwa amevaa vazi la dhihaka na taji ya miiba. Akiwa amevuliwa nguo hadi kiunoni, mgongo wake ulionyesha mistari mirefu ya kikatili iliyokuwa ikivuja damu bila kizuizi. Uso wake ulikuwa na madoa ya damu; na ulikuwa na dalili za kuishiwa nguvu na maumivu; lakini kamwe haukuwahi kupendeza kuliko sasa. Uso wa Mwokozi haukuharibika mbele ya maadui zake. Kila ishara iliashiria uungwana na uvumilivu na huruma ya upole kwa ajili ya maadui zake wakatili. Katika mwenendo wake hakukuwa na udhaifu wa woga, lakini nguvu na adabu ya mateso ya muda mrefu. Katika utofauti wa juu sana alikuwa mfungwa kando yake. Kila mstari wa uso wa Baraba ulimwonyesha kama mtu mgumu na mwovu hali aliyokuwa nayo. Tofauti iijieleza kwa kila mtazamaji. Baadhi ya watazamaji walikuwa wanalia. Walipomwangalia Yesu, mioyo yao ilijaa huruma. Hata makuhani na watawala walishawishika kwamba, alivyokuwa, ni sawa na madai yake yote.

Maaskari wa Kirumi waliomzunguka Kristo hawakuwa wagumu wote; wengine walimwangalia kwa makini usoni kwa ajili ya uthibitisho angalau mmoja kwamba alikuwa mhalifu au mtu hatari. Mara kwa mara waligeuka na kumwangalia Baraba kwa dharau. Haikuhitaji utambuzi wa kina ili kumsoma ndani. Mara walimgeukia tena aliyekuwa kwanye mashitaka. Walimtazama huyu mtesekaji wa Kimbingu kwa hisia za huruma ya kina. Kujisalimisha kwa kimya kwa Kristo kuliweka muhuri wa tukio hili akilini mwao, ambalo haligefutika mpaka hapo au watakapomkiri kama Kristo au kwa kumkataa waamue hatima yao.

Pilato alishikwa na mshangao kwa uvumilivu wa Mwokozi usio na manung`uniko. Hakuwa na mashaka kuwa mwonekano wa Mtu huyu, kwa kutofautisha na Baraba, utawavuta Wayahudi kwa huruma. Lakini hakufahamu ushupavu wa chuki wa makuhani kwa ajili yake, ambaye, kama nuru ya ulimwengu, amedhihirisha giza na makosa yao. Walishawishi watu kwa hasira ya kiwazimu, na tena makuhani, watawala na watu walipaza kelele za kutisha "Msulibishe, Msulibishe." Hatimaye, akipoteza subira yote kwa ukatili wao usio na sababu, Pilato alipiga kelele kwa kukata tamaa, "Mchukueni ninyi mkamsulibishe, maana sikuona kosa lolote kwake."

Mtawala wa Kirumi, ijapokuwa alikuwa mzoefu wa matukio ya kikatili, alishikwa na huruma kwa mfungwa huyu aliyekuwa akiteseka, ambaye, ijapo alihukumiwa na

kupigwa mijeledi, uso uliokuwaukivuja damu na mgongo uliochubuka, bado alikuwa anaonyesha kama mfalme juu ya kiti cha enzi. Lakini makuhani walitangaza "Sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo imempasa kufa maana alijifanya Mwana wa Mungu."

Pilato alishitushwa. Hakufahamu visuri kuhusu Kristo na utume wake; lakini alikuwa na imani isiyo dhahiri kwa Mungu na viumbe vilivyo juu kuliko wanadamu. Wazo ambalo liliwahi kupita mawazoni mwake sasa lilileta sura halisi. Alijiuliza kama siyo nafsi ya Uungu iliosimama mbele zake, imevikwa nguo ya Zambarau, ya dhihaka na kuvishwa taji ya miiba.

Aliingia tena ukumbini, na kumwuliza Yesu, "Wewe umetoka wapi?" Lakini Yesu hakumpa jibu lolote. Mwokozi aliongea wazi kwa Pilato, akielezea utume wake kama shahidi wa kweli. Pilato alikuwa ameidharau nuru. Alikuwa ametumia vibaya cheo cha juu cha mwamuzi kwa kuachia kanuni na mamlaka yake kwa madai ya watu. Yesu hakuwa na nuru zaidi kwa ajili yake. Akiwa ameudhiwa na kimya chake, Pilato alisema kwa kiburi:

"Husemi nami? Hujui ya kuwa mimi nina mamlaka ya kukufungua, nami nina mamlaka ya kukusulibisha?" Yesu akamjibu " Wewe hungekuwa na mamlaka yoyote juu yangu, kama usingepewa kutoka juu; kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako yuna dhambi iliyo kubwa zaidi."

Hivyo Mwokozi mwenye huruma, katikati ya mateso yake makali na huzuni, alisamehe kwa kadri ilivyowezekana tendo la mtawala wa Kirumi aliyemtoa ili asulibiwe. Picha ya jinsi gani tukio hili lingeonyesha ulimwengu kwa nyakati zote! Nuru ya jinsi gani linatoa kwa tabia yake Yeye aliye Mhukumu wa dunia yote!

"Yeye aliyenitia mikononi mwako" Yesu alisema "ana dhambi iliyokubwa zaidi." Kwa maneno haya Kristo alimaanisha Kayafa, ambaye, kama kuhani mkuu aliwakilisha taifa la Kiyahudi. Walifahamu kanuni zilizoongoza mamlaka za Kirumi. Walikuwa na nuru katika unabii uliomshuhudia Kristo, na katika mafundisho yake mwenyewe na miujiza waamuzi wa Kiyahudi walikuwa wamepata ushahidi usio na makosa wa Uungu wa huyu waliyemhukumu kufa. Na kulingana na nuru waliyonayo watahukumiwa.

Hatia kubwa sana na wajibu mzito viliwahusu wale waliosimama katika nafasi za juu za taifa, watunzaji wa hazina takatifu ambayo walikuwa wakiisaliti hasa. Pilato, Herode na maaskari wa Kirumi kwa kulinganisha, hawakumjua Yesu. Walifikiria kuwapendeza makuhani nw watawala kwa kumnyanyasa. Hawakuwa na nuru ambayo taifa la Kiyahudi lilikuwa limeipokea kwa wingi. Kama nuru ingetolewa kwa maaskari, wasingalimtendea Yesu kwa ukatili kama walivyofanya.

Kwa mara nyingine Pilato alipendekeza kumfungulia Mwokozi. "Lakini Wayahudi wakapiga kelele, wakisema, Kama ukimfungua huyu, wewe si rafiki yake Kaisari." Hivyo hawa wanafiki wakajifanya kuona wivu kwa ajili ya mamlaka ya Kaisari. Kati ya wapinzani wote wa utawala wa Warumi, Wayahudi walikuwa wakali sana. Wakati ilipokuwa salama kwao kufanya hivyo, walikuwa wakandamizaji sana katika kulazimisha matakwa ya taifa na dini yao; lakini walipotaka kutenda kusudi fulani la ukatili walikuza uwazo wa Kaisari. Ili kukamilisha uangamivu a Kristo, wangedai kuwa watii kwa utawala huu wa kigeniwaliokuwa wanauchukia.

"Yeyote ajifanyaye kuwa mfalme," waliendelea "humfitini Kaisari." Hii ilikuwa kumshika Pilato mahali dhaifu. Alikuwa anatiliwa mashaka na Serikali ya Kirumi, na alijua kwamba taarifa kama hiyo ingemwangamiza. Alijua kwamba kama wayahudi wakipuuzwa, hasira yao ingeelekezwa kwake. Wangefanya chochote ambacho kilipasa

ili kulipiza kisasi. Alikuwa na mfano mbele yake wa kusisitiza ambako, kwao, walitafuta uhai wa Mmoja waliyemchukia bila sababu.

Baadaye Pilato akakalia kiti cha hukumu, na kumleta tena Yesu mbele ya watu, akisema, "Mtazame mfalme wenu!" Kelele za wazimu zilisikika tena "Mwondoshe, msulibishe." Kwa sauti iliyosikika mbali na karibu Pilato aliuliza "Nimsulibishe mfalme wenu?" Lakini kutoka midomo najisi, yenye kukufuru yalitoka maneno haya "Sisi hatuna mfalme ila kaisari."

Hivyo kwa kuchagua mfalme mmataifa, taifa la Kiyahudi lilikuwa limejiondoa katika Serikali ya Mungu. Walikuwa wamemkataa Mungu kama mfalme wao. Tangu sasa hawakuwa na mwokozi. Hawakuwa na mfalme isipokuwa Kaisari. Katika hili makuhani na waalimu walikuwa wamewaongoza watu. Kwa hili, pamoja na matokeo ya kutisha yaliyofuata, wao ndio waliwajibika. Dhambi ya taifa na uangamivu wa taifa vilitokana na viongozi wa kidini.

"Pilato alipoona kuwa hatashinda kwa vyovyote, lakini ghasia tu zilitokea, alichukua maji, na kunawa mikono yake mbele ya makutano, akisema, mimi sina hatia ya damu ya Mtu huyu mwenye haki; yaangalieni ninyi wenyewe." Kwa woga na kujihukumu mwenyewe Pilato alimwangalia Mwokozi. Katika bahari pana ambayo kila uso ulikuwa umevurugika, uso wake tu ulikuwa na amani. Kuzunguka kichwa chake nuru laini ilionekana kuangaza. Pilato alijisemea moyoni, Yeye ni Mungu. Akiwageukia makutano alitangaza, Mimi sina hatia ya damu yake. Mchukueni ninyi, mkamsulubishe. Lakini angalieni ninyi makuhani na watawala, namtangaza kuwa Mwenye haki. Hebu huyo anayemdai kuwa Baba yake awahukumu ninyi na siyo mimi kwa tendo hili la leo. Halafu kwa Yesu akasema, Nisamehe kwa tendo hili; siwezi kukuokoa. Na baada ya kumpiga tena Yesu mijeledi, alimtoa ili akasulubiwe.

Pilato alitamani sana kumwokoa Yesu. Lakini aliona kuwa hawezi kulifanya hilo, na bado akalinda cheo na heshima yake. Kuliko kupoteza mamlaka ya kidunia, alichagua kutoa kafara maisha yasiyo na hatia. Wangapi leo, ili kuepuka hasara au mateso, kwa jinsi hiyo huuza kirahisi kanuni. Dhamiri na wajibu huelekeza njia moja, na mapenzi ya nafsi huelekeza nyingine. Mkondo unategwa kwa nguvu kuelekea ubaya, na yeye anayeridhia dhambi huchukuliwa katika giza nene la hatia.

Pilato aliridhia madai ya watu. Kuliko kuhatarisha kupoteza cheo chake, alimtoa Yesu ili asulibiwe. Lakini licha ya tahadhari aliyoichukua, jambo lile alilolihofia mbele lilimpata. Heshima zake ziliondolewa kwake, alishushwa kutoka cheo chake cha juu, na, akiwa amechomwa kwa majuto na kiburi kilichojeruhiwa, muda si mrefu baada ya Yesu kusulibiwa, (Pilato) alijiua mwenyewe. Vivyo wote wanaopatana na dhambi watavuna tu huzuni na uharibifu. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti" (Mithali 14:12).

Wakati Pilato alipotangaza kwamba yeye hana hatia ya damu ya Kristo, Kayafa alijibu kwa shari "Damu yake na iwe juu yetu na watoto wetu." Maneno ya kutisha yalichukuliwa na makuhani na watawala, na kupokewa na umati kwa makelele yasiyo ya kibinadamu. Umati wote ulijibu na kusema "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu."

Waisraeli walikuwa wamefanya uamuzi. Wakimsonda Yesu walikuwa wamesema "si mtu huyu, ila Baraba." Baraba, mnyang`anyi na muuaji, alimwakilisha Shetani. Kristo alimwakilisha Mungu. Kristo alkataliwa; Baraba alikubaliwa na watu. Baraba ndiye watakuwa naye. Kwa kufanya uchaguzi huo walimkubali yeye ambaye tangu mwanzo

alikuwa mwongo na muuaji. Shetani alikuwa ndiye kiongozi wao. Kama taifa watatekeleza amri zake. Kazi zake ndizo watazitenda. Utawala wake imewapasa kuuvumilia. Wale watu waliomchagua Baraba badala ya Kristo wataendelea kuhisi ukatili wa Baraba hada mwisho wa wakati.

Wakimtazama Mwanakondoo wa Mungu aliyejeruhiwa, Wayahudi walisema "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu." Kilio kile cha kutisha kilifika katika kiti cha enzi cha Mungu. Hukumu hiyo, waliyojitangazia wenyewe, iliandikwa mbinguni. Ombi lile lilisikiwa. Damu ya Mwana wa Mungu ilikuwa juu ya watoto wao na juu ya watoto wa watoto wao, laana ya kudumu.

Kwa kuogofya sana ilifahamika katika uharibifu wa Yerusalemu. Kwa kuogofya imedhihirishwa katika hali ya taifa la Kiyahudi kwa miaka elfu moja na mia nane, - tawi lililokatwa kutoka kwenye shina, tawi lililokufa, lisilozaa matunda, litakalokusanywa na kuchomwa moto. Toka nchi hadi nchi duniani kote, karne hadi karne, wafu, wafu katika dhambi na uasi.

Kwa utisho mkuu ombi hilo litakamilishwa katika siku kuu ya hukumu. Kristo atakapokuja duniani tena, si kama mfungwa aliyezungukwa na watu wanaofanya ghasia, watu watamwona. Ndiop watakapomwona kama mfalme wa mbinguni. Kristo atakuja katika utukufu wake mwenyewe, katika utukufu wa maliaka watakatifu. Elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu elfu ya malaika, wana wa Mungu wazuri na washindi, wenye uzuri na utukufu uzidio sana, wataandamana naye. Ndipo atakapoketi katika kiti cha enzi cha utukufu wake, na mbele zake watakusanyika mataifa yote. Ndipo kila jicho litamwona, na hao waliomchoma. Badala ya taji ya miiba, atavaa taji ya utukufu, - taji katika taji. Badala ya vazi la zamani la zambarau la Kifalme, atavikwa vazi jeupe sana, "asivyoweza dobi duniani kulifanya jeupe" (Marko 9:3). Na katika vazi lake na paja lake kutakuwa na jina limeandikwa "Mfalme wa wafalme, na Bwana wa Mabwana" (Ufunuo 19:16). Wale waliomdhihaki na kumpiga watakuwa pale. Makuhani na watawala wataangalia tena picha katika jumba la hukumu. Kila tukio litaonekana mbele yao, kana kwamba limeandikwa kwa herufi za moto. Ndipo wale walioomba kwamba "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu," watapokea jibu kwa ombi lao. Ndipo dunia yote itakapojua na kufahamu. Watatambua ni nani, na nini viumbe maskini, dhaifu, wenye upeo wamekuwa wakilkipinga. Katika maumivu makali na utisho watailili milima na miamba, "Tuangukieni, tusitirini mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na hazira ya Mwanakondoo. Kwa maana siku iliyo kuu ya hasira yao imekuja naye ni nani awezaye kusimama? (Ufunuo 16:16, 17).

# Kalwari

"Na walipofika mahali paitwapo Kalwari, hapo ndipo walipomsulibisha."

"Ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe" Kristo "aliteswa nje ya lango" (Waebrania 13:12). Kwa kuasi sheria ya Mungu, Adam na Hawa walifukuzwa kutoka Edeni. Kristo, aliye badala yetu, alipaswa kuteswa nje ya mipaka ya Yerusalemu. Alikufa nje ya lango, mahali wakosaji wakubwa na wauaji walipokuwa anauawa. Ni yenye maana halisi maneno yasemayo, "Kristo ametukomboa kutoka katika laana ya torati, maana amefanywa laana kwa ajili yetu" (Wagalatia 3:13).

Mkutano mkubwa ukamfuata Yesu kotoka katika jumba la hukumu hadi Kalwari. Habari za hukumu yake zilienea Yerusalemu yote, na watu wa makundi yote na ngazi zote wakaandamana kuelekea mahali pa kumsulibisha. Makuhani na watawala walifungwa na ahadi ya kutowasumbua wafuasi wa Kristo kama yeye mwenyewe atakabidhiwa kwao, na wanafunzi na waaminio kutoka mjini na maeneo ya jirani waliungana na umati uliokuwa ukimfuata Mwokozi.

Yesu alipovuka lango la baraza la Pilato, msalaba ulioandaliwa kwa ajili ya Baraba uliwekwa juu ya mabega yake yaliyokuwa yamechubuka na yanavuja damu. Wenzi wawili wa Baraba walipaswa kufa wakati mmoja na Yesu, na juu yao pia misalaba iliwekwa. Mzigo wa Mokozi ulikuwa mzito sana kwake katika hali yake ya udhaifu na mateso. Tangu chakula cha Pasaka pamoja na wanafunzi wake, hakuwa amekula chakula wala kunywa chochote. Alikuwa ameomba kwa uchungu katika vita dhidi ya majeshi ya Shetani katika bustani ya Gethsemane. Alivumilia maumivu ya kusalitiwa, na aliona wanafunzi wake wakimkana na kukimbia. Alikuwa amepelekwa kwa Anasi, halafu kwa Kayafa, ha halafu kwa Pilato. Kutoka kwa Pilato alipelekwa kwa Herode, na kurudishwa tena kwa Pilato. Toka matukano hadi matukano mapya, dhihaka hadi dhihaka, mara mbili alipiwa kwa mijeledi, - usiku ule wote kulikuwa na tukio baada ya tukio lenye kufaribu roho ya mtu hadi upeo wa juu sana. Kristo hakushindwa. Hakutamka neno isipokuwa lile lililomtukuza Mungu. Katika mambo yote ya aibu na mizaha ya majaribu, alijivika uthabiti na uadilifu. Lakini baada ya pupigwa mijeledi mara ya pili na msalaba ukawekwa juu yake, asili ya ubinadamu haikuweza kustahimili. Alianguka akizimia chini ya ule mzigo.

Umati uliomfuata Mwokozi uliona hatua zake dhaifu na za kupepesuka, lakini hawakuonyesha huruma yoyote. Walimsuta na kumtukana kwa sababu hakuweza kuchukua msalaba mzito ule. Msalaba uliwekwa juu yake tena, na kwa mara nyingine alianguka kwa kuzimia hadi chini. Watesi wake waliona kuwa haikuwezekana kwake kuuchukua mzigo wake zaidi. Walitatizwa kumpata mtu yeyote atakayebeba mzigo ule wa kudhalilisha. Wayahudi wenyewe hawawezi kufanya hili, kwa sababu unajisi ungewazuia kuitunza Pasaka. Hakuna hata miongoni mwa kundi la watu waliomfuata ambaye angethubutu kuubeba msalaba.

Wakati huo mgeni, Simoni Mkirene, akitokea chamba, anakutana na umati. Anasikia masuto na dhihaka za ufidhuli za makutano; anasikia maneno yakirudiwa kwa dharau, Fanyeni njia kwa Mfalme wa Wayahudi! Anasimama kwa mshangao kwa tukio hili; na anapoonyesha huruma yake, wanamkamata na kuweka msalaba mabegani kwake. Simoni alikuwa amesikia habari za Yesu. Wanawe walikuwa wamemwamini Mwokozi lakini yeye mwenyewe hakuwa Mwanafunzi. Kuubeba msalaba hadi Kalwari ulikuwa mbaraka kwa Simoni, na daima baadaye alikuwa mwenye Shukrani kwa maongozi hayo ya Mungu. Jambo hili lilimwongoza kuuchukua msalaba wa Kristo kwa kuchagua kwa hiari, na daima kwa furaha alisimama chini ya mzigo wake.

Si wanawake wachache wamo katika mkutano uliomfuata Yeye asiyehukumiwa kuelekea mauti yake ya kikatili. Wanakaza kumwangalia Yesu. Baadhi yao walikuwa wamemwona kabla. Baadhi yao walikuwa wamempelekea wagonjwa wao na wale walioteseka. Baadhi walikuwa wameponywa wao wenyewe. Habari za tukio lililotokea zinaelezwa. Wanashangazwa na chuki ya makutano kwake Yeye ambaye mioyo yao inayeyuka na iko tayari kuvunjika. Na bila kujali tendo la umati wenye wenye wazimu, na maneneo ya hasira ya makuhani na watawala, wanawake hawa wanaonyesha huruma

yao. Yesu anapoanguka na kuzimia chini ya msalaba, wanaanza kulia kwa huzuni ya kuomboleza.

Hili ndilo jambo pekee lililomvutia Kristo. Ingawa amejawa na mateso, anapobeba dhambi za ulimwengu hakukosa kujali udhihirisho wa huzuni. Aliwaangalia wanawake hawa kwa huruma na upole. Hawakuwa wamemwanini; alijua kwamba hawakumlilia kwa kuamini kwamba alitumwa na Mungu, lakini walikuwa wameguswa na huruma ya ubinadamu. Hakudharau huzuni yao. Lakii iliamsha katika moyo wake huruma ya kina zaidi kwa ajili yao. "Enyi binti za Yerusalemu," alisema "msinililie mimi, bali jililieni ninyi na watoto wenu." Kutoka katika tukio hilo mbele yake, Kristo aliangalia mbele katika wakati Yerusalemu utakapoharibiwa. Katika tukio hilo la kutisha, wengi wa wale waliokuwa wanalia kwa ajili yake wangeangamia na watoto wao.

Kutoka anguko la Yerusalemu mawazo ya Yesu yalipita hadi kwenye hukumu pana zaidi. Katika uharibifu wa mji uliokataa kutubu aliona mfano wa uharibifu wa mwisho utakaoujia Ulimwengu. Alisema "Ndipo watakapoanza kuiambia milima, tuangukieni; na vilima tufunikeni. Kwani kama wamefanya hivi kwa mti mbichi, itakuwaje kwa mti mkavu?" Kwa kusema mti mbichi, Yesu alijisema Yeye Mwenyewe, Mkombozi asiye na hatia. Mungu aliruhusu ghadhabu yake dhidi ya uasi imwangukie Mwana wake mpendwa. Yesu atasulibiwa kwa ajili ya dhambi za watu. Ni mateso ya kiasi gani basi atakayopata mdhambi atakayeendelea dhambini? Wote wasiotubu na wasioamini watajua huzuni na msiba ambao lugha haiwezi kueleza.

Kati ya makutano waliomfuata Mwokozi hadi Kalwari, wengi walikuwa wamemsindikiza na hosana za furaha na kupunga matawi ya mitende alipoingia Yerusalemu kwa shangwe. Lakini si wachache waliokuwa wamepaza sauti zao kumtukuza kwa sababu ilikuwa mazoea ya wengi, sasa, walipaza makelele kusema "Asulibiwe, Asulibiwe." Wakati Kristo alipoingia Yerusalemu kwa maandamano kama mfalme, matumaini ya wanafunzi yaliinuliwa juu sana. Walikuwa wamemsogelea Bwana wao karibu sana, wakihisi kuwa ni hishima ya juu kuwa na uhusiano naye. Sasa katika jujidhili kwake walimfuata kwa mabali. Walikuwa wamejaa huzuni, na kuinamisha vichawa chini kwa matumaini yaliyokosa kutimizwa. Jinsi gani maneno ya Yesu yalivyothibitishwa: "Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu; kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga Mchungaji, na kondoo wa kundi lake watatawanyika" (Mathayo 26:31).

Walipofika mahali pa kuulia, wafungwa walifungwa kwenye vifaa vya mateso. Wezi wawili walishindana na wale waliowaweka msalabani; lakini Yesu hakufanya upinzani wowote. Mama yake Yesu, akisaidiwa na Yohana, mwanafunzi mpendwa, alikuwa amefuata nyayo za Mwanae hadi Kalwari. Alikuwa amemwona akizimia chini ya mzigo wa msaaba, na alitamani sana kuweka mkono wa msaada chini ya kichwa chake kilichojeruhiwa, na kuosha uso ule ambao hapo zamani uliegemea kifuani pake. Lakini hakuruhusiwa nafasi hii ya majonzi. Pamoja na wanafunzi bado alishiilia matumaini wamba Yesu ataonyesha uwezo wake, na kujiokoa mwenyewe toka kwa maadui zake. Mara moyo wake ulishuka chini alipokumbuka maneno ambayo kwayo alikuwa ametabiri tukio ambalo lilikuwa linatendeka wakati huo. Wale wezi walipokuwa wakifungwa kwenye misalaba, aliangalia kwa wasiwasi kwaa uchungu. Je, Yeye aliyekuwa amewapa uhai waliokufa ataruhusu yeye mwenyewe asulibiwe? Je, Mwana wa Mungu ataruhusu yeye mwenyewe auawe kikatili hivyo? Je akane imani yake kwamba Yesu alikuwa Masihi? Je, ashuhudie aibu na huzuni yake bila nafasi ya

kumhudumia katika fadhaa yake? Aliona mikono yake ikinyooshwa msalabani; nyundo na misumari viiletwa, na misumari kikapigiliwa kupenya nyama laini, kwa mioyo iliyo na huzuni wanafunzi waliuchukua kutoka kwanye tukio hili la kikatili mwii uliozimia wa mama yake Yesu.

Mwokozi hakufanya manung'uniko yoyote ya kulalamika. Uso wake ulibakia mtulivu na shwari, lakini matone makubwa ya jsho yalisimama usoni. Hakukuwa na mkono wenye huruma wa kupangusa umande wa mauti toka usoni pake, wala hakuna maneno ya huruma na uadilifu usiobadilika kuzuia moyo wake wa kibinadamu. Wakati maaskari wakifanya kazi yao ya kuogofya, Yesu aliomba kwa ajili ya adui zake, "Baba uwasamehe, kwa kuwa hawajui watandalo." Mawazo yake yalihama toka maumivu yake mwenyewe hadi kwenye dhambi ya wale watesi wake, na malipo ya kutisha yatakayowapata. Hakuna laana iliyotolewa kwa maaskari waliokuwa wakimtendea vibaya. Hakuna kisasi kilichoombwa kuja juu ya makuhani na watawala, waliokuwa wakitazama kwa furaha juu ya kufanikisha kusudi lao. Kristo aliwahurumia katika ujinga na hatia yao. Alipumua tu ombi la msamaha kwao, - "Kwa kuwa hawajui watendalo."

Kama wangejua kwamba walikuwa wakimtesa Yeye aliyekuja kuokoa kizazi hiki cha dhambi kutoka uharibifu wa milili, wangeshikwa na majuto na itisho. Lakini kutokujua kwao hakukuondoa hatia yao; kwa sababu ilikuwa ni haki yao kumfahamu na kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Baadhi yao bado wangetambua dhambi yao, na kutubu na kuongoka. Baadhi kwa kutotubu kwao wangefanya isiwezikane kwa ombi la Kristo kujibiwa wa ajili yao. Hata hivyo, kusudi la Mungu lilikuwa linafikia utimilizo wake. Yesu alikuwa anapata haki ya kuwa mtetezi wa watu mbele za Baba.

Lile ombi la Kristo kwa ajili ya watesi wake lilijumuisha dunia yote. Lilimjumuisha kila mdhambi aliyewahi kuishi au angeishi, tangu mwanzo wa dunia hadi mwisho wa wakati. Juu ya wote iko hatia ya kumsulibisha Mwana wa Mungu. Kwa wote, msamaha unatolewa bure. "Yeyote atakaye" anaweza kuwa na amani na Mungu, na kurithi uzima wa milele.

Mara tu Kristo alipopigiliwa msalabani, uliinuliwa na watu wenye nguvu, na kwa nguvu sana ukashushwa mahali palipoandaliwa. Hii ilisababisha maumivu makali sana kwa Mwana wa Mungu. Pilato akaandika maneno kwa Kiebrania, Kiyunani na Kilatini na kuyaweka juu ya msalaba, juu ya kichwa cha Yesu. Yalisoma "Yesu wa Nazereti Mfalme wa Wayahudi." Maandishi haya yaliwaudhi Wayahudi. Katika baraza ya Pilato walipiga kelele, "Msulibishe." "Sisi hatuna mfalme ila Kaisari" (Yohana 19:15). Walikuwa wametangaza kwamba yeyote atakayemkubali mfalme mwingine ni msaliti. Pilato aliandika fikra waliyokuwa wameionyesha. Hakuna kosa lililotajwa, isipokuwa kwamba Yesu alikuwa mfalme wa Wayahudi. Maneno yale yalikuwa kukubali kwa kweli utee wa Wayahudi kwa nguvu za Kirumi. Yalitangaza kuwa yeyote atakayedai kuwa mfalme wa Israeli angehukumiwa nao kuwa anastahili kufa. Makuhani walikuwa wamefanya hila iliyowageukia wao wenyewe. Walipokuwa wanafanya hila ya kumwua Kristo, Kayafa alisema kuwa yafaa mtu mmoja afe ili taifa zima lisiangamie. Sasa unafiki wo ulifunuliwa. Ili kumwangamiza Kristo, walikuwa tayari kuuza hata kuwepo kwa taifa lao.

Makuhani waliona kile walichokuwa wamefanya, nao wakamwomba Pilato abadilishe maelezo. Walisema "Usiandike, Mfalme wa Wayahudi; lakini kwamba, Yeye alisema, Mimi ni mfalme wa Wayahudi. Lakini Pilato alijikasirikia mwenyewe kwa sababu ya

udhaifu aliouonyesha mwanzoni, na aliwadharau kabisa makuhani na watawala wenye wivu na hila. Alijibu kwa moyo mzito, "Niliyoandika nimeandika."

Nguvu ya juu zaidi ya Pilato au Wayahudi ilielekeza uwekwaji wa yale maneno juu ya kichwa cha Yesu. Kwa maongozi ya Mungu yangeamsha fikra na kushunguza maandiko. Hahali Yesu aliposulibiwa palikuwa karibu na mjini. Maelfu ya watu kutoka nchi zote walikuwa Yerusalemu wakati huo, na maandishi yaliyokuwa yanamtangaza Yesu wa Nazareti kuwa Masihi yangeonekana kwao. Ulikuwa ni ukweli ulio hai, ulionakiliwa na mkono ambao Mungu aliliuongoza.

Katika mateso ya Kristo juu ya msalaba unabee ulitimilizwa. Karne nyingi kabla ya kusulibiwa, Mwokozi alitabiri jinsi ambavyo angetendewa. Alisema "Kwa maana, mbwa wamenizunguka Mimi, kusanyiko la waovu wamenisoga, wamenichoma mikono na miguu. Naweza kuhesabu mifupa yangu yote; wao wananitazama na kunikodolea macho. Wanagawanya nguo zangu na vazi langu wanalipigia kura" (Zaburi 22:16-18). Unabee kuhusu mavazi yake ulitekelezwa pasipo kuingiliwa na marafiki au maadui wake yule aliyesulibiwa. Kwa maaskari waliokuwa wamemweka msalabani, ndiko mavazi yalikokwenda. Kristo alisikia mashindano yao walipokuwa wakigawanya mavazi yake kati yao. Vazi lake lilifumwa moja kwa moja bila upindo, nao wakasema "Tusiipasue, lakini tuipigie kura, iwe ya nani."

Katika unabii mwingine Mokozi alitangaza, "Laumu imenivunga moyo, nami ninaugua sana. Nikangoja aje wa kunihurumia, wala hakuna; Na wakunifariji, wala sikuona mtu. Wakanipa uchungu kuwa chakula changu; Nami nilipokuwa na kiu wakaninywesha siki" (Zaburi 69:20, 21). Kwa wale walioteswa kwa kifo cha msalaba, iliruhusiwa kuwapatia dawa ya kupumbaza, ili kutuliza maumivu. Hii ilitolewa kwa Yesu; lakini alipoionja, aliikataa. Asingepokea chochote ambacho kingeduwaza akili zake. Imani yake lazima imshikilie sana Mungu. Hii tu ndio ilikuwa nguvu yake. Kuduwaza hisia zake kungempatia Shetani faida.

Maadui wa Yesu walionyesha wazi hasira yao kwake alipokuwa juu msalabani. Makuhani, watawala na waandishi waliungana na kundi la watu kumdhihaki Mwokozi aliyekuwa anakufa. Wakati wa kubatizwa na alipobadilika sura sauti ya Mungu ilisikika ikitangaza kuwa Kristo ni Mwana wake. Tena, kabla ya Kristo kusalitiwa, Baba alikuwa ametamka, akishuhudia Uungu wake. Lakini sasa sauti kutoka mbinguni ilikuwa kimya. Hakuna ushuhuda kwa ajili ya Kristo uliosikika. Peke yake alivumilia uchungu wa kunyanyaswa na dhihaka kutoka kwa watu waovu.

"Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu" walisema "shuka toka msalabani." "Na ajiokoe mwenyewe, kama yeye ni Kristo, mteule wa Mungu." Katika jangwa la majaribu Shetani alisema "Kama wewe ne Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate." "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini" kutoka kwenye kilili cha hekalu. Mathayo 4:3, 6. Na Shetani na malaika zake katika umbile la kibinadamu walikuwepo pale msalabani. Mkuu wa pepo na majeshi yake walikuwa wakishirikiana na makuhani na watawaa. Waalimu wa watu waliwachochea umati usiojua kutamka hukuu dhidi ya Mmoja ambaye wengi wao hawakuwahi kumtazama, hadi walipolazimishwa kutoa ushahidi dhidi yake. Makuhani, watawala, mafarisayo na umati ule wenye mioyo migumu walipatana pamoja katika wazimu wa kishetani. Viongozi wa kidini waliungana na Shetani na malaika zake. Walikuwa wanafanya maagizo yake.

Yesu, katika mateso na mauti, alisikia kila neno makuhani walipotangaza, "Aliokoa wangine; Mwenyewe hawezi kujiokoa. Yeye ni mfalme wa Isreali; na ashuke sasa

Msalabani naye tutamwamini." Kristo angeweza kushuka chini kutoka msalabani. Lakini ni kwa sabau hakukujiokoa mwenyewe mdhambi anamatumaini ya msamaha na upendeleo kwa Mungu.

Katika dhihaka yao kwa Mwokozi, watu waliodai kuwa wafafanuzi wa unabii walikuwa wanarudi maneno yale yale ambayo uvuvio ulitabiri kwamba watayatamka katika tukio hili. Lakini katika upofu wao hawakuona kama wanatimiza unabii. Wale ambao kwa dhihaka walitamka maneno haya "Alimtumaini Mungu, na Amwokoe sasa, kama Anamtaka, kwa maana alisema, Mimi ni Mwana wa Mungu," walifikiria kidogo sana kuwa ushahidi wao ungeendelea kusikika hata mwisho wa wakati. Lakini ijapokuwa maneno yale yalisemwa kwa dhihaka, yaliwaongoza watu kuchunguza maandiko kuliko walivyowahi kufanya kabla. Wenye hekima walisikia, wakachunguza, wakatafuakari na kuomba, Kuna wale ambao hawakutulia hadi, kwa kulinganisha andiko na andiko, waliona maana ya utume wa Kristo. Kamwe kabla hakukuwahi kuwepo maarifa ya watu wote, kumhusu Yesu kuliko wakati alipokuwa juu ya msalaba. Katika mioyo ya wengi walioangalia tukio la kusulibishwa, na waliokuwa wamesikia maneno ya Yesu, nuru ya ukweli ilikuwa ikiangaza.

Kwa Yesu katika maumivu yake msalabani ulikuja mngao mmoja wa faraja. Lilikuwa ombi la mwivi aliyetubu. Watu wote waliosulibiwa pamoja na Yesu mwanzoni walimshutumu sana, na mmoja katika mateso yake alizidi tu kukata tamaa na kuwa jeuri. Lakini haikuwa hivyo kwa mwenzake. Mtu huyu hakuwa mhalifu mkaidi; alikuwa amepotoshwa na urafiki usiofaa, lakini hatia yake haikuwa kbwa sana kuliko wengi a wale waliosimama kando ya msalaba wakimtukana Mwokozi. Alikuwa amemwona na kumsikia Yesu, na alikuwa amethibitiswha moyoni na mafundisho yake, lakini alikuwa amegeuzwa nia na makuhani na watawala. Akitafuta kukomesha wongofu, alikuwa amezama chini na chini zaidi dhambini, hadi alipokamatwa, kuhojiwa kama mhalifu, na kuhukumiwa kifo cha msalabani. Katika ukumbi wa baraza na njiani kwenda Kalwari alikuwa pamoja na Yesu. Alimsikia Pilato akitangaza "Sioni hatia yoyote kwake" (Yohana 19:4). Alikuwa ameona hali yake ya Uungu, na huruma yake ya msamaha kwa watesi wake. Akiwa msalabani anaona washika dini wakuu wengi wakitupa ndimi zao kwa dhihaka na vicheko vya mzaha kwa Bwana Yesu. Anaona vichwa vinavyotikiswa. Anasikia matamshi ya kukaripia yakichukuliwa na mwivi mwenzake: "Ikiwa wewe ndiye Kristo, jiokoe mwenyewe na sisi." Miongoni mwa wapitaji anawasikia wengi wakimtetea Yesu. Anawasikia wakirudia maneno yake na kusimulia matendo yake. Anasadikishwa tena kwamba huyu ni Kristo. Anamgeukia mhalifu mwenzake na kumwambia, "Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo?" Wevi hawa wanaokufa hawana chochote cha kuogopa tena kwa wanadamu. Lakini kwa mmoja wao anathibitishwa kwa dhati kwamba kuna Mungu wa kuogopwa, na wakati juao unaomfanya atetemeke. Na sasa, kwa jinsi yalivyochafuliwa na dhambi, maisha yake yanakaribia mwisho. "Nayo ni haki kwetu sisi," anaugua "kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lolote lisilofaa."

Hakuna swali sasa. Hakuna mashaka, hakuna mashutumu. Alipohokumiwa kwa uhalifu wake, yule mwivi alipoteza matumaini na kukata tamaa; lakini mawazo mageni, ya upole yaliamshwa. Anakumbuka yote aliyosikia kuhusu Yesu, jinsi alivyoponya wagonjwa na kusamehe dhambi. Alisikia maneno ya wale waliomwamini Yesu na kumfuata huku wakilia. Aliona na kusoma maandishi yaliyokuwa juu ya kichwa cha Mwokozi. Amewasikia wapita njia wakiyarudia, wengine kwa midomo yenye huzuni na

kutetemeka, wengine kwa mzaha na dhihaka. Roho Mtakatifu anaangaza akili zake, na kidogo kidogo mnyororo wa ushahidi unaunganishwa pamoja. Katika Yesu, aliyechubuliwa, kudhihakiwa, na akiwa juu ya msalaba, anamwona Mwanakondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu. Matumaini yanachanganyika na maumivu katika sauti yake kama roho isiyo na msaada na inayokufa, anajisalimisha kwa Mwokozi aliye kifone. "Vwana nikumbuke" analia "siku Utakapokuja katika ufalme wako."

Haraka jibu lilikuja. Sauti nyororo na ya kupendeza, iliyojaa upendo, huruma na nguvu ilisema; Amin, nakwambia leo hivi, utakuwa nami Peponi.

Kwa masaa mengi ya maumivu, matukano na dhihaka viliingia masikioni mwa Yesu. Akiwa juu msalabani, bado sauti za mizaha na laana zanamfuata. Kwa moyo wenye shauku alitafuta kusikia maneno yaonyeshayo imani kutoka kwa wanafunzi wake. Alikuwa amesikia tu maneno ya maombolezo, "Tulitumaini kwamba Yeye ndiye atawakomboa Israeli." Ilkuwa ya kupendeza jinsi gani kwa Mwokozi matamshi ya imani na upendo toka kwa mwivi huyu afaye! Wakati viongozi wa Kiyahudi wanamkana, na hata wanafunzi wake wanaona mashaka kwa Uungu wake, mwivi maskini, akiwa ukingoi mwa umilele, anamwita Yesu Bwana. Wengi walikuwa tayari kumwita Bwana alipofanya miujiza, na baada ya kufufuka kutoka kaburini; lakini hakuna hata mmoja anayemkubali anapokuwa juu msalabani katika mauti isipokuwa mwivi aliyetubu aliyeokolewa saa kumi na moja.

Wale waliosimama kando walisikia maneno ya yule mwivi alipomwita Yesu Bwana. Sauti ya mtu aliyetubu ilivuta usikivu wao. Wale ambao chini ya msalaba walikuwa wakigombania mavazi ya Kristo, na kupigia kura vazi lake walisimama ili kusikiliza. Sauti zao za hasira zilikomeshwa. Kwa pumzi za wasiwasi wanamtazama kristo, na kusubiri jibu kutoka midomo ili iliyokuwa kifoni.

Alipotamka maneno ya ahadi, kiwingu cheusi kilichoonekana kuuzinga msalaba kilipenywa na nuru ing'aayo nailiyo hai. Kwa mwivi aliyetubu ilikuja amani kamilifu ya kukubaiwa na Mungu. Kristo katika kujidhili kwake alitukuzwa. Yeye ambaye machoni pa wote alionekana kushindwa alikuwa Mshindi. Alitambulika kama mbeba chambi. Watu wanaweza kuonyesha uwezo juu ya mwili wake wa kibinadamu. Wanaweza kuchoma vipaji vyake (uso) kwa taji ya miiba. Wana weza kumvua nguo na kushindana katika kuigawanya. Lakini hawawezi kumnyang'anya uwezo wake wa kusamehe dhambi. Katika kufa anashuhudia Uungu wake na kwa utukufu wa Baba. Sikio lake si zito kwamba hawezi kusikia, wala makono wake haukupungua kwamba usiweze kuokoa. Ni haki yake ya kifalme kuokoa hata upeo wote wamjiao Mungu kwa Yeye.

Ninakwambia leo hivi, utakuwa nami Peponi. Kristo hakuahidi kwamba yule mwivi atakuwa naye Peponi siku ile. Yeye mwenyewe hakwenda Peponi siku ile. Alilala kaburini, na katika asubuhi ya ufufuo alisema "Sijapaa bado kwenda kwa Baba" (Yohana 20:17). Lakini katika siku ya kusulibiwa, siku ya mwonekano dhahiri wa kushindwa na giza, ahadi ilitolewa. "Leo" wakati anakufa msalabani kama mhalifu, Kristo anamhakikishia mdhambi maskini, utakuwa nami Peponi.

Wevi waliosulibiwa na Yesu waliwekwa "Kila upande mmoja na Yesu katikati." Hili lilifanywa kwa maelekezo ya makuhani na watawala. Nafasi ya Kristo katikati ya wevi ilionyesha kwamba yeye ndiye aliyekuwa mhalifu mkuu kati yao watatu. Hivyo yalitimizwa maandiko, "Alihesabiwa pamoja na wakosaji" (Isaya 53:12). Lakini maana kamili ya tendo lao makuhani hawakuona. Kwa Yesu, Akisulibiwa pamoja na wevi, aliwekwa "katikati," vivyo msalaba wake uliwekwa katikati ya dunia iliyokuwa

dhambini. Na maneno ya samaha yaliyosemwa kwa mwivi aliyetubu yaliwasha nuru ambayo itang'aa hadi mipaka ya ndani kabisa ya kunia.

Kwa mshangao malaika walitazama upendo wa Yesu usio kifani, ambaye, katika mateso makali ya akili na mwili, aliwafikiria tu wengine, na kumtia moyo aliyetubu kuamini. Katika kujidhili kwake Yeye kama nabee alikuwa amewahubiri binti za Yerusalemu; kama kuhani na wakili alimsihi Baba kuwasamehe watu wale waliomuua; kama Mwokozi mwenye upendo alisemehe dhambi za wivi aliyetubu.

Macho ya Yesu yalipokuwa yanaangaza kwenye umati uliomzunguka, sura moja ilivuta mawazo yake. Chii ya msalaba alisimama mama yake, akiwa maeshikiliwa na mwanafunzi Yohana. Hakuweza kuvumilia kuwa mbali na mwanawe; na Yohana, akijua kuwa mwisho ulikuwa karibu, alikuwa amemleta tena pale msalabani. Katika saa Yake ya kufa, Kristo alimkumbuka mama yake. Akiangalia uso wake wenye majonzi na tena kwa Yohana, alimwambia, "Mama tazama mwanao!" halafu kwa Yohana, alisema "Tazama mama yake!" Yohana alielewa maneno ya Kristo, naakakubali jukumu hilo. Naye tangu hapo akamchukua Mariamu nyumbani kwake na kumtunza kwa upole. Ee, Mwokoze mwenye huruma na upendo; katika maumivu yake makali ya mwili na akili, alikumbuka utunzaji wa mama yake. Hakuwa na fedha za kutoa ili kumfariji, lakini alikuwa ni hazina moyoni mwa Yohana, na alimkabidhi mama yake kama wosia wa thamani. Hivyo alimpatia mama yake kile alichohitaji sana, -huruma ya upole ya yule aliyempenda kwa sababu alimpenda Yesu. Na katika kumpokea kama jukumu takatifu, Yohana alikuwa anapokea mibaraka mikuwa. Alikuwa kumbukumbu ya kudumu ya bwana wake ampendaye.

Mfano kamili wa Kristo wa wajibu wa upendo kwa wazazi huangaza mbele kwa utukufu usiofifia kati ya ukungu wa miaka. Kwa karibu miaka thelathini Yesu kwa kazi zake za kila siku alikuwa amesaidia kubeba mzigo wa nyumbani. Na sasa, hata katika maumivu makali ya mwisho, anakumbuka kutoa kwa ajili ya mama yake mwenye huzuni, na mjane. Roho hiyo hiyo itaonekana kwa kila mwanafunzi wa Bwana wetu. Wale wanaomfuata Kristo watahisi kwamba ni sehemu ya dini yao kuheshimu na kuwatunza wazazi wao. Katika moyo ulio na upendo wa Kristo, baba na mama hawatakosa kupata utunzaji wa kufaa na huruma ya upole.

Na sasa Bwana wa utukufu alikuwa anakufa, ukombozi kwa wanadamu. Kwa kutoa uhai wake wa thamani, Kristo hakutukuzwa kwa furaha ya ushindi. Kila kitu kilionekana kuwa giza lililolemea. Haikuwa hofu ya mauti iliyomlemea. Hayakuwa maumivu na aibu ya msalaba vilivyosababisha maumivu yake yasiyoelezeka. Kristo alikuwa mfalme wa watesekao; lakini mateso yake yalitokana na hisia ya ubaya wa dhambi, ujuzi ambao kutokana na kuzoelea dhambi, mwanadamu amekuwa kipofu kwa ubaya wake. Kristo aliona jisi kilivyo kina cha nguvu ya dhambi katika moyo wa mwanadamu, wachache jinsi gani watakaokuwa tayari kutoka katika nguvu zake. Alijua kwamba pasipo msaada kutoka kwa Mungu, wanadamu lazima waangamie, na aliona makutano wakiangamia mahali wanapoweza kupata msaada tele.

Juu ya Kristo kama badala yetu na dhamana yetu, iliwekwa hatia yetu sote. Alihesabiwa mkosaji, ili aweze kutukomboa kutoka hukumu ya sheria. Hatia ya kila mzao wa Adamu ilielemea moyo wake. Ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi, udhihirisho wa kutisha wa hasira yake juu ya uovu, ilijaza moyo wa mwanawe na wasiwase. Katika maisha yake yote Kristo alikuwa ameutangazia ulimwengu ulioanguka habari njema za rehema za Baba wa upendo wa msamaha. Wokovu kwa Mdhambi mkuu

lilikuwa somo lake kuu. Lakini sasa pamoja na uzito wa hatia utishao ulio juu yake, hawezi kuuona uso wa upatanisho wa Baba. Kuondolewa kwa uso wa Uungu kutoka kwa Mwokozi katika saa hii ya maumivu makuu kulichoma moyo wake na huzuni isiyoweza kufahamiwa na wanadamu. Maumivu haya yalikuwa makubwa sana kiasi cha kutohisi maumivu ya kimwili.

Shetani na majaribu yake makali alisonga moyo wa Yesu. Mwokozi hakuweza kuona zaidi ya mlango wa kaburi. Tumaini halikumpatia kuona kutoka kwake kaburini kama mshindi, au kumweleza ukubali wa Baba kwa kafara yake. Aliogopa kwamba dhambi ilikuwa ya kuchukiza sana kwa Mungu kiasi kwamba utengano wao utakuwa wa milele. Kristo alipata maumivu ambayo mdhambi atayapata wakati rehema itakapokoma kusihi kwa ajili ya kizazi chenye hatia. Ilikuwa hisia ya dhambi, ikileta hasira ya Baba juu yake aliye badala ya wanadamu, iliyofanya kikombe alichokinywea kuwa kichungu sana, na kuvunja moyo wa Mwana wa Mungu.

Kwa mshangao mkubwa sana malaika walishuhudia maumivu makuu ya kukata tamaa ya Mwokozi. Majeshi ya mbinguni yalifunika nyuso zao toka tukio hili la kuogofya. Viumbe asili visivyo hai vilionyesha huzuni pamoja na uumba wao aliyedhihakiwa na aliyekuwa anakufa. Jua lilikataa kuangalia picha hii ya kutisha. Miali yake kamili na angavu ilimulika dunia wakati wa mchana, na mara ghafla lilionekana kutoweka. Giza kamili, kama nguo ya kufunika jeneza, liliuzunguka msalaba. “Kulikuwa na giza juu ya nchi yote hadi saa tisa.” Hakukuwa na kupatwa kwa jua wala sababu nyingine ya asili ya giza hili lililokuwa zito kama usiku wa manane bila mwizi wala nyota. Ulikuwa muujiza wa ushuhuda uliotolewa na Mungu ili imani ya vizazi vijavyo ithibitike.

Katika giza lile nene kuwepo kwa Mungu kulifichwa. “Hufanya giza kuwa hema yake, na kuficha utukufu wake machoni pa wanadamu.” Mungu na malaika zake watakatifu walikuwa kando ya msalaba. Baba alikuwa pamoja na Mwanawe. Lakini kuwepo kwake hakukudhihirihwa. Laiti utukufu wake ungemulika kutoka katika wingu, kila mtazamaji wa kibinadamu angeangamizwa. Na katika saa hiyo ya kuogofya Kristo asingefarijiwa kwa uwepo wa Baba. Alikanyaga shinikizo peke yake, na katika watu hapakuwa na mmoja pamoja naye.

Katika giza nene, Mungu alifunika maumivu ya mwisho ya ubinadamu wa Mwana wake. Wote waliomwona Kristo katika mateso yake walikuwa wamethibitishwa kuhusuUungu wake. Uso ule, uliokuwa umetazamwa na wanadamu, kamwe haukusahauliwa. Kama uso wa Kaini ulivyoonyesha hatia yake kama muuaji, vivyo uso wa Kristo haukuonyesha hatia, bali amani, ukarimu, - sura ya Mungu. Lakini washitaki wake hawakujali ishara ya mbinguni. Katika masaa mengi ya maumivu Kristo alitazamwa na mkutano wenye dhihaka. Sasa kwa rehema alifishwa na joho la Mungu.

Kimya cha Kaburii kilionekana kufika juu ya Kalwari. Hofu isiyo na jina iliwashika umati uliokusanyika kando ya msalaba. Kulaani na kudhihaki vilikoma kati ya sentensi zisizokamilika. Waume, wake na watoto walianguka chini kifudifudi. Umeme wa dhahiri mara kadhaa ulionekana kutoka katika wingu, na kudhihirisha msalaba na Mkombozi aliyesulibiwa. Makuhani, watawala, waandishi, wauaji na watu, wote walifikiri kwamba muda wa kupatilizwa umefika. Baada ya muda mfupi, baadhi walinong’ona kwamba sasa Yesu atashuka toka msalabani. Wengine walijaribu kupapasa njia ya kurudi mjini, wakijipigapiga vifuani na kulia kwa huzuni ya woga.

Ilipofika saa tisa giza liliondoka kwa watu, lakini liliendelea kumfunika Mwokozi. Ilikuwa ni alama ya maumivu na utisho uliokuwa ukielemea moyo wake. Hakuna jisho

ambalo lingeweza kupenya giza lililouzuguka msalaba, na hakuna ambalo lingeweza kupenya giza la kina zaidi lililozunguka roho iliyokuwa ikiteseka ya Kristo. Umeme wenye hasira ulionekana kumwelekea kwa nguvu akiwa juu ya msalaba. Halafu "Yesu akalia kwa sauti kubwa, akisema, Eloi, Eloi, lama sabactani?" "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Giza lilipomzunguka Mwokozi, sauti nyingi zilisikika zikisema: kisasi cha mbingu kiko juu yake. Mishale Ya Ghadhabu ya Mungu imeelekezwa kwake, kwa sababu alidai kuwa Mwana wa Mungu. Wengi waliomwamini walisikia kilio chake cha kukata tamaa. Tumaini lilimwacha kama Mungu alimwacha Yesu, wafuasi wake watumainie kitu gani?

Wakati giza lilipoondoka kutoka roho ya Kristo iliyoteseka, aliamshwa kwa hisia ya maumivu ya kimwili, na kusema, "Naona kiu." Mmoja wa maaskari wa Kirumi, akiguswa na huruma alipoangalia midomo iliyoshidishwa kwa kiu, alidhukua sifongo kwa mti wa hisopo, na kuichovya kwenye chombo cheye siki, na kumpatia Yesu. Lakini makuhani walidhihaki maumivu yake. Giza lilipoifunika nchi, waliingiwa na woga, hofu yao ilipopungua, waliogopa tena kuwa Yesu bado angeweza kuwatoroka. Maneno yake "Eloi, Eloi, lama sabaktani?" waliyafasiri vibaya. Kwa dharau ya uchungu na dhihaka walisema, "Huyu mtu anamwita Eliya." Nafasi ya mwisho kupunguza mateso yake waliikataa. "Acheni" walisema "na tuone kwamba Eliya anakuja kumwokoa."

Wana wa Mungu asiye na doa aliangikwa msalabani, mwili wake ukiwa umechubuliwa kwa kupigwa, mikono ile ambayo mara nyingi ilinyooshwa kubariki, ikiwa imepigiliwa misumari kwenye mti, miguu ile isiyochoka kwa huduma za upendo, imepigwe misumari kwenye mti; kichwa kile cha kifalme kikiwa kie chomwa kwa taji ya miiba, midomo ile iliyotetemeka ikiwa imetengenezwa kwa kilio cha ole (misiba). Na yote aliyovumilia – matone ya damu yaliyochuruzika kishwani, mikononi, miguuni, maumivu yaliotesa umbile lake, na maumivu yasiyoelezeka yaliyojaza roho yake uso wa Baba yake ulipofichwa – huzungumza kwa kila mwanadamu, vikitangaza kuwa, ni kwa ajili yako Mwana wa Mungu anakubali kubeba mzigo huu wa hatia, kwa ajili yako anaharibu utawala wa mauti, na kufungwa malengo ya Paradiso. Yeye aliyetuliza mawimbi yenye hasira na kutembea katika mawimbi makubwa yaliyofunikwa povu, aliyewafanya mashetani kutetemeka na magonjwa kukimbia, aliyefungua macho ya vipofu na kufufua wafu, - anajitoa mwenyewe juu ya msalaba kama kafara, na hii ni kutokana na upendo kwako. Yeye, mbeba dhambi, anavumilia hasira kali ya haki ya Mungu, na kwa ajili yako anakuwa dhambi yenyewe.

Wakiwa kimya watazamaji walisubiri mwisho wa tukio hili la kutisha. Jua liliangaza tena, lakini msalaba bado ulifunikwa na giza. Makuhani na watawala walitazama kuelekea Yerusalemu; na ona, wingu zito lilitulia juu ya mji na bonde lote la Uyahudi. Jua la Haki, Nuru ya Ulimwengu, lilikuwa linaondoa miali yake toka mji uliokuwa umependelewa wa Yerusalemu. Umeme wa nguvu wa hisira ya Mungu ulielekezwa dhidi ya mji uliohukumiwa adhabu.

Ghafla giza lilitoweka msalabani, na kwa sauti dhahiri kama tarumbeta, iliyoonekana kurudisha mwangwi kwa viumbe vyote, Yesu alisema "Imekwisha." "Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." Nuru iliuzuka msalaba, na uso wa Mwokozi ukang'aa kwa utukufu kama jua. Halafu akainamisha kichwa chake kifuani, akafa.

Kati ya giza la kutisha, ikionikana kwamba amekataliwa na Mungu, Kristo alikuwa ameondoa chembechembe za mwisho za misiba ya wanadamu. Katika masaa yale ya kutisha alikuwa ametumainia ushahidi wa kukubaliwa na Baba aliokuwa amepewa.

Alkuwa anaijua tabia ya Baba yake vizuri, aliifahamu haki yake, rehema na uendo wake mkuu. Kwa imani alipumzika kwake yeye ambaye daima ilikuwa furaha yake kumtii. Na kwa unyenyekevu alipojisalimisha kwa Mungu, hisia ya kupoteza upendo wa Baba iliondolewa. Kwa imani Kristo alikwa Mshindi.

Kamwe kabla dunia haikuwahi kushuhudia tukio kama hilo. Makutano walisimama wameishiwa nguvu, na kwa pumziza woga walimtazama Mwokozi. Mara giza lilitanda tena juu ya nchi, na ngurumo iliyopwea, kama radi nzito, ilisikika. Kulikuwa na tetemeko kuu la nchi. Watu walitetemeswa pamoja katika makundi. Wazimu na fadhaa viliwashika. Katika milima iliyokuwa karibu miamba ilipasuka, na ilikwenda na kutupwa kwa kugongana uwandani. Makaburi yalifunuka, na wafu wakatupwa nje kutoka makaburini mwao. Viumbe vilionekana kutetemeka hadi chembe ndogo kabisa. Makuhani, watawala, maaskari, wauaji, na watu, wakiwa kimya kwa hofu, walilala kufudifudi juu ya nchi.

Wakati kilio kikuu, "Imekwisha" kilipotoka mdomoni pa Kristo, makuhani walikuwa wakihudumu hekaluni walikuwa wakihudumu hakaluni. Ilikuwa ni saa ya dhabihu ya jioni. Kondoo aliyemwakilisha Kristo aliletwa ili kuchinjiwa. Katika mavazi rasmi na yenye kupendeza, kuhani alisimama na kisu kilichoinuliwa kama alivyofanya Ibrahimu alipokuwa tayari kumchinga Mwanawe. Kwa shauku watu waliangalia. Lakini nchi inatikisika na kutetemeka; maana Bwana Mwenyewe anakaribia. Kwa sauti ya kuchanika pazia la ndani la hekalu linapasuka toka juu hadi chini kwa mkono usioonekana, na kufungua wazi watu kutazama mahali ambapo awali palijazwa na kuwepo kwa Mungu. Katika mahali hapo Shekina ilikaa. Hapo Mungu alionyesha utukufu wake juu ya kiti cha Rehema. Hakuna mtu, isipokuwa kuhani Mkuu aliyefunua pazia lililotenganisha chumba hiki na sehemu nyingini za hekalu. Aliingia hapo mara moja kwa mwaka kufanya upatanisho kwa dhambi za watu. Lakini ona, pazia hili linapasuliwa vipande viwili. Patakatifu sana pa hema ya duniani siyo wakfu tena.

Yote ni kitisho na machafuko. Kuhani yu tayari kumchinga mnyama; lakini kisu kinadondoka kutoka mkono wake ulio na ganzi na kondoo anatoweka. Mfano umekutana na kitu halisi katika kifo cha Mwana wa Mungu. Kafara kuu imetolewa. Njia ya kupaingia Patakatifu imefunguliwa. Njia mpya iliyo hai imeandaliwa kwa wote. Mwanadamu mdhambi na mwenye huzuni haitaji tena kusubiri kuja kwa huhani mkuu. Tangu sasa Mwokozi angehudumu kama kuhani na wakili katika mbingu za mbingu. Ilikuwa kana kwamba sauti iliyo hai iliwaambia waabuduo: Sasa ni mwisho wa kafara na sadaka zote kwa ajili ya dhambi. Mwana wa Mungu amekuja sawasawa na neno lake, "Tazama nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) niyafanye mapenzi yako Mungu." "Bali kwa damu yake Mwenyewe" aliingia "mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele kwa ajili yetu" (Waebrania 10:7; 9:12).

Imekwesha

Kristo hakutoa uhai wake hadi alipokamilisha kazi aliyokuja kuifanya na pamoja na kutengana na pumzi yake, alisema "Imekwisha" (Yohana 19:30). Ameshinda vita. Mkono wake wa kuume na mkono wake mtakatifu ndio uliomshindia. Kama Mshindi alisimamisha bendera yake katika vilele vya milele. Je, hakukuwa na furaha miongoni mwa malaika? Mbingu zote zilishangilia ushindi wa Mwokozi. Shetani alishindwa, na akajua kuwa ufalme wake ulikuwa umepotea.

Kwa Malaika na dunia ambazo hazikuasi kilio kuwa "Imekwisha" kilikuwa na ishara ya kina. Ilikuwa ni kwa ajili yao na kwa ajili yetu kwamba kazi kubwa ya ukombozi ilikuwa imekamilishwa. Wao na sisi tunashirikiana matunda ya ushindi wa Kristo.

Ni hadi kifo cha Kristo ndipo tabia ya shetani ilidhihirika wazi kwa malaika na kwa kunia ambazo hazikuanguka. Mwasi mkuu alijivika udanganyifu kiasi kwamba hata viumbe watakatifu hawakuwa wameelewa kanuni zake. Hawakuwa wameona wazi asili ya uasi wake.

Kilikuwa kiumbe chenye nguvu za ajabu na utukufu kilichokuwa kimejiweka kuwa kinyume na Mungu. Kuhusu Lusifa Bwana anasema, "Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri" (Ezekieli 28:12). Lusifa alikuwa kerubi afunikaye. Alikuwa amesimama katika mwanga wa kuwepo kwa Mungu. Alikuwa ndiye kiumbe wa juu sana wa viumbe vyote, na alikuwa na juhudi katika kufunua makusudi ya Mungu kwa ulimwengu. Baada ya kuwa ametenda dhambi, uwezo wake wa kudanganya ulikuwa wa udanganyifu zaidi, na kufunua tabia yake kulikuwa kugumu zaidi, kwa sababu ya cheo cha juu sana alichokuwa nacho pamoja na Baba.

Mungu angeweza kumwangamiza Shetani na wale walioungana naye kirahisi kama mtu anavyoweza kutupa kijiwe chii; lakini hakufanya hivyo. Uasi usingeweza kushindwa kwa kutumia nguvu. Nguvu ya kulazimisha inapatikana tu kama kanuni ya serikali ya Shetani. Kanuni za Bwana sio za mfumo huo. Mamlaka yake yanategemea wema, rehema, na upendo; na kudhihirisha kanuni hizo ndiyo njia inayopaswa kutumika. Serikali ya Mungu ni adilifu, na ukweli na upendo vinapaswa kuwa nguvu inayotawala.

Lilikuwa kusudi la Mungu kuweka vitu katika misingi ya milele ya usalama na katika mabaraza ya mbinguni iliamuliwa kuwa muda lazima utolewe kwa Shetani kukuza kanuni zilizokuwa misingi wa mfumo wa serikali yake. Alikuwa amedai kwamba kanuni zake ni za juu zaidi ya kanuni za Mungu. Muda ulitolewa kwa ajili ya utendaji wa kanuni za Shetani, ili ziweze kuonwa na ulimwengu wa mbinguni.

Shetani aliwaongoza watu dhambini, na mpango wa ukombozi ukaanzishwa. Kwa miaka elfu nne, Kristo alifanya kazi kwa ajili ya kumwinua mwanadamu, na Shetani kwa ajili ya kumharibu na kumdhalilisha. Na mbingu zote lilitazama hayo yote.

Yesu alipokuja duniani, nguvu za Shetani lilielekezwa dhidi yake. Tangu wakati alipotokea kama mtoto katika Bethlehemu, Mnyang'anyi alijaribu kumwangamiza. Kwa kila njia iliyowezekana alitafutaa kumzuia Yesu kujenga tabia kamilifu utotoni, utu uzima usio na hatia, huduma takatifu na kafara isiyo na mawaa. Lakini alishindwa. Hakuweza kumwongoza Yesu kutenda dhambi. Hakuweza kumkatisha tamaa, au kumwondoa kwenye kazi aliyokuja duniani kuifanya. Toka nyikani hadi Kalwari, dhoruba ya ghadhabu ya Shetani ilimpiga, lakini kadiri ilivyokuja bila huruma, ndivyo kwa uthabiti zaidi Mwana wa Mungu alishikilia mkono wa Baba yake, na kuendelea

mbele katika njia yenye alama za damu. Juhudi zote za Shetani kumkandamiza na kumshinda zilidhihirisha katika uru safi tabia yake isiyo na doa.

Mbingu yote na dunia ambazo hazikuasi wamekuwa mashahidi wa vita. Kwa shauku jinsi gani walifuatilia matukio ya mwisho ya pambano. Walimwona Mwokozi akiingia bustani ya Gethsemane, roho yake ikiwa na huzuni ya kitisho cha giza kuu. Walisikia kilio chake cha uchungu "Baba kama ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke" (Mathayo 26:39). Kuwepo kwa Baba kulipoondolewa, walimwona akihuzunika kwa uchungu wa huzuni inayopitaile ya shindano kubwa la mwisho pamoja na mauti. Jasho la damu ilitoka kwenye vinyweleo vyake, na kudondoka kama matone ardhini. Mara tatu ombi la kuokolewa lilisikika kutoka midomo yake. Mbingu hazikuweza kustahimili kuona hali hiyo, na mjumbe wa faraja alitumwa kwa Mwana wa Mungu.

Mbingu zilimwona Mwokozi akisalitiwa mikononi mwa kundi la wauaji, na kwa dhihaka na jeuri akihamishwa toka baraza ya hukumu moja hadi nyingine. Zilisikia vicheko vya dharau vya watesi wake kutokana na kuzaliwa kwa kujishusha. Ilisikia kukana kukana kwa kulaani na kuapa kwa mmoja wa wanafunzi wake wapendwa. Iliona kazi ya wazimu ya Shetani, na uwezo wake juu ya mioyo ya watu. Oh, tukio la kutisha! Mwokozi akikamatwa usiku wa manane Gethsemane, akibururwa huku na huko kutoka jumba la utawala hadi ukumbi wa baraza, akishitakiwa mara mbili mbele ya makuhani, mara mbili mbele ya Sanhedrini, mara mbili mbele ya Pilato, na mara moja mbele ya Herode, akizomewa kupigwa mijeledi, kuhukumiwa, na kuongozwa nje kusulibiwa, akichukua mzigo mzito wa msalaba, kati ya vili vya huzuni vya binti za Yerusalemu na dhihaka za makutano.

Mbingu ziliangalia kwa uchungu na mshangao Kristo akiwa ameangikwa msalabani, damu zikichuruzika kutoka panja la kichwa, na jasho likiwa na damu lilisimama katika paji la uso. Kutoka mikononi na miguuni damu ilichuruzika, tone kwa tone, juu ya mwamba uliochimbwa kwa ajili ya kusimika msalaba. Majeraha yaliyosababishwa na misumari yalipanuka kwa kadri usito wa mwili wake ulivyovuta mikono yake. Kupumua kwake kwa taabu kuliongezeka kasi na nguvu, wakati roho yake ikitweta chini ya mzigo wa dhambi za ulimwengu. Mbingu zote zilistaajabu wakati ombi la Kristo lilipotolewa katikati ya ateso yake ya kutisha, - "Baba uwasamehe; kwa kuwa hawajui watendalo" (Luka 23:34). Lakini bbado walisimama watu pale, walioumbwa kwa mfano wa Mungu, wakiungana kuondolea mbali uhai wa Mwana wake pekee. Picha ya jinsi gani kwa Mbingu kuangalia!

Malaka na nguvu za giza ziliuzunguka msalaba, wakitupa vivuli vya kuzimu vya kutoamini mioyoni mwa watu. Mungu alipoumba viumbe hawa ili kusimama mbele ya kiti chake cha enzi, walikuwa wazuri na wenye utukufu. Kupendeza na utukufu wao uliingana na kiwango cha juu cha cheo chao. Walitajirishwa kwa hekima ya Mungu, na kufunikwa mavazi ya thamani ya mbinguni. Walikuwa ni wahudumu wa Yehove. Lakini ni nani angeweza kutambua katika malaika waovi, maserafi wenye utukufu ambao mwanzo walihudumu katika baraza la mbinguni?

Mawakala wa Shetani waliungana na watu waovu kuwaongoza watu kuamini kuwa Kristo ni mkuu wa wadhambi, na kumfanya yeye kuwa lengo la chuki yao. Wale waliomdhihaki Kristo alipoangikwa msalabani walijazwa na roho wa yule mwasi mkuu wa kwanza. Aliwajaza maneno maovu na ya kuchukiza mno. Alivuvia masuto yao. Lakini kwa yote haya hakupata faida yoyote.

Kama dhambi hata moja ingepatikana ndani ya Kristo, kama kwa jambo fulani angejisalimisha kwa Shetani ili kuepuka mateso ya Kutisha, adui wa Mungu na wanadamu angeshangilia ushindi. Kristo aliinamisha kichwa chake na akafa, lakini laishikilia imani yake kwa dhati na kujisalimisha kwa Mungu. "Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake, kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu mchana na usiku" (Ufunuo 12:10).

Shetani aliona kuwa hila yake iliharibiwa. Utawala wake ulifunuliwa wazi kwa malaika ambao hawakuamguka na kwa ulimwengu wote wa mbinguni. Alijidhihirisha kuwa ni muuaji. Kwa kumwaga damu ya Mwana wa Mungu, alijiondoa kabisa kwenye huruma ya viumbe vya mbinguni. Tangu hapo kazi zake ziliwekewa mipaka. Kwa namna yoyote ambayo angeweza kufanya, asingewangojea malaika walipotoka katika baraza la mbinguni, na kuwashitaki ndugu zake Kristo kuwa wamevikwa mavazi ya giza na kuchafuliwa na dhambi. Kiungo cha mwisho cha huruma kati ya Shetani na ulimwengu wa mbinguni kilikuwa kimevunjika.

Lakini bado Shetani hakuangaizwa. Malaika hata hivyo hawakutambua yote yaliyohusika katika vita kuu. Kanuni zilizokuwa hatarini zilipaswa kufunuliwa zaidi. Na kwa ajili ya wanadamu, maisha ya Shetani yalipaswa kuendelea. Watu hali kadhalika malaika lazima watofautishe kati ya Mfalme wa nuru na mfalme wa giza. Ni lazima achague ni nani atakayemtumikia.

Katika mwanzo wa vita kuu, Shetani alitangaza kuwa sheria za Mungu haziwezi kutiiwa, kwamba haki haikupatana na rehema, na kwamba, kama sheria ingevunjwa, isingewezekana kwa mdhambi kusamehewa. Kila chambi lazima ikutane na hukumu yake, alisisitiza Shetani; na kama Mungu angeondoa adhabu ya dhambi, asingekuwa Mungu wa kweli na hakei. Wanadamu walipovunja sheria ya Mungu, na kutotii mapenzi yake, Shetani alishangilia. Ilithibitika, alidai, kwamba sheria haziwezi kutiiwa; mtu hawezi kusamehewa. Kwa sababu, yeye, baada ya uasi wake, alihamishwa mbinguni, Shetani alidai kwamba wanadamu lazima watengwe milele nje ya upendo wa Mungu. Mungu hawezi kuwa mwenye haki, alidai, na bado aonyeshe rehema kwa mdhambi.

Lakini hata kama mdhambi, mtu aikuwa katika nafasi tofauti na ile ya Shetani. Lusefa mbinguni alitenda dhambi katika nuru ya utukufu wa Mungu. Kwake yeye tofauti na viumbe wengine alifunuliwa zaidi juu ya upendo wa mungu. Akifahamu tabia yake Mungu, akijua wema wake, Shetani alichagua kufuata ubinasi wake mwenyewe, nia huru. Uchaguzi huu ulikuwa wa mwisho. Hakukuwa na zaidi ambalo Mungu angefanya kumwokoa. Lakini mwanadamu alidanganwa; mawazo yake yalitiwa giza kwa hila za Shetani. Kimo na kina cha upendo wa Mungu hakuvifahamu. Kwa kutazama tabia yake anaweza kuvutwa na kumrudia Mungu.

Kwa njia ya Yesu, rehema zake Mungu zilidhihirishwa kwa wanadamu; lakini rehema haiondoi haki. Sheria hudhihirisha sifa za tabia ya Mungu, na siyo yudi wala nukta yake inweza kubadilishwa ili kulingana na mtu katika hali yake ya anguko. Mungu hakubadili sheria yake, bali alijitoa Mwenyewe, katika Kristo, kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. "Mungu alikuwa ndayi ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake" (2 Wakorintho 5:19).

Sheria inahitaji kutenda haki, - maisha matakatifu, tabia kamilifu; na hivi mtu hana ili aweze kuvitoa. Hawezi kukidhi matakwa ya sheria takatifu ya Mungu. Lakink Kristo, akija duniani kama mtu, aliishi maisha matakatifu, na kukuza tabia kamilifu. Hizi

anazitoa kama zawadi bure kwa wote watakaozipokea. Maisha yake yanasimama kwa ajili ya maisha ya watu. Hivyo wanapata ondoleo la dhambi zilizopita, kwa njia ya uvumilivu wa Mungu. Zaidi ya hayo, Kristo huwajaza watu na sifa za tabia ya Mungu. Hujenga tabia ya mwanadamu ili kufanana na tabia ya Mungu, mavazi mazuri ya nguvu za kiroho na uzuri. Hivyo haki halisi ya sheria hutimizwa ndani yake anayemwamini Kristo. Mungu anaweza "kuwa mwenye haki, na mwenye kumhesabia haki yeye amwaminiye Yesu" (Warumi 3:26).

Upendo wa Mungu umedhihirishwa katika haki yake kwa jinsi ile ile kama ilivyo katika rehema zzake. Haki ndio msingi wa kiti chake cha enzi, na tunda la upendo wake. Limekuwa kusudi la shetani kuondoa rehema kutoka katika kweli na haki. Alitafuta kuthibitisha kwamba haki ya sheria ya Mungu ni adui wa amani. Lakini Kristo anaonyesha kwamba katika mpango wa Mungu zinadumu zikiungana pamoja; kimoja hakiwezi kuwepo bila kingine. "Rehema na kweli vimekutana, haki na amani zimebusiana" (Zaburi 85:10).

Kwa maisha yake na kifo chake, Kristo alithibitisha kwamba haki ya Mungu haikuharibu rehema yake, lakini ni ili dhambi iweze kusamehewa, na kwamba sheria ni ya haki na inaweza kutiiwa kwa ukamilifu. Mashitaka ya Shetani yalikanushwa. Mungu alikuwa amempatia mtu ushahidi usio na makosa wa upendo wake.

Udanganyifu mwingine sasa uliwekwa mbele. Shetani alidai kwamba rehema iliondoa haki, kwamba kifo cha Kristo kilifuta sheria ya Baba. Kama ingaliwezakana sheria kubadidlshwa au kufutwa, basi Kristo hakuwa na haja ya kufa. Lakini kuondoa sheria kungemaanisha kuufanya uasi udumu milele, na kuiweka dunia chini ya utawala wa Shetani. Ni kwa sababu sheria haiwezi kubadilika, kwa sababu mtu angeokolewa tu kwa utee wa kanuni zake, kwamba Kristo aliangikwa juu msalabani. Hata hivyo kwa kitendo kile ambacho Krosto aliithibitisha sheria, Shetani huwakilisha kama kuvunga sheria. Katika hili litakuja shindano la mwisho la vita kuu kati ya Kristo na Shetani.

Kwamba sheria iliyotamkwa na Mungu mwenyewe ina makosa, kwamba baadhi ya matakwa yake yamewekwa kando, ni madai ambayo Shetani sasa huyatoa. Ni udanganyifu mkuu wa mwisho atakaoleta juu ya uso wa dunia. Hahitaji kushambulia sheria yote; kama anaweza kuongoza watu kutojali kanuni moja, lengo lake litakuwa limepatikana. Maana "yeyote atakayeishika sheria yote, akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote" (Yakobo 2:10). Kwa kukubali kubunja kanuni moja, wanadamu huwekwa chini ya nguvu za Shetani. Kwa kuweka sheria za wanadamu badala ya sheria za Mungu, Shetani atatafuta kuimiliki dunia. Kazi hii imetabiriwa katika unabii. Kuhusu mamlaka kuu ya uasi ambayo humwakilisha Shetani, imetangazwa, "Naye atanena maneno makuu kinyume chake aiye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake aliye juu, naye ataazimu kubadili majira na sheria: nao watatiwa mikononi mwake" (Danieli 7:25).

Wanadamu kwa hakika wataweka sheria zao dhidi ya sheria za Mungu. Watataka kulazimisha dhamiri za wengine, na katika juhudi zao kulazimisha sheria hizi watawekandamiza wanadamu wenzao.

Vita dhidi ya sheria ya Mungu, vilivyoanzishwa mbinguni, vitaendelea hadi mwisho wa wakati. Kila mtu atajaribiwa. Utii au kutotii ni swali litakalo jibiwa na ulimwengu wote. Wote watatakiwa kuchagua kati ya sheria za Mungu na sheria za wanadamu. Hapa mstari unaotenganisha utashorwa. Kutakuwa na makundi mawili tu. Kila tabia itafikia upeo wa juu; na wote wataonyesha kama wamechagua upande wa utee au ule wa kuasi.

Ndipo mwisho utakapokuja. Mungu ataithibitisha sheria yake na kukomboa watu wake. Shetani na wote ambao wameungana naye katika uasi watakomeshwa. Dhambi na wadhambi wataangamia, shina na tawi (Malaki 4:1) – Shetani aliye shna, na wafuasi wake ni matawe. Maneno haya yatatimizwa kwa mfalme wa uovu, "Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu; …nitakuangamiza, ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. …Utakuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwepo tena milele." Ndipo "asiye haki hatakuwepo, atapaangalia mahali pake wala hatakuwapo;" "nao watakuwa kana kwamba hawakuwa kamwe" (Ezekieli 28:6-19; Zaburi 37:10; Obadia 16).

Hili silo tendo la kutumia nguvu vibaya kwa upande wa Mungu. Wale waliokataa rehema yake wanavuna kile walichopanda. Mungu ni chemichemi ya uzima; na mtu anapochagua kutumikia dhambi, hujitenga na mungu, na hivyo hujitenga mwenyewe mbali na uzima. Yeye "ametengwa kutoka uhai wa Mungu." Kristo anasema "wote wanichukiao hupenda mauti" (Waefeso 4:18; Mithali 8:36). Mungu anawapa uhai kwa muda ili waweze kukuza tabia zao na kudhihirisha kanuni zao. Hili linapotimilizwa, wanapokea matokeo ya uchaguzi wo. Kwa maisha ya uasi, Shetani na wote wanaoungana naye hujiweka wenyewe katika hali ya kutopatana na Mungu kiasi kwamba kuwepo kwake, huwa kwao moto ulao. Utukufu wake yeye aliye upendo utawaharibu.

Mwanzoni mwa vita kuu, malaika hawakuelewa hili. Kama Shetani na malaika zake wangeachwa kuvuna matokeo kamili ya dhambi, wangeangamizwa; lakini isingekuwa dhahiri kwa viumbe vya mbinguni kwamba hayo ndiyo yalikuwa matokeo ya dhambi yasiyoepukika. Mashaka kuhusu wema wa Mungu yangebaki katika akili zao kama mbegu mbaya, ambayo ingezaa matunda ya kufisha ya dhambi na misiba.

Lakini sivyo wakati vita kuu itakapokoma. Ndipo mpango wa ukombozi ukiwa umemalizika, tabia ya Mungu inafunuliwa kwa viumbe vyote vyenye akili, kanuni za sheria yake zinaonekana kuwa kamili na zisizobadilika. Dhambi imeonyesha asili yake, Shetani tabia yake. Ndipo kuangamizwa kwa dhambi kutathibitisha upendo wa Mungu na kusimamisha heshima yake mbele ya ulimwengu wa wale viumbe wanaopendezwa kufanya mapenzi yake, na ambao katika miyo yao imo sheria yake.

Vema, sasa, malaika wangeweza kufurahi walipoutazama msalaba wa Mwokozi; maana ijapokuwa hawakufahamu kila kitu, walijua kuwa kuangamizwa kwa dhambi na Shetani kulikuwa hakika, kwamba ukombozi a wanadamu ulikuwa umehakikishwa, na kwamba ulimwengu wote ulifanywa kuwa salama milele. Kristo mwenyewe alitambua kwa ukamilifu matokeo ya kafara iliyotolewa Kalwari. Kwa yote haya aliangalia mbele wakati akiwa msalabani aliposema "Imekwisha."

Ndani ya Kaburi la Yusufu

Hatimaye Yesu alipumzika. Siku ndifu ya aibu na kuteswa ilifika mwisho. Jinsi mionzi ya mwisho ya machweo ya Jua ilipoikaribisha Sabato, Mwana wa Mungu alilala kimya kwenye kaburi la Yusufu. Kazi yake imemalizika, mikono yake ikiwa imekunjwa kwa amani, alipumzika katika masaa matakatifu ya siku ya Sabato.

Hapo mwanzo Baba na Mwana walipumzika siku ya Sabato baada ya kazi yao ya uumbaji. Wakati "Mbingu na nchi zilipomalizika, pamoja na jeshi lake lote" (Mwanzo 2:1), Muumbaji na viumbe vyote vya mbinguni walifurahia wakitafakari tukio hio la utukufu. "Nyota za asubuhi ziliimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa furaha" (Ayubu 38:7). Sasa Yesu alipumzika kwa kazi ya ukombozi; na ingawa kulikuwa na uchungu miongoni mwa wale waliompenda duniani, mbinguni kulikuwa na furaha. Ahadi ya wakati ujao ilikuwa yenye utukufu kwa viumbe vya mbinguni. Uumbaji uliorejeshwa, watu waliokombolewa, ambao baada ya kushinda dhambi wasingeanguka tena, - haya, matokeo yenye kububujika kutoak kazi ya Kristo iliyotimilika, Mngu na malaika waliyaona. Na tukio hili, siku ambayo Yesu alipumzika vimeunganishwa milili. Kwa maana "Kazi yake ni kailifu" na "lolote atendalo Mungu, litakuwa ni la milele" (Kumbukumbu la Torati 32:4; Mhubiri 3:14). Wakati kutakapokuwa na "Urejeshwaji wa vitu vyote, ambavyo Mungu alisema kwa vinywa vya manabii wote watakatifu tangu kuumbwa dunia" (Matendo 3:21), Sabato ya Uumbaji, siku ambayo Yesu alipumzika kaburini mwa Yusufu, bado itakuwa ni siku ya kupumzika na kufurahi. Mbingu na dunia zitaungana kusifu, na "Sabato hata Sabato" (Isaya 66:23) mataifa ya waliokombolewa watasujudu katika ibada ya furaha ka Mungu na Mwanakondoo.

Katika matukio ya mwisho ya siku ya kusulibiwa, ushahidi mpya ulitolewa wa utimizo wa unabii, na ushahidi mpya ulitolewa kwa Uungu wa Kristo. Giza lilipoondoka msalabani, na kilio cha kufa kwa Mwokozi kilipotamkwa, hapo hapo sauti nyingine ilisikika, ikisema, "Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu" (Mathayo 27:54).

Maneno haya hayakusemwa kwa sauti ya kunongona. Macho yote yaligeuzwa kutazama kule yalikotokea. Ni nani aliyeyasema? Alikuwa ni akida, askari wa Kirumi. Uvumilivu wa Kiungu wa mwokozi, na kifo chake cha ghafla, na sauti ya ushindi katika midomo yake, vilimvutia mtu huyu wa mataifa. Katika mwili uliochubuliwa, na kuharibiwa uliangikwa msalabani, akida alimtambua Mwana wa Mungu. Hakuweza kujizuia kukiri imani yake. Hivyo tena ushahidi ulitolewa kwamba Mkombozi wetu ataona matunda ya taabu ya nafsi yake. Katika siku hiyo ya mauti yake, watu watatu, waliotofautiana sana, walitangaza imani yao, - yeye aliyewaamuru walinzi wa Kirumi, yeye aliyeuchukua msalaba wa Mwokozi, na yule aliyekufa msalabani ubavuni pake.

Jioni ilipokaribia utulivu usio wa kawaida ulikuwa juu ya Kalwari. Makutano walitawanyika, na wengi walirudi Yerusalemu wakiwa wamebadilika sana rohoni tofauti na walivyokuwa asubuhi. Wengi walikusanyika kwenye kusulibiwa kwa ajili tu ya udadisi, na wala siyo kwa chuki dhidi ya Kristo. Bado waliamini mashitaka ya makuhani, na walimwona Kristo kama mhalifu. Chini ya msisimko usio wa kawaida waliungana na kundi la watu waliomkamata katika kumdhihaki. Lakini dunia ilipofunikwa na giza, na wakasimama wakishitakiwa na dhamiri zao, walijiona ni wenye hatia ya kosa kubwa. Hakuna dhihaka au kuzomea kulikosikia kati ya giza lile la

kuogofuy; na giza lilipoondoka, walishika njia kuelekea majumbani mwao kwa kimya cha kicho. Walihakikishwa mioyoni kuwa mashitaka ya makuhani yalikuwa ya uongo, kwamba Yesu hakuwa mwenye kujifanya; na wiki chache baadaye, Petro alipohubiri siku ya Pentekoste, walikuwa miongoni mwa maelfu walioongoka kwa Kristo.

Lakini viongozi wa Kiyahudi hawakubadilika kwa matukio waliyoyashuhudia. Chuki yao kwa Yesu haikupungua. Giza lililoifunika dunia katika saa ya kusulibiwa, halikuwa zito kuliko lile lililoendelea kufunika akili za makuhani na watawala. Katika kuzaliwa kwake nyota ilimtambua Kristo, na iliwaongoza mamajusi hadi horini alipolazwa. Majeshi ya mbinguni yalimfahamu, na kuimba sifaa zake juu ya nyanda za Bethlehemu. Bahari ilitambua sauti yake na kuteii amri yake. Magonjwa na mauti vilitambua mamlaka yake, na viliwaachia huru mateka wao. Jua lilimfahamu, na katika kuona maumivu makali ya kufa kwake, lilificha uso wake wa nuru. Miamba ilimjua na ilitetemeka na kuwa vipande vipande kwa kilio chake. Viumbe visivyo na uhai vilimtambua Kristo, na kushuhudia Uungu wake. Lakini makuhani na watawala wa Israeli hawakumjua Mwana wa Mungu.

Hata hivyo makuhani na watawala bado hawakutulia. Walikuwa wametekeleza kusudi lao la kumwua Kristo; lakini hawakujisikia ushindi waivyotarajia. Hata katika saa ya ushindi wao dhahiri, walisumbuliwa na hofu ya kile ambacho kingetokea halafu. Walikuwa wamesikia kilio, “Imekwisha.” “Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu” (Yohana 19:30; Luka 23:46). Waliona miamba ikipasuka, na kusikia tetemeko kubwa la ardhi, na walikuwa na wasiwasi na wasiotulia.

Waliona kijicho kwa mvuto wa Kristo kwa watu alipokuwa hai; walimwonea wivu hata alipokuwa amekufa. Walimwogopa sana, zaidi sana. Kristo aliyekufa kuliko walivyowahi kumwogopa Kristo aliye hai. Waliogopa kama mawazo ya watu yataelekezwa zaidi kwenye matukio yaliyoambatana na kusulibiwa kwake. Walihofia matokea ya kazi ya siku ile. Kwa namna yoyote wasingeuacha mwili wake juu ya msalaba siku ya Sabato. Sabato sasa ilikaribia, na ingekuwa uvunjaji wa utakatifu wake kama miili ingebakia msalabani. Hivyo, kwa kutumia sababu hiyo isiyo ya kweli, viongozi wa wayahudi walimwomba Pilato ili vifo vya watuhumiwa viharakishwe, na miili yao iondolewe kabla ya jua kuzama.

Pilato naye hakuwa radhi kama wao kwa mwili wa Yesu kubakia msalabani. Baada ya kupata ukubali wake, miguu ya wale wawili (wevi) ilivunjwa ili kuharakisha vifo vyao, lakini Yesu alikutwa amekwisha kufa. Maaskari jeuri walikuwa wamelainika kutokana na kile walichokisikia na kukiona kwa Kristo, na walizuiwa kuvunja miguu yake. Hivyo katika kumtoa Mwanakondoo wa Mungu ilitimizwa sheria ya Pasaka, “Hawatasaza sehemu yake yoyote hata asubuhi, wala kuvunja mfupa wake wowote: sawasawa na sheriaya Pasaka ilivyo ndivyo watakavyoishika” (Hesabu 9:12).

Makuhani na watawala walishangazwa kukuta kwambba Kristo alikuwa amekufa. Kifo kwa njia ya msalaba kilikuwa ni cha kukawia; ilikuwa vigumu kuamua wakati uhai ulipokoma. Lilikuwa jambo lisilowahi kusikika la mtu kufa katika muda wa masaa sita ya kusulibiwa. Makuhani walitaka kuhakikisha kwamba yesu amekufa, na kwa ushauri wao askari mmoja alichoma mkuki ubavuni pa Mwokozi. Kutoka katika jeraha hilo, ilitiririka mikondo miwili dhahiri, mmoja wa damu, na mwingine wa maji. Hili lilionekana kwa wote waliotazama, na yohana huelezea tukio hili kwa usahihi. Anasema “Askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji. Naye aliyeona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli, naye anajua ya kuwa anasema kweli,

ili ninyi mpate kusadidi. Kwa maana hayo yalitukia ili andiko litimie, hapana mfua wake utakaovunjwa. Na tena andiko lingine lanena, "Watamtazama yeye waliyemchoma" (Yohana 19:34-37).

Baada ya ufufuo makuhani na watawala walisambaza habari kwamba Kristo hakufa msalabani, kwamba alizimia tu, na baadaye aliamka. Taarifa nyingine ilithibitisha kuwa siyo mwili halisi wa nyama na mifupa, bali mfano wa mwili, ndio uliowekwa kaburini. Kitendo cha maaskari wa Kirumi kinakanusha uongo huo. Hawakuvunja miguu yake, maana alikuwa amekwisha kufa. Ili kuwaridhisha makuhani, walichoma ubavu wake. Kama uhai usingekuwa umetoweka, donda lile lingesababisha kifo palepale.

Lakini haikuwa nguvu ya mkuki, hayakuwa maumivu ya msalaba, yaliyosababisha kifo cha Yesu. Kile kilio kilicho tamkwa "Kwa sauti kuu" (Mathayo 27:50; Luka 23:46), wakati wa kufa, mikondo ya damu na maji iliyotiririka kutoka ubavuni kwake vilitangaza kwamba alikufa kutokana na moyo uliovunjika. Moyo wake ulivunjwa na maumivu makali ya akili. Dhambi za ulimwengu ndizo zilizomwuua.

Pamoja na kifo cha Kristo matumaini ya wanafunzi yalitoweka. Waliangalia kope za macho yake zilizofumba na kichwa kinachoanguka, nywele zilizolowa kwa damu, miguu na mikono iliyotobolewa, na uchungu wao haukuelezeka. Hadi mwisho hawakuamini kwamba atakufa; ilikuwa vigumu kwao kuamini kwamba alikuwa amekufa. Wakiwa wamevunjika moyo kwa huzuni, hawakukumbuka maneno yake yaliyokuwa yanaeleza tukio hilo. Hakuna lolote alilolisema, ambalo sasa liliwafariji. Waliuona tu msalaba na mtuhumiwa aliyekuwa akitokwa damu. Siku za usoni zilionekana kuwa giza kwa kukata tamaa. Imani yao kwa Yesu iliangamia; lakini hawakuwahi kumpenda Bwana wao kama sasa. Kamwe kabla hawakuwahi kuona uthamani wake, na hitaji lao la kuwepo kwake kama sasa.

Hata katika mauti, mwili wa Kristo ulikuwa wa thamani kwa wanafunzi wake. Walitamani kumpatia mazishi ya heshima, lakini hawakujua namna ya kulitekeleza hili. Fitina dhidi ya Serikali ya Kirumi ulikuwa ndio uhalifu ambao kwao Yesu alihukumiwa, na watu waliouawa kwa kosa hili walipelekwa kwenye eneo la mazishi lililoandaliwa maalum kwa wahalifu wa jinsi hiyo. Mwanafunzi Yohana pamoja na wanawake kutoka Galilaya walibaki pale msalabani. Hawakuweza kuacha mwili wa Bwana wao kuchukuliwa na Maaskari wasio na huruma, na kuzikwa kwenye kaburi lisilo na heshima. Hata hivyo hawangeweza kulizuia hilo. Wasingeweza kupata upendeleo wowote kutoka kwa viongozi wa Kiyahudi, na hawakuwa na ushawishi kwa Pilato.

Katika saa hii ya dharura, Yusufu wa Arimathayo na Nikodemo walikuja kuwasaidia wanafunzi. Watu hawa wote walikuwa wajumbe wa baraza la Sanhedrini, na walifahamiana na Pilato. Wote walikuwa watu wenye utajiri na mvuto. Walikuwa wamekusudia kwamba mwili wa Yesu upewe mazishi ya heshima.

Yusufu alimwendea Pilato kwa ujasiri, na kumwomba mwili wa Yesu. Kwa mara ya kwanza, Pilato anafahamu kuwa hakika Yesu alikuwa amekufa. Taarifa zinazopingana zilikuwa zimemfikia kuhusu matukio yaliyoambatana na kusulibiwa, lakini habari za kifo cha Krissto zilifichwa kwake kwa makusudi. Pilato alikuwa ameonywa na makuhani na watawala dhidi ya udanganifu wa wanafunzi wa Kristo kuhusiana na mwili wake. Aliposikia ombi la Yusufu, alimwita akida aliyesimamia mambo pale msalabani, na akapata uhakika wa kifo cha Yesu. Pia alipata taarifa ya matukio ya Kalwari, akithibitisha ushahidi wa Yusufu.

Ombi la Yusufu lilikubaliwa. Wakati Yohana akifadhaika kuhusu mazishi ya Bwana wake, Yusufu alirudi na hati ya Pilato kuhusu mwili wa Kristo; na Nikodemo alifika akileta mchanganyiko wa manemane na uudi, yapata ratili mia, ili kumpaka asioze. Yule aliyeheshimika sana katika Yerusalemu yote asingeweza kupewa heshima zaidi katika mauti. Wanafunzi walistaajabu kuona hawa watawala tajiri wakionyesha moyo kama wao wenyewe katika mazishi ya Bwana wao.

Si Yusufu wala Nikodemo aliyekuwa amemkiri wazi Mwokozi aipokuwa hai. Walifahamu kwamba hatua kama hiyo ingewatenga kutoka baraza la Sanhedrini, na walitumaini kumtetea kutokana na mvuto wao katika vikao vyao. Kwa muda walionekana kufaulu, lakini makuhani werevu, walipoona upendeleo wao kwa Kristo, walipindua mipango yao. Wakati hawapo Yesu alihukumiwa na kutolewa akasulibiwe. Sasa kwamba alikuwa amekufa, hawakuendelea kuficha kushikamana kwao naye. Wakati wanafunzi wakiogopa kujitokeza wazi kama wafuasi wake, Yusufu na Nikodemo walijitokeza kwa ushujaa kuwasaidia. Msaada wa hawa watu matajiri na wenye kuheshimiwa ulihitajika sana wakati huu. Wangeweza kufanya kwa ajili ya Bwana wao aliyekufa kile ambacho haikuwezekana kwa wanafunzi makini kukifanya; na utajiri na mvuto wao uliwakinga kwa kiasi kikubwa, dhidi ya uovu wa makuhani na watawala.

Kwa taratibu na kicho waliuondoa kwa mikono yao wenyewe mwili wa Yesu toka msalabani. Machozi yao ya huzuni yalidondoka kwa haraka walipoangalia mwili wake uliochubuliwa na kuraruliwa. Yusufu alikuwa na kaburi jipya, lililochongwa mwambani. Hili alilitunza kwa ajili yake mwenyewe,, lakini lilikuwa karibu na Kalwari, na sasa aliliandaa kwa ajili ya Yesu. Mwili, pamoja na manukato yaliyoletwa na Nikodemo, kwa uangalifu vilizongwa kwanye shuka ya kitani, na mkombozi alichukuliwa kwenda kaburini. Pale wanafunzi watatu waliinyosha miguu iliyopinda, na kukunja mikono iliyo chubuliwa katika kifua kisicho na mapigo ya moyo. Wanawake wagalilaya walikuja kuangalia kama yote yaliyopaswa kufanyika yalifanyika kwa ajili ya mwili uliokufa wa Mwalimu wao mpendwa. Halafu waliona jiwe zito likivingirishwa kwenye mlango wa baburi, na mwokozi aliachwa amepumzika. Wanawake walikuwa wa mwisho msalabani, na wa mwisho kwenye kaburi la Kristo. Wakati vivuli vya jioni vilipokuwa vinajikusanya, Mariamu Magdalena na wale Mariamu wengine walikawia mahali Bwana wao alipopumzika, wakitoa machozi ya huzuni kwa ajili ya yule waliyempenda. “Wakarudi, …Na siku ya Sabato walistarehe kama ilivyoamriwa” (Luka 23:56).

Hiyo ilikuwa Sabato isiyoweza kusahaulika kwa wanafunzi wenye huzuni, na pia kwa makuhani, watawale, waandishi na watu. Wakati wa jua kuzama jioni ya siku ya maandalio tarumbeta zililia, zikiashiria kwamba Sabato ilikuwa imeanza. Pasaka iliadhimishwa kama ilivyofanyika karne zote, wakati yeye iliyeelekeza kwake alikuwa ameuawa na mikono miovu, na alilala katika kaburi la Yusufu. Siku ya Sabato ukumbi wa hekalu ulifurika waabuduo. Kuhani mkuu kutoka Golgotha alikuwepo pale, akiwa amevalia kifahari mavazi ya kikuhani. Makuhani wenye vilemba vyeupe, wakiwa na kazi tele, walitekeleza wajibu wao. Lakini baadhi ya waliokuwepo hawakuwa na amani wakati damu ya mafahali na mbuzi ilipotolewa kwa ajili ya dhambi. Hawakuwa na habari kwamba mfano ulikuwa umekutana na kitu halisi, kwamba kafara isiyo kifani ilikuwa imetolewa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Hawakujua kwamba hakukuwa na faida tena katika kutekeleza taratibu hizo za kidini. Lakini kamwe hawakuwahi hushuhudia ibada hii kwa hisia zinazopingana kama ilivyokuwa siku hiyo. Tarumbeta na vyombo vya muziki na sauti za waimbaji zilikuwa kubwa na dhahiri kama kawaida.

Lakini hisia ngeni ilienea kote. Mmoja baada ya mwingine aliuliza kuhusu tukio geni lililotokea. Hata sasa mahali Patakatifu mno palikuwa pamelindwa dhidi ya uvamizi. Lakini sasa palikuwa wazi kwa macho yote. Pazia zito la zulia, lililotengenezwa kwa kitani safi, na kupambwa kwa dhahabu, rangi nyekundu, na zambarau, lilíraruliwa toka juu hadi chini. Mahali ambapo Yehove alikutana na kuhani mkuu, ili kudhihirisha utukufu wake, mahali ambapo palikuwa chumba wakfu cha Mungu cha kusikizisha watu, palikuwa wazi kwa kila jicho, - mahali pasipo tambuliwa tena na Mungu. Kwa huzuni ya onyo la mambo yatakayokuja makuhani walihudumu mbele ya madhabahu. Kufunuliwa kwa siri takatifu ya mahali Patakatifu sana kuliwajaza hofu ya msiba uliokuwa unakuja.

Akili za watu wengi zilishughulika na mawazo yaliyoanzishwa na matukio ya Kalwari. Tangu kusulibiwa hadi ufufuo, macho mengi yasiyo na usingizi daima yalichunguza unabii, wengine ili kujifunza maana kamili ya sikukuu waliyokuwa wakiiadhimisha wakati huo, wengine kupata ushahidi kwamba Yesu hakuwa kama alivyokuwa anadai; na wengine kwa mioyo ya huzuni walitafuta uthibitisho kwamba Yeye alikuwa ndiye masihi wa kweli. Ijapokuwa walitafiti kwa malengo tofauti, wote walithibitishwa kwa ukweli ule ule, - kwamba unabii ulitimizwa katika matukio ya siku chache zilizopita, na kwamba yeye aliyesulibiwa alikuwa mkombozi wa ulimwengu. Wengi ambao kwa wakati huo waliungana katika huduma kamwe hawakushiriki tena katika desturi ya Pasaka. Wengi hata Makuhani walihakikishwa kuhusu tabia halisi ya Yesu. Kuchunguza kwao unabii hakukuwa bure, na baada ya kufufuka kwake walimkiri kuwa Mwana wa Mungu.

Nikodemo, alipoona yesu ameinuliwa juu msalabani, alikumbuka maneno yake aliyosema usiku katika mlima wa Mizeituni: “Kama Musa alivyomwinua nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika Yeye” (Yohana 3:14, 15). Katika Sabato hiyo, Kristo alipolala kaburini, Nikodemo alikuwa na muda wa kutafakari. Nuru safi sasa iliangaza mawazo yake, na maneno ambayo Yesu alimwambia hayakuwa mafumbo. Alijisikia kwamba alikuwa amepoteza sana kwa kutojiungamanisha pamoja na Mwokozi wakati wa uhai wake. Sasa alikumbuka matukio ya Kalwari. Ombi la Kristo kwa ajili ya wauaji wake na jibu lake kwa ombi la mwivi aliyekuwa kifoni, vilizungumza katika moyo wa huyu mshauri msomi. Alimwangalia tena Mwokozi katika mateso yake; tena akasikia kilio kile cha mwisho, “Imekwisha,” kikisemwa kama maneno ya mshindi wa vita. Tena aliangalia dunia ikiwayawaya, mbingu zilizotewa giza, pazia lililopasuliwa, miamba iliyotetemeka, na imani yake ilithibitika milele. Tukio lili lie lililovunja matumaini ya wanafunzi liliwathibitishia Yusufu na Nikodemo Uungu wa Yesu. Woga wao ulishindwa kwa ujasiri wa imani thabiti na isiyo na mashaka.

Kamwe Kristo hakuwahi kuvuta mawazo ya watu wengi kama wakati huu alipokuwa amelazwa kaburii. Kulingana na desturi yao, watu waliwaleta wagonjwa na wale walioteswa kwenye ukumbi wa hekalu, wakiuliza, Ni nani anayeweza kutueleza habari za Yesu wa Nazareti? Wengi walikuja kutoka mbali ili kumtafuta Yeye aliyewaponya wagonjwa na kufufua wafu. Kutoka kila upande kilio kilisikika, Tunamtaka Kristo mponyaji! Katika wakati huu wale waliodhaniwa uonyesha dalili za ukoma walikuwa wakikaguliwa na makuhani. Wengi walilazimishwa kusikia waume zao, wake au watoto wao wakitangazwa kuwa wenye ukoma, na wakilazimika kuondoka kutoka hifadhi ya nyumba zao na utunzaji wa rafiki zao, na kutoa kilio cha tahadhari kwa mgeni, “Mimi ni najisi, najisi!” Mikono ya kirafiki ya Yesu wa Nazareti, ambayo kamwe haikukataa

kugusa kwa kuponya mkoma mwenye kuchukiza sana, ilikuwa imekunjwa kifuani pake. Midomo iliyokuwa imejibu kusihi kwake na maneno ya faraja, "Nataka, takasika" (Mathayo 8:3), sasa ilikuwa kimya. Wengi waliomba kwa wakuu wa makuhani na watawala huruma na msaada, lakini bila mafanikio. Kwa mwonekano walidhamiria kuwa na Kristo aliye hai kati yao tena. Kwa bidii iliyoendelea walizidi kumuomba. Hawakuweza kugeuzwa kuacha nia yao. Lakini walifukuzwa kutoka hekaluni, na maaskari wakawekwa milangoni ili kuuzuia umati uliokuja na wagonjwa wao na walio kifoni, wakidai kuingia.

Walioteseka waliokuwa wamekuja ili kuponywa na mwokozi walizama katika uchungu wao. Mitaa ilijaa vilio vya maombolezo. Wagonjwa walikuwa wanakufa kwa kukosa mguso wa uponyaji wa Yesu. Matabibu walitakwa ushauri lakini haikufaa kitu; hakukuwa na ujuzi kama wa Yule aliyelala katika kaburi la Yusufu.

Vilio vya maombolezo vya wanaoteseka vilirejesha katika mawazo ya watu wengi uthibitisho kwamba nuru kuu ilikuwa imetoweka duniani. Bila Kristo, dunia ilikuwa ni weusi na giza. Wengi ambao sauti zao zilipaza kilio "Msulibishe, msulibishe," sasa walitambua msiba uliowapata, na wangeweza kupaza vilio, Tupatieni Yesu! Kama angekuwa bado hai.

Watu walipofahamu kwamba Yesu ameuawa na makuhani, walihoji kuhusu kifo chake. Taarifa za kesi yake zilifanwa siri kadri ilivywezekana; lakini wakati akiwa kaburini, jina lake lilikuwa katika midomo maelfu, na taarifa za kesi yake iliyofanywa kwa dhihaka, na kukosa utu kwa makuhani na watawala, ziliendea kila mahali. Watu wenye akili nyingi waliwataka makuhani na watawala kueleza unabii wa agano la kale kumhusu Masihi, na wakati wakijarubu kuunda uongo ili kujibu walikuwa kama watu wenye wazimu. Unabii ulioelekeza kwenye mateso na kifo cha Kristo hawakuweza kueleza, na wengi waliokuwa wakihoji walihakikishwa kwamba maandiko yalikuwa yametimia.

Kisasi ambacho makuhani walifikiri kitakuwa ni kitamu sana tayari kilikuwa uchungu kwao. Walijua kwamba walikuwa wanapata lawama nyingi za watu; walijua kwamba watu wale waliowachochea dhidi ya Yesu sasa waliogofywa na matendo yao ya aibu. Hawa makuhani walijaribu kuamini kwamba Yesu ni Mdanganifu; lakini ilikuwa bure. Baadhi yao walikuwa wamesimama kando ya kaburi la Lazaro, na walimwona yule aliyekuwa amekufa akifufuliwa. Walitetemeka kwa hofu kuwa Kristo mwenyewe angefufuka toka kwa wafu, na kuonekana tena mbele yao. Walikuwa wamemsikia akisema kwamba alikuwa na uwezo wa kuutoa uhai wake na wa kuutwaa tena. Walikumbuka kwamba alikuwa amesema "Livunjeni hili hekalu, na katika siku tatu nitalisimamisha" (Yohana 2:19). Yuda alikuwa amewaambia maneno aliyoyasema kwa wanafunzi katika safari ya mwisho kuelekea Yerusalemu; "Angalieni tunapanda kwenda Yerusalemu; na Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa Makuhani na waandishi; nao watamhukumu afe; kisha watampeleka kwa mataifa wapate kumdhihaki, na kumpiga mijeledi, na kumsulibisha; na siku ya tatu atafufuka" (Mathayo 20:18, 19). Waliposikia maneno haya, walidhihaki na kucheka. Lakini sasa walikumbuka kwamba utabiri wa Kristo hadi sasa ulikuwa umetimizwa. Alisema kwamba atafufuka siku ya tatu, na ni nani angeweza kukanusha kwamba hili halitatimia? Walitamani kuondoa mawazo haya, lakini hawakuweza. Kama baba yao, Ibilisi, waliamini na kutetemeka.

Sasa wazimu wa msisimko ulikuwa umekwisha. Sura ya Kristo iliingia mawazoni mwao. Walimtazama akisimama kwa utulivu na bila kunung'unika mbele ya maadui

zake. Akiteseka bila kunung'unikia masuto na unyanyasaji wao. Matukio yote ya kesi yake na kusulibiwa yaliwarudia kwa nguvu kubwa ya ushawishi kwamba alikuwa Mwana wa Mungu. Walijihisi kwamba saa yoyote atasimama mbele yao, mshitakiwa kuwa mshitaki, mhukumiwa kuwa mhukumu, aliyeuawa kudai hai katika mauti ya wale waliomwua.

Walipumzika kidogo sana siku ya Sabato. Ijapokuwa wasingevuka mlango wa mataifa kwa kuogopa kunajisika, lakini walifanya kikao kuhusu mwili wa Kristo. Mauti na kaburi lazima vimshikilie yeye waliyemsulibisha. "Wakuu wa makuhani na Mafarisayo walikuja pamoja kwa Pilato, wakisema, Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, baada ya siku tatu atafufuka. Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba, na kuwaambia watu, amefufuka katika wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza. Pilato akawaambia, mna akari; nendeni mkalilinde salama kaburi mjuavyo" (Mathayo 27:62-65).

Makuhani walitoa maelekezo kwa usalama wa kaburi. Jiwe kubwa lilikuwa limewekwa mbele ya mlango. Na mwisho hadi mwisho wa jiwe hilo waliweka kamba, zilizoshikiwa mwambani na kuziweka muhuri kwa muhuri wa Kirumi. Jiwe lisingeweza kuondolewa bila ya kuvunja muhuri. Kundi la askari walinzi mia moja liliwekwa kuzunguka kaburi ili kuzuia lisije likaharibiwa. Makuhani walifanya yote waliyoweza kuuzuia mwili wa Kristo kubakia mahali ulipolazwa. Aliwekewa muhuri kuhifadhiwa kaburini kana kwamba angebakia pale kwa wakati wote.

Hivyo watu dhaifu walishauriana na kupanga. Ni kidogo sana walifahamu kutofaa kwa juhudi zo. Lakini kwa tendo lao Mungu alitukuzwa. Juhudi zilizofanywa kuzuia kufufuka kwa Kristo ni hoja zenye kuthibitisha uhakika wake. Kwa idadi kubwa ya maaskari waliowekwa kaburini, ungekuwa mkubwa ushahidi kwamba amefufuka. Miaka mamia kabla ya mauti ya Kristo, Roho Mtakatifu alitangaza kupitia mwandishi wa Zaburi, "Mbona mataifa wanafanya ghasia, na makabila wanatafakari ubatili? Wafalme wa dunia wanajipanga, na wakuu wanafanya shauri pamoja, juu ya Bwana, na juu ya Masihi wake, …Yeye aketiye mbinguni anacheka, Bwana anawafanyia dhihaka" (Zaburi 2:1-4). Walinzi wa Kirumi na silaha za Kirumi hazikuwa na nguvu kumfungia Mfalme wa uzima kaburini. Saa ya kufunguliwa kwake ilikuwa inakaribia.

“Bwana Amefufuka”

Usiku wa siku ya kwanza ya juma ulitoweka polepole. Saa ya giza sana , kabla tu ya mapambazuko ilifika. Kristo bado alikuwa mfungwa katika kaburi lake jembamba. Jiwe kubwa lilikuwa mahali pake; muhuri wa Kirumi haukuwa umefunguliwa; walinzi wa Kirumi walitunza zamu zao. Na kulikuwa na waangalizi wasioonekana. Majeshi ya malaika waovu walikusanyika kuzunguka pale. Kama ingewezekana, mfalme wa giza na jeshi lake la uasi wangelinda milele likiwa limefungwa kaburi lililomchukua Mwana wa Mungu. Lakini jeshi la mbinguni lililizunguka kaburi. Malaika wenye nguvu sana walililinda kaburi, na wakingojea kumlaki Mfalme wa Uzima.

“Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi, kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni.” Akiwa amevikwa utukufu wa Mungu, malaika huyu aliondoka katika baraza ya mbinguni. Miali ing’aayo ya utukufu wa Mungu ilimtangulia, na kuangaza njia yake. “Sura yake ilikuwa kama umeme, na mavaziyake meupe kama theluji. Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka wakawa kama wafu.”

Sasa, makuhani na watawala, uko wapi uwezo wa walinzi wenu? Maaskari shujaa ambao hawajawahi kuogopa nguvu za kibinadamu sasa ni kama mateka waliochukuliwa bila upanga au mkuki. Uso wanaouona sio uso wa askari wa kibinadamu; ni uso wa mwenye uwezo kabisa wa jeshi la Bwana. Mjumbe huyu ndiye anayeshikilia nafasi ambayo Shetani alianguka. Ndiye ambaye katika vilima vya Bethlehemu alitangaza kuzaliwa kwake. Dunia inatetemeka anapokaribia, majeshi ya giza yanakimbia, na anapovingirisha lile jiwe, mbingu zinaonekana kushuka chini duniani. Maaskari wanamwona akiondoa jiwe kama ni kijiwe kidogo tu, na wanamsikia akilia, “Mwana wa Mungu, toka nje; Baba yako anakuita.” Wanamwona Yesu akitoka kaburini, na wanamsikia akitangaza juu ya kaburi lililovunjwa, “Mimi ni ufufuo na uzima.” Anapotoka kwa enzi na utukufu, jeshi la malaika linainama chini kumwabudu Mkombozi, na kumkaribisha kwa nyimbo za sifa.

Tetemeko la nchi liliashiria saa Kristo aliyokufa, na tetemeko jingine lilishuhudia wakati alipotwaa uhai tena kwa ushindi. Yeye aliyeshinda kifo na kaburi alitoka kaburini kwa kishindo cha mshindi, kati ya kuyumbayumba kwa dunia, kuangaza kwa umeme, na kwa ngurumo za radhi. Atakapokuja tena duniani, atatetemesha “siyo dunia peke yake, bali na mbingu pia.” “Dunia inalewalewa kama mlevi, nayo itaondolewa kama kibanda.” “Mbingu zitakunjwa pamoja kama ukurasa;” “Na viumbe vya asili vitayeyuka, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.” Lakini “Bwana atakuwa tumaini la watu wake, na ngome ya wana wa Israeli” (Waebrania 12:26; Isaya 24:20; 34:4; 2 Petro 3:10; Yoeli 3:16)

Katika kufa kwa Yesu maaskari waliona nchi ikifunikwa giza mchana; lakini katika ufufuo waliona mng’ao wa malaika ukiangaza usiku, na kusikia wakazi wa mbinguni wakiimba kwa furaha na shangwa: Umemshinda Shetani na nguvu za giza; umemeza mauti kwa kushinda.

Kristo alitoka kaburini ametukuzwa, na walinzi wa Kirumi walimwona. Macho yao yalivutwa usoni pake Yeye ambaye muda mfupi uliopita walimfanyia mzaha na dhihaka. Katika huyu aliyetukuzwa walimwona mfungwa waliyekuwa wamemwona katika ukumbi wa hukumu, yule ambaye kwa ajili yake walisokota taje ya miiba. Huyu ndiye

yule aliyesimama bila ubishi mbele za Pilato na Herode, mwili wake ukiwa umechubuliwa kwa kupigwa mijeledi kikatili. Huyu ndiye aliyesulibiwa msalabani, ambaye kwake makuhani na watawala, kwa kujikanai walitikisa vichwa waisema "Aliokoa wengine; mwenyewe hawezi kujiokoa" (Mathayo 27:42). Huyu ndiye aliyewekwa kulala katika kaburi jipya la Yusufu. Tangazo la mbinguni lilimfungulia mateka. Milima juu ya milima juu ya kaburi lake isingeweza kuzuia kufufuka kwake.

Kwa kuwaona malaika na Mwokozi mwenye utukufu walinzi wa Kirumi walizimia na kuwa kama wafu. Wakati msafara huu wa kimbingu alipofichwa machoni pao, waliamka na kusimama, na kwa haraka kadiri miguu yao iliyotetemeka ilivyoweza kuwachukua, walikimbia hadi kwenye lango la bustani. Wakiyumbayumba kama walevi, waliharakisha hadi mjini, wakiwaeleza waliokutana nao habari zile za ajabu. Walikuwa wanaelekea kwa Pilato, lakini taarifa zao zilikuwa zimefikishwa kwa viongozi wa kiyahudi, na wakuu wa makuhani na watawala wakaagiza waletwa mbele yao kwanza. Ni mwonekano wa ajabu maaskari waliouonyesha. Wakitetemeka kwa hofu, nyuso zao zimepauka, walitoa ushuhuda wao wa kufufuka kwa Kristo. Maaskari walieleza kila kitu, jinsi walivyoona; hawakuwa na muda wa kufikiri au kusema chochote isipokuwa ukweli. Kwa uchungu walitamka, Ni Mwana wa Mungu ndiye aliyesulibiwa; tumemsikia malaika akimtangazza kama Mkuu wa Mbinguni, Mfalme wa utukufu.

Nyuso za makuhani zikawa kama za watu waliokufa. Kayafa alijaribu kuzungumza. Midomo yake ilicheza, lakini haikutoa sauti yoyote. Maaskari walikuwa karibu kuondoka ukumbini, wakati sauti ilipowazuia. Hatimaye Kayafa aliweza kutoa sauti. Ngojeni, ngojeni, alisema. Msimwambie mtu yeyote mambo mliyoyaona.

Taarifa ya uongo ilitoewa kwa maaskari. "Semeni ninyi" makuhani walisema, "Wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba tulipokuwa tumelala." Hapa makuhani walijidanganya wenyewe. Ni kwa jinsi gani maaskari wangesema kwamba wanafunzi walimwiba wakati wamelala? Kama walilala, walijuaje? Na kama wanafunzi wamethibitishwa kuwa na hatia ya kuuiba mwili wa Yesu, makuhani wasingekuwa wa kwanza kuwahukumu? Au kama maaskari wa zamu walilala kaburini, makuhani wasingekuwa wa kwanza kuwashitaki kwa Pilato?

Maaskari walishitushwa na wazo la kujitetea mashitaka wao wenyewe ya kulala kazini kwao. Hili ni kosa lililoadhibiwa kwa kifo. Je, watoe usuhuda wa uongo wakidanganya watu, na kuhatarisha maisha yao? Je, hawakutunza ulinzi wao wa kuchosha kwa bidii isiyosinzia? Wangewezaje kukabili kesi, hata kama ni kwa ajili ya pesa, kama walisema uongo wao wenyewe?

Ili kunyamazisha ushuhuda waliouogopa, makuhani waliahidi kutafuta usalama wa walinzi, kwa kusema kwamba Pilato hatahitaji taarifa kama hizo zisambazwa zaidi ya walivyokuwa wamefanya. Maaskari wakauza uaminifu wao kwa Wayahudi kwa fedha. Walikuja mbele ya makuhani wakilemewa na mzigo wa ujumbe wa kutisha wa ukweli; lakini waliondoka na mzigo wa fedha, na katika ndimi zao, taarifa ya uongo iliyotengenezwa kwa ajili yao na makuhani.

Wakati ule ule taarifa za kufufuka wa Kristo zilikuwa zimemfikia Pilato. Ijapokuwa Pilato alikuwa anawajibika kwa kumtoa Kristo ile afe, hakuonekana kujali. Wakati alimhukumu Mwokozi bila kupenda, na kwa hisia ya huruma, hakuwa amepata majuto ya kweli hata sasa. Kwa hovu sasa alijifungia ndani ya nyumba yake, akikusudia kutoonana na mtu yeyote. Lakini makuhani walikwenda hadi mbele yake, na kueleza hadithi waliyoibuni, na kumhimiza kutojali uzembe wa maaskari wa zamu. Kabla ya kulikubali

hili yeye binafsi aliwahoji walinzi faraghani. Wao, wakihofia usalama wao, hawakutaka kuficha chochote, na Pilato alipata kutoka kwao maelezo ya mambo yote yaliyotendeka. Hakuendelea kulipeleleza zaidi, lakini tangu hapo hakukuwa na amani kwake.

Yesu alipowekwa kaburini, Shetani alishangilia. Alithubutu kutumaini kwamba Mwokozi hatatwaa uhai wake tena. Alidai mwili wa Bwana, na kuweka walinzi wake kaburini, akitaka kumshikilia Kristo kama mfungwa. Alichukia sana malaika zake walipokimbia wakati Mjumbe wa mbinguni alipokaribia. Alipomwona Kristo akitoka kaburini kwa ushindi, alijua kwamba ufalme wake utakoma, na kwamba lazima mwisho afe.

Makuhani kwa kumwua Kristo, walijifanya kuwa vyombo vya Shetani. Sasa walikuwa chini ya nguvu zake kabisa. Walikuwa wamenaswa kwanye mtego ambao hawakuona njia ya kutokea isipokuwa kuendeleza vita vyao dhidi ya Kristo. Waliposikia taarifa ya kufufuka kwake, walihofia hasira za watu. Walihisi kwamba maisha yao yamo hatarini. Tumaini pekee kwao lilikuwa kuthibitisha kuwa Kristo ni mlaghai kwa kukana kwamba amefufuka. Waliwahonga maaskari, na kufanikiwa kumnyamazisha Pilato. Walieneza taarifa yao ya uongo mbali na karibu. Lakini kulikuwa na mashahidi ambao hawakuweza kuwanyamazisha. Watu wengi walikuwa wamesikia ushuhuda wa maaskari kuhusu kufufuka kwa Kristo. Na baadhi ya wafu waliokuwa wamefufuka na Kristo waliwatokea wengi, na kutangaza kwamba amefufuka. Taarifa zilipelekwa kwa makuhani za watu waliowaona hawa waliofufuka, na kusikia ushuhuda wao. Makuhani na watawala walikuwa kwenye hofu daima, isijekuwa katika kutembea barabarani, au katika faragha ya nyumba zao, wakakutana na Kristo uso kwa uso. Walihisi kwamba hakukuwa na usalama kwao. Makomeo na vyuma ulikuwa ulinzi hafifu dhidi ya Mwana wa Mungu. Mchana na usiku tukio lile la kutisha kwenye ukumbi wa hukumu, walipopiga kelele, "Damu yake iwe juu yetu, na watoto wetu" lilikuwa mbele yao (Mathayo 27:25). Kamwe kumbukumbu ya tukio lile haitafutika akilini mwao. Kamwe usingizi wa amani hautakuja kwenye mito yao.

Wakati sauti ya malaika mwenye nguvu iliposikika Kwenye kaburi la Kristo, ikisema, Baba yako anakuita, Mwokozi alitoka kaburini kwa uhai uliokuwemo ndani yake. Sasa ulithibitishwa ukwele wa maneno yake, "Nautoa uhai wangu, ili niutwae tena…Nami ninao uwezo wa kuutoa, ninao na uwezo wa kuutwaa tena." Sasa ulitimizwa unabii aliokuwa amewaambia makuhani na watawala "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha" (Yohana 10:17, 18; 2:19).

Juu ya kaburi lililovunjwa la Yusufu, Kristo alitangaza katika ushindi, "Mimi ndimi ufufuo na uzima." Maneno haya yangeweza kusemwa tu na Uungu. Vitu vyote vilivyoumbwa vinaishi kwa mapenzi na nguvu za Mungu. Ni wapokeaji tegemezi wa uhai wa Mungu. Tangu Serafi wa juu kabisa hadi kiumbe hai cha chini, wote hujazwa tena toka chanzo cha uhai. Ni yule tu aliye mmoja na Mungu anaweza kusema, ninao uweza wa kuutoa uhai wangu, na nina uweza wa kuutwaa tena. Katika Uungu wake, Kristo alikuwa na uwezo wa kuvunja vifungo vya mauti.

Kristo alifufuka kutoka wafu kama limbuko lao waliolala. Alikuwa ndiye halisi wa kutikisa miganda, na kufufuka kwake kulitokea siku ile ambayo miganda ya kutikiswa ingetolewa mbele za Bwana. Kwa zaidi ya miaka elfu moja sikukuu hii kielelezo ilikuwa imefanyika. Kutoka katika mashamba ya mavuno, masuke ya kwanza ya nafaka zilizokomaa yalikusanywa, na watu walipokwenda yerusalemu kwanye sikukuu ya Pasaka, miganda ya mavuno ya kwanza ilitikiswa kama sadaka ya shukrani kwa Mungu.

Ni mpaka sadaka hii ilipotolewa ndipo mundu ulipowekwa kwenye nafaka, na kukusanywa katika matita. Miganda iliyotolewa kwa Mungu iliwakilisha mavuno, hivyo Kristo kama mavuno ya kwanza (limbuko) aliwakilishaMavuno makubwa ya kiroho yatakayokusanywa kwa ufalme wa Mungu. Ufufuo wake ni mfano na kiap cha ufufuo wa watakatifu wote waliokufa. "Maana kama twaamini ya kwamba Yesu alikufa na akafufuka, vivyo hivyo wale waliolala katika Yesu Mungu atawaleta pamoja naye" (1 Wathesalonike 4:14).

Kristo alivyofukuka, aliwatoa makaburini makutano ya mateka. Tetemeko la nchi katika kufa kwake lilifunua makaburi yao, na alipofufuka, wakatoka pamoja naye. Walikuwa ni wale waliokuwa watendakazi pamoja na Mungu, na ambao kwa gharama ya uhai wao waliushuhudia ukweli. Sasa wangelikuwa mashahidi wake Yeye aliyewafufua kutoka kwa wafu.

Wakati wa huduma yake, Yesu alikuwa amewafufua wafu. Alimfufua mwana wa mjane wa naini, na binti akida na Lazaro. Lakini hawa hawakuvikwa kutokufa. Baada ya kufufuliwa, bado walikuwa na hali ya kufa. Lakini wale waliotoka makaburini Kristo alipofufuka, walifufuliwa kwa uzima wa milele. Walipaa pamoja naye kama ishara ya ushindi wake dhidi ya mauti na kaburi. Hawa, alisema Kristo, sio mateka tena wa Shetani; nimewakomboa. Nimewatoa makaburini mwao kama malimbuko ya uweza wangu. Ili wawe pamoja nami mahali nilipo, kamwe kabisa wasione mauti au kupata huzuni.

Hawa walioingia mji, na kuwatokea wengi, wakitangaza kwamba kristo amefufuka katika wafu, na sisi tumefufuka pamoja naye. Hivyo ukafanywa wa daima ukweli mtakatifu wa ufufuo. Watakatifu waliofufuka walitoa ushuhuda kwa ukweli wa maneno, "Wafu wako watakuwa hai tena, pamoja na maiti wangu watafufuka." Ufufuo wao ulikuwa kielelezo cha utimizo wa unabee, "Amkeni na kuimba, ninyi makaao mavumbini: maana umande wako ni kama umande wa mimea, na nchi itawatoa waliokufa" (Isaya 26:19).

Kwa muumini, Kristo ni ufufuo na uzima. Katika Mwokozi wetu uzima uliopotea kwa njia ya dhambi unarudishwa; maana anao uzima ndani yake ili kumfufua amtakaye. Anayo haki ya kutoa kutokufa. Uhai ulioutoa katika ubinadamu, aliutwaa tena, na kuutoa kwa wanadamu. "Nimekuja," alisema "ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." "Yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa yatakuwa ndani yake chemichemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele, nami nitamfufua siku yaa mwisho"(Yohana 10:10; 4: 14; 6:54).

Kwake aaminiye, kifo ni jambo dogo tu. Kristo anakizungumzia kama ni cha muda mfupi tu. "Kama mtu akilishika neno langu, hataona mauti kamwe," "hataonja mauti kamwe." Kwa Mkristo, kufa ni kulala, kitambo cha ukimya na giza. Uzima umefichwa na kristo katika Mungu, na "wakati Kristo, aliye uzima wetu atakapoonekana, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu" (Yohana 8:51, 52; Wakolosai 3:4).

Sauti iliyosikika kutoka msalabani ikisema "Imekwisha" ilisikiwa miongoni mwa wafu. Ilipenya kuta za makaburi, na kuwaamuru waliolala kuamka. Ndivyo itakavyokuwa wakati sauti ya Kristo itakaposikika kutoak mbinguni. Sauti hiyo itapenya makaburi na kuyafungua, na waliolala katika Kristo wataamka. Wakati wa kufufuka Mwokozi, makaburi machache yalefunguka, lakini wakati wa marejeo yake, wema wote waliokufa wataisikia sauti yake, nao watatoka kwa ajili ya uzima wa utukufu wa milele. Uwezo ule ule uliomfufua Kristo kutoka kwa wafu, utaamsha kanisa lake, na kulitukuza

pamoja naye, kupita mamlaka zote, kupita nguvu zote, kupita kila jina liitwalo jina, siyo tu katika ulimwengu huu, bali pia katika ulimwengu ujao.

Back cover
Upendo wa Mungu Ulihuisha

Lakini Mungu ni nani? Swali linaamshwa ndani ya kila moyo. Je ni mtawala katili na mwenye kulipiza kisasi, akituangalia bila huruma tukigaagaa katika taabu tulizojisababishia, bila juhudi yoyote kutusaidia, na mara nyingi akitupatiliza mapigo machache ili kuongeza maumivu zaidi katika hali yetu ya taabu? Je, Yeye ne nafsi? Au Mungu ni asili isiyo na nafsi inayotuzunguka kama hewa tunayovuta?

Katika Yesu Kristo siri ya tabia ya Mungu inafunuliwa katika ufahamu wa wote watakaomwangalia Yeye. "Aliyeniona mimi," alisema "Amemwona Baba." Angalia maisha yyake ya uponyaji wa huruma. Sikia maneno yake ya ukweli unaochoma. Amini katika tendo kuu la upendo wa Mungu uliodhihirishwa katika kujitoa kafara uhai wake. Katika yote, Mungu anadhihirishwa kama alivyo.

Yesu anathibitisha kwamba Mungu ni nafsi, aliye na upendo usio na upeo, na mwenye bidii kuokoa wadhambi. Katika "Upendo wa Mungu ulihuisha" utakutana na mvuto usio kifani wa maisha ya Kristo na kifo chake pamoja na uzuri dhahiri unaoeleweka kwa maneno yanayoonekana kama maelezo ya Sahidi aliyeona.

Published by:
Leaves of Life-International
P.O. Box 17
Mafinga Iringa Tanzania E. Africa